**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani. |

| | |
|---|---|
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake. |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |

| | |
|---|---|
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |

| | |
|---|---|
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 79.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 22 Oktoba, 2014**

*(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)*

## WIMBO WA TAIFA

## DUA

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua*

## KIAPO CHA UAMINIFU

Mheshimiwa Said Hassan Said.

*(Mheshimiwa aliyetajwa hapo juu alikula kiapo cha Uaminifu na kukaa katika sehemu yake ndani ya Ukumbi wa Baraza)*

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, karibu sana wewe sasa uko rasmi Mjumbe wa Baraza hili kupitia nafasi yako ya kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wote mumpe ushirikiano Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Said Hassan Said ili aweze kutekeleza majukumu yake katika chombo hiki akiwa ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Na wewe Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, nikuombe ushirikiane na Wawakilishi wenzio ambao wapo waliokupongeza sana mara baada ya kuapishwa kuwa Mjumbe wa Baraza hili, wanategemea sana kuwa utekelezaji wa shughuli zako utakuwa mzuri kwa mashirikiano makubwa ili hatimae ufanisi wa chombo hiki kupitia weledi wako na kazi yako kama Mwanasheria Mkuu usaidie sana katika shughuli za Serikali na shughuli zetu kwa ujumla kwa chombo hiki.

Karibu sana tayari umechukua nafasi yako na Wajumbe wako tayari kushirikiana nawe. Ahsante sana, karibu. *(Makofi)*

## TAARIFA YA SPIKA

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, ninazo taarifa mbili ambazo zinakuja chini ya wiki hii kwa shughuli hizi kama taarifa ya Spika, moja ni taarifa ya kawaida ya kazi na taarifa hii ni kama ifuatavyo.

Waheshimiwa Wajumbe, Katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Baraza la Nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 11 Disemba, 2013 hadi tarehe 20 Disemba, 2013, Baraza lilipitisha Miswada mitatu (3) ya sheria kama ifuatavyo:

1) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

2) Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Amri ya Barabara Sura 134 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

3) Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya Ukimwi Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu wanaoishi au walioathirika na Virusi vya Ukimwi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Baraza la Nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 22 Januari, 2014 hadi tarehe 5 Februari, 2014, Baraza lilipitisha Miswada miwili (2) ya sheria kama ifuatavyo:

1) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria za Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

2) Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Karafuu Nam. 11 ya 1985 na Kuweka Sheria Mpya ya Maendeleo ya Karafuu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Baraza la Nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 14 Mei, 2014 hadi tarehe 28 Juni, 2014, Baraza lilipitisha Miswada miwili (2) ya sheria ambazo ni:

1) Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

2) Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Billioni Mia Saba na Saba, Mia Nane na Ishirini na Tisa Millioni, Mia Sita na Arubaini Elfu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Siku ya Tarehe Thalathini Juni, Mwaka wa Elfu Mbili na Kumi na Tano na Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo Pamoja na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Kama inavyotakiwa chini ya Kifungu 90(3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2012, naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo sasa imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Waheshimiwa Wajumbe, hiyo ndio taarifa ya kwanza ya kazi mliyofanya katika mikutano mitatu mbali mbali ya Baraza hili.

Taarifa ya pili ya Spika, inahusiana na kifo cha aliyekuwa Spika, mstaafu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar Marehemu Ali Khamis Abdalla, kilichotokea tarehe 7 Septemba, 2014.

Waheshimiwa Wajumbe, Marehemu Ali Khamis Abdalla alizaliwa mwaka 1914 Nganani, Makunduchi na alikulia katika kijiji cha Ndijani na alipata elimu yake ya awali mwaka 1925 katika skuli ya Ndijani hadi mwaka 1928.

Baada ya kufaulu mitihani ya skuli ya msingi mnamo mwaka 1929 alijiunga na skuli ya Ben Bella *Government Boys School* hadi 1932. Baadae katika 1933 aliendelea na mafunzo ya Ualimu katika skuli hiyo hiyo ya Ben Bella na kutunukiwa cheti cha Ualimu. Marehemu alijiunga na Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda kwenye mwaka 1935-1941, katika fani ya Stashahada ya Kilimo.

Baada ya kurejea masomoni aliajiriwa kama Msaidizi Afisa Kilimo *Assistance Agricultural Officer* mnamo mwaka 1942. Ambapo mwaka 1952 aliteuliwa kuwa Meneja wa shamba la Serikali Kizimbani, pamoja na majukumu hayo aliendelea na kazi hizo za kilimo katika maeneo ya Chukwani na Selemu, Pemba hadi 1963.

Mwishoni mwa mwaka huo 1963 alichaguliwa kuwa Katibu katika Ubalozi wa Zanzibar nchini Misri na alitumikia kwa miezi minne (4) hadi April 1964 , baadae aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo hadi 1967 na mwaka 1968-1975 alifanyakazi katika mashamba ya mikonge Tanga.

Mnamo tarehe 21 Oktoba mwaka 1985 alichaguliwa kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi akiwa Spika wa pili toka kuanzishwa kwa Baraza hilo mwaka 1980 na alidumu na wadhifa huo hadi mwaka 1995.

Wakati wa uongozi wake akiwa kama Spika alikuwa na busara, hekma na jasiri katika kusimamia maamuzi ya chombo hicho cha Baraza la Wawakilishi ambacho ni chombo muhimu cha kutunga sheria na miongoni mwa baadhi ya mambo aliyoyasimamia ni haya yafuatayo:

Amefanikiwa kuliingiza Baraza la Wawakilishi katika Mabaraza ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola (*CPA*) na Chini ya Uongozi wake alifanikiwa vile vile kuendesha kikao ambacho kilichopitisha Sheria namba 15 ya mwaka 1992 iliyohusiana na mfumo wa siasa ya vyama vingi nchini Tanzania jambo ambalo limetengeneza historia kubwa nchini kwetu Tanzania.

Marehemu Ali Khamis hadi kufa kwake amejaaliwa kupata watoto 13 na wajukuu 39 na ameacha kizuka mmoja. Mungu awajaalie uvumilivu, watoto na wajukuu hao pamoja na kizuka aliyemwacha.

Marehemu alizikwa tarehe 8 Septemba, 2014 hapo shambani kwake Fuoni Zanzibar akiwa ametimiza miaka mia (100) ya uhai wake.

Mola amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Baada ya taarifa hiyo Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba tusimame kwa dakika moja ili kukumbuka mzee wetu huyo na kazi kubwa aliyoifanya katika nchi yetu.

*(Hapa Wajumbe walisimama kwa dakika moja ili kuomboleza)*

## HATI ZA KUWASILISHA BARAZANI

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niungane nawe katika kuendelea kutoa pole kwa marehemu aliyekuwa Spika wetu, Mzee Ali Khamis Abdalla namtakia malazi mema peponi. *Amin* na Mungu atujaalie na sisi tuweze kupita umri kama ambao yeye ameupata.
Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa Spika, Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 29 Juni, 2014. Naomba kuwasilisha Mheshimiwa Spika.

**Mhe.Spika**, Ahsante sana hati zimewasilishwa, naomba sasa nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Afya, naye awasilishe hati, tumpongeze Mheshimiwa Waziri wa Afya, anaanza kufanyakazi yake rasmi katika chombo hiki.Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria.

**MSWADA WA SHERIA YA WAUGUZI NA WAKUNGA, 2014**

**Mhe. Waziri wa Afya:** Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga Nam. 9 ya Mwaka 1986 na Kuanzisha Badala yake Sheria Mpya ya Wauguzi na Wakunga na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Spika naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba Kuwasilisha Mezani maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga Namba Tisa ya Mwaka 1986 na Kuanzisha Badala yake Sheria ya Wauguzi na Wakunga na Mambo mengine yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uwasilishaji wa hati kwa uwasilishaji wa hati hiyo. Katibu.

**MASWALI**

**Nam. 1**

**MLIPUKO WA BOMU ENEO LA DARAJANI**

**Mhe. Salim Abdalla Hamad -** Aliuliza:-

Mnamo siku ya Ijumaa ya tarehe 13/06/2014 kulitokea mlipuko wa bomu katika eneo la Darajani, kwenye majira ya saa 2:00 usiku.

a) Serikali imelichukulia vipi tokeo hili lenye kuhatarisha na kuvunja amani ya nchi hii tulivu.

b) Kutokana na utafiti uliofanywa bomu hilo ni la kutupwa au la kutengwa.

c) Serikali inaweza kueleza athari zilizotokezea kutokana na tukio hili na hatua gani madhubuti zimechukuliwa ili kudhibiti hali hiyo isijitokeze tena.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe suali lake Nam. 1 lenye vifungu (a), (b), (c) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, Serikali imesikitishwa sana na tukio la mripuko wa bomu lilitokea siku ya Ijumaa ya tarehe 13/6/2014 mnamo majira ya saa 2:45 za usiku, katika eneo la Darajani Mjini Unguja. Serikali imelani tukio hilo kupitia vyombo vya habari. Tukio hilo likiashiria kwamba baadhi ya wananchi wenzetu wanaendeleza vitendo vya uvunjifu wa amani visivyostahiki bila ya kujali uhai na maslahi ya wananchi na Taifa kwa jumla.

b) Mhe. Spika, jeshi la polisi Zanzibar limethibitisha kwamba bomu hilo lilikuwa la kutupwa.

c) Mhe. Spika, athari zilizojitokezea kutokana na tukio hilo ni pamoja na kifo cha mtu mmoja na watu saba wamejeruhiwa. Majeruhi walipelekwa kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Al-Rahma. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu hali zao zinaendelea vizuri na tunazidi kuwaombea wawe na afya njema.

Mhe. Spika, vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vimejipanga kukabiliana na vitendo vyovyote vya uhalifu nchini na vile vyenye kuhatarisha usalama wa nchi na wale wote watakaohusika na uvunjifu wa amani watachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, nawaomba wananchi wajiepushe na vitendo vyovyote vile vya uvunjifu wa amani katika nchi yetu ili tuendele kuishi kwa amani na upendo.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kupata nafasi hii ya kuuliza suali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, ninavyofahamu ni kuwa Zanzibar ni tafauti na kama ilivyokuwa kabla ya Mapinduzi, siku hizi wananchi hawaruhusiwi kumiliki silaha. Vitendo hivi vilivyofanywa vinaashiria kuwa kuna watu wanamiliki silaha

kinyume na sheria. Kwa sababu hiki si kitendo cha mwanzo ni msururu wa mambo unaoendelea unaohatarisha amani yetu na kwa sababu Zanzibar watu wanaingia tu bila ya kuwa na utaratibu maalum, hakuna *passport* wala hakuna lolote.

Mhe. Spika, hatuoni kuwa imefika wakati sasa kwa vile tumeshaona mambo yametokea huyuma, Zanzibar kubadilisha mfumo na kuona kuwa hakuna ule mtindo wa watu kuingia ovyo ovyo ambao unahatarisha amani yetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, ningeomba kidogo arudie pale mwisho sikumsikia vizuri lile suali lake. Maelezo nimeyasikia, lakini lile suali sikulisikia. Naomba akisema kidogo aelekeze kwenye spika zetu hizi kwa sababu ya eko.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa, rudia suali, maelezo ameyafahamu, lakini suali lenyewe.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mheshimiwa, suali ni kuwa kutokana na kuwa tumeshuhudia vitendo aina kwa aina vya uhalifu na kwa vile wananchi hapa hawaruhusiwi kumiliki silaha ikioneshea kuwa sio Wazanzibari wanaofanya hivyo, haionekani kuwa sasa wakati umefika Zanzibar kubadilisha mfumo wa uingizaji wa watu ili tuhakikishe kuwa hawaingii na mambo kama haya yanayohatarisha amani yetu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kila tahadhari inachukuliwa na Serikali yetu kupitia vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama ili kuhakikisha kwamba hali ya uvunjifu wa amani na vitendo vya uhalifu vinadhibitiwa. Lakini kadiri tunavyochukua jitihada hizo bado mbinu mbali mbali za wahalifu na wao wanatumia katika kutafuta mwanya na wao kufanya vitendo vyao.

Mhe. Spika, ni vizuri basi kwa kila wakati tukabuni mbinu mbali mbali katika kushughulikia mambo hayo.

Kwa hivyo, ushauri tunaupokea ili tuviarifu vyombo vya ulinzi na usalama kuzidisha mikakati na mbinu na kuchukua hatua katika kukabiliana na vitendo vya uvunjifu wa amani na vile vinavyoashiria kuhatarisha maisha ya wananchi wetu.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe.Spika, wakati Mhe. Waziri akijibu suali lake amesema kwamba waliofanya vitendo hivi ambao hawana nia njema huwa wanajaribu kutumia mbinu mbali mbali kila siku ili kuweza kufanya haya matukio na kufanikiwa kwa kiasi fulani.

Mhe. Spika, kwa kuwa wahalifu wanajaribu kutumia mbinu mbali mbali na kwa kuwa dunia yetu hivi sasa imepiga hatua kuweza kukabiliana na hizo mbinu za wahalifu kwa kuweka *system* za kisasa za mitambo ikiwemo kama mambo ya *city camera*. Je, Serikali ina mpango gani ya kuweka vyombo vya kisasa ili kuweza kuwabaini wale ambao wanafanya uhalifu na kuweza kuchukuliwa hatua baada ya matukio.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, Serikali ina mpango wa kuanzia katika Manispaa yetu ya Zanzibar kuweka hizo alama maalum ama taa maalum au *CCTV* kwa nia ya kudhibiti uhalifu katika nchi yetu. Hata hivyo, pale tutakapopata uwezo zaidi hatua hizo zitaendelezwa katika maeneo mengine. Vile vile, tutauchukua ushauri huu kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kuhakikisha tunachukua hatua mbali mbali ili kudhibiti uhalifu nchi hii na vitendo vyote vile ambavyo vinapelekea uvunjifu wa amani.

Mhe. Spika, kubwa ni kwa wananchi wenyewe kushirikiana na vyombo hivi vya ulinzi na Serikali yao katika kuhakikisha kwamba tunapambana na uvunjifu huu wa amani. Wanauvunja amani ni wananchi wenyewe, kama tutachukua hatua hizo kuwa madhubuti kushirikiana vizuri, naamini mambo haya hayatoweza kutokea.

**Mhe. Spika:** Suala la mwisho la nyongeza linakwenda kwa Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Ahsante Mhe. Spika, na kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri, suala moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Kwanza kwa kuwa ni kawaida inapotokea uhali wa aina hii jeshi la polisi huwa linafanya uchunguzi. Sasa, je, nini matokeo ya uchunguzi uliofanywa na jeshi la polisi katika kugundua hili. Namaanisha hawa waliofanya hili tendo ni watu wa aina gani? Ni Wazanzibari halisi au ni wageni wanaoingia.

b) Hali ya usalama inapotetereka katika nchi moja katika athari kubwa tunayoipata ni mtiririko wa watalii ambao ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Je, tatizo hili halikujitokeza.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, ukweli kwamba jeshi la polisi inapotokea vitendo kama hivi hufanya

uchunguzi na upelelezi, kwa nia ya kuwatambua wahalifu na kuwapeleka katika vyombo vya sheria ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mpaka sasa bado jeshi la polisi halijaweza kuwatambua waliofanya uhalifu huu na linaendelea kufanya upepelezi, mara baada ya kukamilika upelelezi huu taarifa tutazileta rasmi katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, suala linalohusu kushuka kwa utalii yanapotokea matendo haya ya uhalifu Mheshimiwa Spika, ni kwali kabisa kwamba kunapokuwepo na vitendo vya uhalifu na vya uvunjifu wa amani, vinaharibu sio tu biashara ya utalii, lakini pia, inaharibu suala zima la kuimarika kwa uchumi kwa nchi yetu. Msingi huu unasababisha kuzidi kupelekea kuwa katika hali ya umasikini. Kwa hivyo, ni vizuri sana na wananchi wote kushirikiana katika kupambana na vitendo vyote vya uhalifu na vile vyote vinavyoashiria uvunjifu wa amani katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nakubaliana naye kwamba yanapotokezea haya utalii huwa unashuka. Lakini kwa sasa hali yetu ya utalii inakwenda vizuri na mimi napenda nichukue fursa hii kupongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na watu wa Kamisheni ya Utalii katika suala zima la kuimarisha utalii nchini.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, ahsante sana kabla suala langu Nam. 64 halijapatiwa majibu na mimi naomba niungane na wenzangu kutoa mkono wa pole kwa aliyekuwa Spika wetu kwa Baraza hili Mhe. Shehe Ali, *Inshallah* Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema Peponi na famili yake waendelee kuwa wastahamilivu.

Baada ya utangulizi huo kwa heshima kubwa na unyenyekevu, naomba suali langu Nam. 64 lipate majibu hivi sasa.

**Nam. 64**

**Ujenzi wa Majengo ya Kisasa kwa Ajili ya Ofisi za Viongozi Wakuu (Ikulu Ndogo)**

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, katika kufanikisha kazi za viongozi wetu wakuu pamoja na kuwa karibu na wananchi wa mijini na vijijini, Serikali imeamua kujenga Ikulu ndogo katika kila mkoa wa Unguja na Pemba. Kwa kuwa nyumba hizi za Ikulu ndogo nyingi zao ni za kurithi na hivyo kukosa viwango vya kuweza kuwafanya viongozi wetu kufanyakazi zao kwa ufanisi pamoja na kupumzika vizuri.

a) Je, ni lini Serikali itajenga nyumba ya kisasa kwa aili ya Ikulu ndogo ya Mkokotoni na kuachana na ile ya sasa ambayo haina kiwango kwa ajili ya mapumziko ya viongozi wetu wakuu.

b) Ni lini Serikali italipatia ufumbuzi tatizo la uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanywa na bahari katika Ikulu ndogo iliyopo eneo la Fumba.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe, Saleh Nassor Juma wa Jimbo la Wawi, suala lake Nam. 64 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja iliunda Kamati ndogo iliyopewa jukumu la kutafuta eneo yaani *side* kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mpya ya kisasa ya mapumziko katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Mhe. Spika, hata hivyo, Kamati hiyo imependekeza kuwa badala ya kupata au kutafuta *city* mpya. Lakini wamependekeza kwamba nyumba ya mapumziko iliyopo Mkokotoni kwa uzuri wa *city* yake, basi ikabidhiwe Ikulu iweze kuiendeleza na kuwa ndiyo makaazi rasmi ya mapumziko kwa Mhe. Rais na viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa ambapo Ofisi yetu tayari imepanga kuifanyia matengenezo makubwa nyumba hiyo katika sehemu zake za ndani na nje pamoja na kuezeka upya paa la jengo hilo.

a) Mhe. Spika, kwa kuanzia katika mwaka huu wa fedha wa 2014/15, Ofisi imetenga jumla ya shilingi milioni 42 ambazo zilitarajiwa kutumika kwa kuanza kazi ya kuzungushia ukuta eneo hilo iliopo nyumba hiyo ya mapumziko.

b) Mhe. Spika, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora tayari imeanza kazi ya kulipatia ufumbuzi tatizo la uharibu mkubwa wa mazingira unaofanywa na bahari katika nyumba ya mapumziko ya Bwefumu pamoja na maeneo mengine yenye athari kama hizo katika nyumba za mapumziko za Kibweni, Mkokotoni na Mkoani.

   Mhe. Spika, katika hatua za awali Ofisi yangu tayari imekwisha andaa andiko la mradi mpya wa maendeleo unaojulikana kwa jila la ujenzi wa ukuta kudhibiti mmong'onyoko wa ardhi katika Ikulu ndogo za Mkoani, Bwefumu na Kibweni, ambao utaombewa fedha katika bajeti ya mwaka wa Fedha 2015/16. Fedha ambazo zitatumika

kurekebisha maeneo yaliyoathiriwa na mmong'onyoko wa ardhi, yaani kufanya *land exclamation* katika maeneo yote ya nyumba za mapumziko za Serikali zilizotajwa. Ahsante.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa heshima kubwa naomba kiti chako kinilinde kwa sababu mazungumzo yamekuwa mengi huku, tunashindwa hata kusikiliza vizuri majibu ya Serikali. Kwa hivyo, naomba kiti chako kijaribu kuangalia vizuri huku nyuma nyuma.

Baada ya maelezo hayo, Mheshimiwa kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu mno naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa juhudi iliyochukua katika kufanyia matengenezo baadhi ya hizo *state lodge*. Kwa kuwa viongozi hawa watatu kwa maana ya Mhe. Rais na Makamu wake wawili hawa kwa maana ya Makamu ya Kwanza na Makamu wa Pili wana kazi kubwa ya kuongoza nchi hii tena katika visiwa vyote viwili na mara nyengine hulazimika kutembelea hata katika kisiwa cha Pemba kule na inabidi walale kule.

Mhe. Spika, kwa kuwa Serikali kwa sasa imepanga utaratibu wa kuwakodia nyumba za watu binafsi katika maeneo maeneo tu hivi na kwa kuwa viongozi hawa wanahitaji mapumziko makubwa pale baada ya kufanyakazi za mchana kubwa za Serikali wanapokuwepo katika kisiwa cha Pemba pale na kwa kuwa kuna maeneo mazuri, yaani ya *county side* ya kile kisiwa ambapo kuna *beach* nzuri. Je, ni lini serikali itaachana na utaratibu huu wa Uswahilini kuwakodia Makamu wa Kwanza katika Uswahilini huku na kumuweka Makamu wa Pili pale kwenye fujo fujo Machomane pale.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa fupisha maneno uliza swali.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ndio ninakuja Mheshimiwa, ni lini Serikali itaacha utaratibu wake wa kuwaweka viongozi wetu hawa kwa maana ya Makamu wa Pili kumuweka katika ki-*lodge* pale Machomane na huyu Makamu wa Kwanza kumuweka hapa Mkoroshoni uswahilini hivi na kuwajengea makaazi ya kudumu katika *country side* ya Kisiwa cha Pemba ili waweze kuwatumikia wananchi vizuri.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Spika, lengo la Serikali ni kuwatunza viongozi wake wote wakuu hilo ndio lengo letu. Kama wewe Mheshimiwa Mwakilishi tunavyokutaka ukae katika nyumba ya maana

basi na wao ndio *number one* tunapenda na sisi swali limeuliza *rest house* ya Mkokotoni ndio swali. Lakini Serikali kwa ujumla nasema kwa kupitia Wizara husika mazungumzo ya Makamu wa Kwanza, Makamu wa Pili na wao Wizara wenyewe ndio wana jukumu hilo la kutafuta *side* kujenga makaazi mazuri kwa viongozi wao na Serikali Kuu ita-*support* mradi huo.

Pia, amezungumza Hoteli anayokaa Mhe. Makamu wa Pili, Hoteli anayokaa Mhe. Makamu wa Pili kuna *suite* pale maalum ile ya ina *status* ya *presidencial suite* na hiyo ndio Kimataifa, hata hii hoteli inayojengwa sasa Kempist kuna *presidencial suite* kama tano pale, Kilimanjaro kote ni jambo la Kimataifa hilo kwenda kukaa kwenye *state lodge* ni suala jengine, lakini kwa kweli ni jambo la kawaida. Kwa hivyo, si kama tunam-*undervalue* Makamu wa Pili la muhimu iko kwenye *standard* na tunahakikisha kwamba anakaa vizuri. Ahsante.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini baada ya kusema hayo nilikulaumu sana kutokana na kauli uliyopitisha Bungeni, 50 kwa 50 ukaweza kuninyima swali kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri, ni sababu gani ambazo zinasababishwa Ikulu zote kujengwa karibu na bahari.

Lakini (b) Serikali imelifanyia utafiti wa kina Ikulu ndogo iliyoko Fumba kutokana na maji ya bahari ambayo yanapita chini kwa chini hadi katika Ikulu ile. Ahsante.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa kweli kama swali la msingi lilivyouliza nyingi ya nyumba zile zilikuwa za urithi tokea hapo zamani, haidhuru kuna nyengine mpya tumezijenga kama Fumba nayo ilikuwa ya urithi. Lakini nataka kusema kwamba zaidi tunatizama uzuri wa sehemu, naamini uzuri wa *side* ya baharini kwa upepo wake mandhari yake ninafikiri inavutia zaidi kuliko kupata sehemu iliyoko katikati. Kwa hivyo, zaidi naangalia kimandhari, kivutio hiyo ndio sababu kubwa hapa na nafikiri hata mahoteli yetu mengi ya kitalii ukitembea Unguja na Pemba, mengi *locations* zake yako kwenye bahari yanavutia zaidi mandhari, nafikiri hiyo ndio sababu kubwa hasa.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi nimuulize Mheshimiwa swali moja la nyongeza lenye (a) na (b). Swali (a) katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri, hapa alisema kwamba wana mpango wa kutafuta eneo jengine katika Mkoa wa Kaskazini kujenga Ikulu ndogo. Mimi nilikuwa nimuulize Mhe. Waziri, ninavyokumbuka mimi

kulikuwa kuna kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ikulu ndogo kule Nungwi, sijui kiwanja kila kiko wapi.

(b) Katika majibu yake vile vile alitueleza kwamba wamepanga kujenga uzio katika Ikulu ndogo ya Mkokotoni ambapo imeshatenga kiasi cha milioni arubaini na mbili kwa mwaka huu katika bajeti yake. Mimi nilitaka kujua tu ni lini ujenzi ule utaanza na ni Kampuni gani ambayo wameipa ujenzi wa uzio ule.

**Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, kwanza naomba nisahihishe tu kidogo vile alivyozungumza Mhe. Mtando, kwamba hakunifahamu vizuri. Awali ile Kamati ndogo ilikuwa na azma hiyo ya kutafuta eneo la kujenga hiyo Ikulu, walifikiria kwamba labda ile Ikulu ndogo ya Mkokotoni haifai. Lakini ile Kamati baada ya kuranda wakaona *location* ya *side* ile ya Mkokotoni ni nzuri zaidi ndio wakaona bora tuboreshe kile kile kilichopo pale kuliko kutafuta *side* nyengine.

Kwa hivyo, si kama wanakwenda kutafuta *side* nyengine la la la, kwa hivyo, hiyo azma mwanzo ilikuwa hivyo. Lakini baada ya wao kuranda wee, wakatafakari wakaona ile ni bora zaidi, kwa hivyo, bora tuiboreshe ile tuiendeleze ile na kama nilivyosema fedha milioni 42 zimeshatengwa na nilisema mkakati wa kisheria yaani wa taratibu, kuna taratibu za kiserikali lazima tutafute tenda, tutafute nani turushe tenda tumtafute mjenzi, wewe mwenye Mjumbe wa Kamati yetu ya *PAC* tunaogopa tena usije ukatu-*query* mmempa tena nani bila ya kufanya taratibu. Kwa hivyo, tutafata utaratibu tuone tupate uhakika nani mjenzi apatikane. Ahsante.

**Nam. 53**
**Kujengewa Uwezo Vyuo vya Qur-an (Madrasa)**

**Mhe. Saleh Nassor Juma -** Aliuliza:-

*Tahfidhil Qur-an* ni moja ya juhudi kubwa zinazochukuliwa na madrasa zetu katika maeneo mbali mbali ya mjini na vijijini. Kwa kuwa walimu (*maustadh*) wa madrasa zetu kukabiliwa na changamoto ya gharama kubwa na zenye kuwazidi uwezo, hali inayopelekea kuhangaika kutafuta ufadhili kutoka kila pembe ya nchi, mara nyengine bila ya mafanikio.

Je, Wizara yako ina mpango gani endelevu wa kuendeleza utaratibu huu pamoja na kuzijengea uwezo madrasa zetu katika kufanikisha azma hii nzuri.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla sijajibu swali namba 53 kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Mwanasheria Mkuu, mpya Mhe. Said Hassan Said, si mgeni katika wizara yangu na alikuwa akitusaidia wakati wote katika shughuli zetu. Kwa hivyo, tutaendelea kushirikiana naye na tutasaidiana katika kujenga Taifa letu. Kwa hivyo, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, karibu sana.

Mhe. Spika, baada ya kwisha kusema hayo, naomba sasa nimjibu Mheshimiwa Saleh Nassor Juma wa Jimbo la Wawi swali lake namba 53 kama linavyofuata.

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba niseme tu kwamba Afisi ya Mufti wa Zanzibar chini ya Sheria ya Mufti Nam. 9/2001 Sheria za Zanzibar, ndio yenye mamlaka kisheria kusimamia Vyuo vya *Qur-an*. Wizara yangu kwa kupitia Afisi hiyo imeyaona hayo na inajitahidi kuvisaidia vyuo vya *Qur-an* kuendeleza elimu ya nchini. Wizara kwa kupitia Afisi ya Mufti na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana zinajitahidi kila mara kuwapatia misaada kwa ajili ya kuendeleza huduma hii nzuri. Kwa kuwa Bajeti inayotokana na Serikali ni ndogo Wizara yangu imezungumza na wafadhili mbali mbali na inaendelea na kuzungumza na wafadhili hao na pale haja inapotokea ambapo hutoa michango mikubwa kwa vyuo vyetu pamoja na walimu wake. Wafadhili hao ni pamoja na Uturuki, Saudia na Oman na wengineo.

Mhe. Spika, nia yao kubwa pale itakapowezekana ni kutoa kiasi cha fedha kwa kila madrasa ili madrasa hizo zianzishe miradi ya kujitegemea. Kwa kujua idadi kamili ya madrasa zote za Unguja na Pemba. Afisi ya Mufti wa Zanzibar imeanza na mchakato huo kwa upande wa Unguja kwa kushirikiana na wakuu wa wilaya na masheha. Aidha, fomu kutoka Afisi ya Mufti wa Zanzibar zimeshasambazwa kwa wahusika na zoezi la kuzikusanya fomu hizo linaendelea.

Aidha, suala la Serikali kutafuta mpango endelevu hili tumeshalijadili sana katika wizara yangu. Hata hivyo, kwa sababu hili ni suala kubwa ambapo tunavihusisha vyuo visivyopungua 2000 Zanzibar na Pemba na walimu wasiopungua 8000 wa vyuo hivyo, ni lazima kuchukua muda kidogo kuyatafakari yote kabla ya kutoa maamuzi ya vipi watasaidiwa walimu hao pamoja na vyuo vyao.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali dogo la nyogeza kama ifuatavyo:

(a) Kwa kuwa Serikali inaendeleza na jitihada za kutafutia ufumbuzi matatizo ya madrasa na walimu na kwa kuwa tatizo hili ni la kipindi kirefu sana hususan katika hali za madrasa, yaani madrasa zenyewe ziko hali mbaya na kwa kuwa walimu wamefanya bidii kujenga madrasa hizi,lakini madrasa nyingi zimekwama katika hatua, aidha ya kuezeka au katika hatua hata ya kuweka *floor* tu. Je, Wizara yake ni lini itaanza utaratibu kama ulioanzishwa na Wizara ya Elimu wa kuweza kuendeleza juhudi za wazazi pale napojenga mabanda ya shule na hatua wao kuendelea kumalizia. Ni lini wizara yake itaandaa utaratibu kama ule wa Wizara ya Elimu.

(b) Kwa kuwa walimu hawana hata lile posho la sabuni pamoja na jitihada walizofanya, ni lini hawa walimu wa madrasa watapatiwa angalau posho dogo tu la kupata sabuni ili waweze kufanya vizuri kazi zao.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, naomba aelewe kwamba yote hayo aliyoyazungumza lazima kuwe na bajeti, bajeti ya shughuli hizo wizara yangu haipo. Kwa hivyo, hata kama chuo au madrasa itafanya juhudi zake za kujenga mabanda, wizara yangu haichukui ahadi ya kusema kwamba tutamaliza madrasa ile. Wizara yangu inachofanya kwa kupitia Ofisi ya Mufti na Katibu Mtendaji, tunapotembelea katika maeneo haya na kama misaada tumepata tunawasaidia katika hali hiyo hiyo tuliyonayo na hilo tutaendeleza, lakini sichukui au hatutoi ahadi kwamba kila banda au kila madrasa tutaezeka au tutasaidia kukamilisha itakuwa hiyo ni ahadi ambayo hatuwezi kuitekeleza.

La pili, kama alivyosema hivi sasa kwa mujibu wa utafiti wetu na *registration* yetu kuna walimu wa madrasa wanaopita 8,000. Sasa ukisema kwamba kila mwalimu tumlipe ina maana ni mzigo kwa Serikali, walimu 8,000 ni fedha nyingi sana na hawa utizame hizi ni *private* sasa hatujiwezi kujiingiza katika masuala ya *private* tunachofanya Idara ya Mufti na Idara ya Wakfu tunasaidiana pale ambapo tunapata misaada. Kwa mfano kama nilivyosema tuna wenzetu Uturuki, Saudia na Oman wanatupa misaada ya vyuoni. Kwa hivyo, pale ambapo tunahisi kwamba kuna haja ya kusaidia kwa mujibu wa tarakimu tulizonazo, takwimu hapo tunasaidia katika misingi hiyo. Lakini hatuwezi kusema kwamba kila mwalimu ambao sasa ni zaidi 8,000 kwamba kila mwalimu atapata posho kutoka Serikalini hiyo haitawezekana.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, ninakushukuru na mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani, naomba nimpongeze sana Mhe. Mwanasheria Mkuu mpya ambaye leo tumeungana humu katika Baraza lako tukufu la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe.Waziri, swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b), amekiri hapa kwamba Serikali haina uwezo wa kusaidia

majengo ya madrasa na sababu kubwa ni tatizo la bajeti. Wizara ya Elimu wao walipoamua kusaidia shule walitenga bajeti kwenye wizara yao ni kwa nini wewe wizara yako haijaamua kutenga bajeti maalum kwa ajili ya kusaidia madrasa zetu, wakati mkijua kwamba Zanzibar asilimia 99 ni Waislamu na hivyo hivyo ukijua kwamba elimu ya dini ya Kiislam ndio msingi wa malezi ya Wazanzibari wote.

(b) Mara kadhaa katika awamu mbali mbali tumeshuhudia Serikali ikitoa motisha kwa vikundi vya sanaa mbali mbali ndani na nje ya nchi kuviwezesha kwa fedha na vifaa. Hivyo, kuna ugumu gani Serikali kutoa motisha kwa madrasa za Kiislamu Zanzibar. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hija maswali yake ya nyongeza. Vyuo vya *Qur-an* na madrasa ni vyuo vya kibinafsi na kama nilivyosema hivi ni vyuo vya kibinafsi ambavyo vinaanzishwa na kila mtu na ndio maana kwanza tukataka kuvisajili kujua kuna vyuo vingapi katika kuzuia mambo mengine ambayo yanatokea tokea.

La pili, usifananishe vyuo vya *Qur-an* na Skuli kwa sababu Skuli ni za Serikali, kwa hivyo, Serikali ina wajibu huo kwa sababu zile Skuli ni za Serikali. Sisi katika utaratibu huo wa Skuli, utaona kila Skuli kuna sehemu ambazo dini inasomeshwa. Kuna dini, *Qur-an* na mambo mengine. Kwa hivyo, unapokwenda katika sehemu za Serikali haya yanapatikana, lakini watu kwa ile hamu yao ya kutaka kuongeza dini wanaanzisha vyuo vya kibinafsi. Sisi Wizara yangu tunawapa motisha, motisha gani kuna misahafu tunatoa, kuna baadhi ya vyuo tunatoa fedha kuwasaidia. Kuna baadhi ya vyuo tunatoa hata mambo mengine tunawapa saruji, kutegemea misaada ambayo tunapata.

Kwa hivyo, hiyo nafikiri ni motisha kubwa ambayo tunatoa Serikali kwa kusaidia vyuo vyetu hivi vya madrasa na kama nilivyosema kwamba hivi sasa kuna walimu *registered* ni 8,000 na sasa tukisema tuwaingize huko kwanza itategemea *policy* ya Serikali mpaka suala lijadiliwe na mambo hayo. Lakini kwa sababu ni *private* sisi tunasaidia kwa upande huo.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, muda wetu kidogo leo umekuwa mfupi na shughuli zilikuwa ni nyingi, kwa hivyo, kwa swali hili tukomee hapa. Ninakushukuru Mheshimiwa. Tunaendelea.

Kwa heshima na taadhima kabla ya kuuliza swali langu, naomba uniruhusu kama dakika tatu au mbili tu nichukuwe fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein kwa uteuzi mdogo wa Mawaziri na Naibu

Waziri aliofanya hivi karibuni. Nimpongeze kwa dhati kabisa na hasa pale Wizara ya Kilimo ilipokuwa na misuko suko kutokana na Kamati yako uliyoiunda kwa vikao karibu sita mpaka vinane haijawahi kumuona Mhe. Waziri, ikikaimiwa tu na wakati mwengine hata kukosa waziri. Mhe. Mohammed Aboud, nilipokuwa nikichangia nikamwambia tena ishatosha mawazo na fikra zishachukuliwa kwa hilo.

Mhe. Spika, niendelee  kukushukuru wewe kwa dhati kabisa kwa juhudi zako na fikra za kuendesha Baraza hii na pia, kuwapongeza mawaziri walioteuliwa ikiwa Mheshimiwa Juma Duni Haji, maarufu babu kwa kupata wizara mpya na kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama chake. Vile vile, nichukuwe fursa hii kumpongeza Waziri wa Kilimo ambaye alikuwa Naibu Waziri hii inatokana na uwezo wake na utaalamu wake na ujuzi wake katika Baraza hili kupewa Wizara hiyo.

Vile vile, nataka nimpongeze Mheshimiwa Rashid Seif, kupewa wizara mpya, wizara ambayo ni wizara nyeti, wizara ambayo Mheshimiwa Rais, ameteuwa katika wizara yake ya mwanzo Wizara ya Afya na si kwa sababu tu imeanzia *alphabet* ya (a) ndiyo akaiteua, lakini anaijua vizuri Mheshimiwa Rais, wizara hiyo. Vile vile, nataka nimpongeze…

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa swali?

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mahamoud Thabit Kombo, rafiki yangu, jirani yangu hapa, lakini nataka kuwatoa Waheshimiwa Wajumbe, wasi wasi…

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa Jaku, nilizuia…

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Nijibiwe swali la wananchi.

**Nam 10**

**Kuvunjwa kwa Majengo ya Bandari ya Malindi Zanzibar**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub** – Aliuliza:-

Majengo ya Bandari ya Malindi ni miongoni mwa majengo yaliyopo eneo la Mji Mkongwe ambao umeingizwa katika urithi wa dunia na *UNESCO*. Hivi karibuni tumeshuhudia majengo hayo yakivunjwa na kubadilishwa sura yake asilia.

a) Kwa nini Serikali imeamua kuruhusu majengo hayo kubomolewa wakati ni kinyume na masharti ya uhifadhi wa Mji Mkongwe.

b) Hatua hiyo inasaidia vipi mipango ya kuendeleza na kuhifadhi majengo ya Mji Mkongwe ambao umepewa sifa ya kuwa urithi wa dunia.

**Mhe. Spika:** Haya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi, swali lake Nam. 10 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ililazimika kuchukua hatua za kuvunja majengo mawili yaliyokuwa sehemu ya mizigo katika eneo la bandarini, Bandari ya Malindi. Majengo hayo mawili ya mizigo ya bandarini yalivunjwa katika mwaka 2006 kutokana na Serikali kulazimika kuchukua hatua hiyo baada ya mjenzi kubadili mfumo wa ujenzi wa gati kutoka maumbile ya mvungu na kwenda maumbile ya ukuta ambapo eneo hilo lilitumika kwa ajili ya kujenga nanga za kufungia ukuta kwa gati mpya.

Mhe. Spika, katika mwaka 2013 majengo mawili ya bandarini katika gati ya abiria yalibadilishwa sura yake na kufanywa majengo ya abiria yaani kwa *passenger terminal* ambapo kazi hiyo ilifanywa kwa ushirikiano mkubwa na Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe ili kuhakikisha kuwa sheria na masharti ya uhifadhi wa maeneo ya urithi wa dunia yamefatwa kikamilifu.

Aidha, katika mwaka 2013-2014 Shirika la Bandari lilifanya matengenezo makubwa jengo lilokuewa *duty free shop* bandarini na kuibadilisha sura yake, kazi hii pia nayo ilisimamiwa na kuratibiwa na uhifadhi wa Mji Mkongwe.

Aidha, naomba ifahamike kwamba Serikali inapolazimika kuvunja moja wapo ya majengo yaliyomo katika eneo la bandari taratibu na masharti ya uhifadhi wa Mji Mkongwe ambao ni urithi wa dunia yanafuata kikamilifu kwa Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe kushirikishwa.

Mhe. Spika, jibu (a) Serikali hairuhusu majengo hayo kubomolewa bila ya sababu za msingi na ridhaa kutoka kwa mamlaka husika za usimamizi wa uendelezaji wa Mji Mkongwe.

b) Serikali itaendelea na jitihada za kuendeleza Mji Mkongwe kwa kutambua umuhimu wa uhifadhi wa mji huo na sifa kubwa kwa nchi yetu, lakini pia, ikiwa ndiyo kitovu cha kivutio cha utalii Zanzibar.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante, pamoja na majibu ya rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, tayari mmeshavunja mabanda kule ndani na pana ukuta tu uliobaki pale mbele ambao naona hauna faida yoyote kwa hivi sasa umeleta usumbufu pale wanapopanda abiria kuelekea Dar es Saalam au kutoka Dar es Salaam kuja Zanzibar ukuta ule mbele. Huo ni sawa sawa na mlango wa nyumba kufunga wa mbele na ukaacha mlango wa nyumba wazi, ni lini ukuta ule mtauondoa.

Hapa ulipokuwa ukijibu swali kipindi kilichopita aliuliza swali Maalim Saleh kwa niaba yangu, pana makalbi pale yanaudhi watu njia ile na ukasema mtatia angalau zebra leo inafika miezi sita au mwaka unakaribia. Ni lini mtaondoa makalbi yale kuondosha usumbufu kwa wananchi mkijua barabara zile zinachangiwa na wananchi na barabara ni mzigo haiwezi kusema mzigo ule unaendelea barabara kuchimbika. Lini baada ya kauli ya Serikali kutoa makalbi yale yataondolewa na hadi hii leo hayajaondolewa.

La pili, *duty free* imechukua karibu miaka 20 imekuja kujengwa juzi baada ya vishindo vya Wawakilishi humu ndani. Huoni hivi sasa ipo haja ofisi zilizomo ndani mule zikaboreshwa kwa kuhamia jengo lile.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, maswali mawili ya Mheshimiwa Mwakilishi; la kwanza, lilikuwa anaulizia ukuta uliobakia katika eneo la *terminal* na la pili, alikuwa anaulizia makalbi. Sasa hili la ukuta kama maelezo yetu ya awali tulivyoyasema kwamba tumebadilisha majengo ambayo hivi sasa yanatumika kama eneo la *terminal* na masharti ya wenzetu wa Mji Mkongwe walitwambia kwamba ukuta ule uendelee kubaki kwa sababu ukuta ule ndiyo unaoonekana na ndiyo unaotoa hiyo haiba ya Mji Mkongwe kwa mtu ambaye anapita katika eneo husika. Kwa hiyo, kukwambia ukuta lini tutauvunja, hatutauvunja bila ya idhini na maelekezo kutoka kwa wenzetu wanaosimamia sheria na uhifadhi wa Mji Mkongwe.

Mhe. Spika, suala la makalbi, ni kwamba makalbi yale yaliwekwa kwa tatizo maalum ambapo ilitokana na barabara kufungwa eneo la Shangani kule,

ambapo kulikuwa bado harakati za ujenzi zinaendelea. Hivi sasa eneo lile limefunguliwa, lakini kufunguliwa kwake kimefunguliwa kipenyu bado nafasi ni ndogo ya kupita. Kwa hiyo, tunaamini kwamba nafasi ile ya ujenzi ule utakapokamilika eneo lile lilikuwa linatumika lote kwa ajili ya kupita magari na makalbi hayo tutaondosha ili waendelee watu kupata huduma kama ilivyokuwa awali.

Suala la pili, aliuliza suala la *duty free* hivi sasa Mhe. Spika, tayari jengo ambalo lilikuwa na *duty free* linatumiwa na maafisa wa shirika la Bandari kwa ajili ya kazi zao. Takribani watu wote wanaofanya kazi za *operation*, ofisi zao zimehama wamehamia katika jengo hilo. Kwa hiyo, jengo lile hivi sasa tayari linatumika.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, nashukuru sana na mimi leo hii kuweza kumuuliza swali zuri Mhe. Waziri, pamoja na majibu yake Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja ambalo ni zito sana. Mhe. Naibu Waziri, ulisema na umekiri kama ni kweli tumo katika mkataba wa *UNESCO* katika hali ambayo mazingira ya wenzetu ya mji kuweka uzuri wa urithi.

Lakini vile vile, Serikali inataka kutafuta uchumi kwa kuona nyinyi kutanua ile bandari ili kupata uchumi endelevu. Je, Mhe. Naibu Waziri, huoni ni kukiuka mkataba ambao uliowekwa na Umoja wa Mataifa wa *UNESCO*.

Lakini pili, ni hatua gani ambayo ni *fine* tutaweza kupigiwa kutokana na kuvunja mkataba huo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kama nilivyoelezwa katika majibu mama kwamba mabadiliko yote ambayo yatafanyika katika eneo la Mji Mkongwe, mabadiliko hayo hayatopata baraka na hayatofanikiwa kabla ya wasimamizi wa sheria za Mji Mkongwe kutoa idhini yao. Tunaamini kwamba wao wenyewe hawatoruhusu mabadiliko hayo kabla ya wao kuwasiliana na vyombo vinavyohusika ikiwemo *UNESCO*. Siamini kama Serikali itakuwa sehemu ya kushiriki katika kuvunja mkataba baina ya Serikali ama taasisi husika pamoja na *UNESCO*, ninachokiamini mabadiliko hayo yatakuwa na baraka kutoka katika vyombo husika vya hapa ndani pamoja na vyombo vya Kimataifa kwa kutambua wote lengo letu ni moja kutaka kuenzi na kuuendeleza Mji Mkongwe kama sehemu ya urithi wa ulimwengu.

**Nam. 2**

**Deni la *ZFA* katika Hoteli ya Bwawani**

**Mhe. Nassor Salim Ali** – Aliuliza:-

Kwa kuwa chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) kwa muda mrefu tokea kihamishe ofisi zake kutoka katika Hoteli ya Bwawani, kimekuwa na uhaba wa samani na mafaili yao hivi sasa yamewekwa chini ya sakafu kutokana na kuzuiliwa vyombo na samani zao katika hoteli hiyo. Hali hiyo imetokana na chama hicho kushindwa kulipa deni wanalodaiwa na Hoteli ya Bwawani, ambalo ni zaidi ya shilingi milioni nane. Je, wizara imechukua juhudi gani kulipatia ufumbuzi tatizo hilo.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi, swali lake Nam. 2 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, sikweli kwamba Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) kimehamishwa kwenye ofisi yake iliyokua katika Hoteli ya Bwawani. Kilichofanyika ni kwamba *ZFA* ilikuwa imekodi ofisi kwenye Hoteli ya Bwawani, lakini ilikuwa hailipii kodi yake na baadaye yenyewe iliamua kuhama kwenda kukodi nyumba nyengine huko Kiembesamaki.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo, uongozi wa Bwawani uliamua kuzuia samani za chama hicho ili kuitaka *ZFA* kulipa deni wanalodaiwa. Uamuzi huo wa Bwawani ulifanyika baada ya *ZFA* kutaka kuhamisha vifaa vyao kinyemela bila kufuata utaratibu, iliamua kutoka na mali au vitu kinyume na utaratibu wa kihoteli.

Mhe. Spika, juhudi zilizochukuliwa na Wizara ya Habari, Utalii na Michezo katika kulipatia ufumbuzi tatizo hilo ni kuwataka *ZFA* walipe deni hilo. Aidha, wizara imeishauri *ZFA* wakae pamoja na uongozi wa Bwawani kuangalia watasuluhisha vipi tatizo hilo.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kuhusiana na swali hili la deni la *ZFA* la Hoteli ya Bwawani.

Mhe. Spika, *ZFA* ni chombo ambacho kinajiendesha wenyewe, lakini kutokana na hali halisi ya uwezo wa kujiendesha imefikia wakati *ZFA* inaendesha shughuli zake kwa matatizo na kutokana na hali hiyo ipo haja ya

kuingalia wizara suala hili, ili *ZFA* kuweza kuvipata vile vyombo vikiwemo vitu vya samani kama vile meza, viti na vitu vyengine ili kuweza kuendesha shughuli zake za kiofisi.

Je, wizara haioni kwamba ipo haja kuiamuru Hoteli ya Bwawani kuvipatia *ZFA* vyombo vile ili kuendesha shughuli zake na kwa vile *ZFA* huwa inapata ruzuku kutoka Baraza la Michezo kuweza kuikata kidogo kidogo deni lile kupitia ruzuku hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, Mheshimiwa Mwakilishi, nakubaliana na wewe najua wewe ni mdau mkubwa wa michezo, lakini nakuhakikishia sisi wizara pamoja na Meneja wa Hoteli ya Bwawani na *ZFA* tutakakaa pamoja ili kulitatua tatizo hili.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri, swali la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Spika, *ZFA* ni Chama cha Mpira wa Miguu na kinatuongoza Zanzibar nzima na ni chama kikubwa na ni tegemeo kwa wanamichezo kwa Zanzibar na chama hiki kwa sababu kinapata misaada ya kila aina na kinachotegemewa kuendesha michezo, leo kuenda kukodi nyumba ikawa mpaka leo hii hawalipi kodi za watu mpaka kufika kuchukuliwa vitu vyao. Je, hawaoni kama kuna haja sasa chama hiki kujenga jengo lake la ofisi zake na kukaa kama hawana ofisi mpaka kushikiwa vyombo vyao ni kutia aibu kwa Serikali yetu ya Zanzibar kwa sababu ni chama kikubwa cha michezo na ni lini watajenga jengo lao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Mhe. Spika, ahsante, Mheshimiwa Mwakilishi, kitu chochote kile unatakiwa uwe na busara na uweze kukitafuta na sio kwamba *ZFA* hawapati misaada, wanapata lakini kiwanja kipo na tuna tegemeo kubwa watajenga na wawe na ofisi yao na wao waweze kutulia na waweze kufanya shughuli zao za michezo kama kawaida.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, mniwie radhi muda hauturuhusu Mhe. Naibu Waziri, nakushukuru, tunaendelea.

**Nam. 46**

**Elimu ya Kilimo cha Umwagiliaji kwa Njia ya Matone kwa Wakulima**

**Mhe. Saleh Nassor Juma –** Aliuliza:-

Kwa kuwa mabadiliko ya tabia ya nchi bado yanaendelea kukwaza sekta mbali mbali za kiuchumi ikiwemo kilimo na kwa kuwa ukosefu wa mvua ni

moja ya athari za mabadiliko ya tabia ya hali ya hewa (*Climatic Changes*) na kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji maji kwa njia ya matone (*Drop Irrigation)* ni nzuri, yenye tija na haihitaji maji mengi na yenye gharama nafuu.

Je, ni kwa kiasi gani Serikali imetoa taaluma kwa wakulima pamoja na kupeleka wataalamu vijijini kuelimisha aina hii ya umwagiliaji mazao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 46 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Umwagiliaji kwa njia ya matone ni utaratibu wa kumwagilia maji taratibu kwenye udongo kwa kutumia vyombo maalum kwa kunyunyizia maji kwenye sehemu iliyochaguliwa kufuata mistari inayotoa maji, vinyunyizo hivi huwekwa juu ya ardhi au kufukiwa chini ya ardhi.

Faida za umwagiliaji huu hupunguza upotevu wa maji, kwani hulenga pale tu panapo mmea unaohitaji kumwagiliwa na maji hupenya vizuri ndani ya ardhi, husaidia kupunguza na kuyayusha chumvi kwenye mmea na hupunguza uotaji wa magugu.

Kwa kuzingatia faida za utaratibu huu wa umwagiliaji maji, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili imeanza kuchukua hatua rasmi ya kushajihisha matumizi ya aina hii ya umwagiliaji pamoja na kupeleka wataalamu vijijini kuelimisha aina hii ya umwagiliaji.

Wizara kwa kushirikiana na wawekezaji washirika wa maendeleo, wanaotoa huduma kwa wakulima, miradi ya kijamii na sekta binafsi ambayo imeonesha utayari wa kutumia njia hii hasa katika kuongeza uzalishaji wa mazao yenye thamani kubwa hasa mboga na matunda.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili pia inashirikiana na Shirika la *USAID* kupitia mradi wa *TAPP* na *TAHA* kuanzisha kituo cha mafunzo na maonyesho ya ukulima bora wa mboga kwa kutumia teknologia za kisasa ikiwemo umwagiliaji maji kwa njia ya matone hapo katika chuo cha kilimo Kizimbani.

Kituo hiki kitatoa fursa kwa wakulima na wadau wengine wa kilimo kijifunza juu ya mbinu bora za ukulima kwa kutumia teknolojia za kisasa kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo ili hatimae waweze

kuongeza kipato na kuinua hali ya maisha kama ilivyo dhamira ya Mapinduzi ya Kilimo hapa nchini.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, ahsante sana, kwa heshima kubwa naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza Mhe. Naibu Waziri. Kwa kuwa *drop irrigation* ni mkombozi wa wakulima wadogo wadogo na kwa kuwa miundombinu ya kuweza kufanya umwagiliaji wa matone ni ghali sana ikiwemo uchimbaji wa visima na zile *pipes* kuzipitisha kule.

Na kwa kuwa wanawake wameekeza sana katika jimbo langu kwa mfano wanawake walioko Gombani ya Kati, wanawake walioko Vitongoji pale uwandani, walioko Vumba, walioko Wawi hapa Mji wa Chini pamoja na Furaha wameekeza sana katika kulima mboga mboga, lakini tatizo lao ni *capital* ya kuweza kufanya hiyo *drop irrigation*. Je, ni lini Serikali itawapa kupitia vyombo vya fedha, itatoa mkopo kwa wakulima hawa wenye masharti nafuu, kusudi waweze kuwekeza na wao katika *drop irrigation* na hatimaye kujikomboa kimaisha akina mama wa jimbo langu la Wawi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, kama nilivyosema Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inawasaidia wakulima ili kujiimairisha katika mfumo huu wa kilimo cha umwagiliaji. Wakulima wa jimbo la Wawi katika sehemu yake kama nilivyosema tuna mradi huu wa TAHA, na mradi huu tunatarajia kufika katika maeneo yote ili kuwagomboa wakulima hawa, lakini suala la kuwakopesha wakulima hawa mpaka tukae pamoja na washirika wetu wa maendeleo, nadhani kuna mbinu ambazo sisi tunazozitumia kama Wizara ya Kilimo ni kutoa taaluma tu ndio msaada wetu mkubwa kwa wakulima hawa.

Kwa hivyo, suala la kuwakopesha hatuwezi tukatoa jibu rasmi, kwamba tuwakopeshe wakulima juu ya suala hili, mpaka tukae tufikirie. Tunachokifanya katika Wizara yetu ni kutoa taaluma kwa wakulima.

**Mhe. Bikame Yusuf Hamad:** Mhe. Spika, kwa kuwa suala la umwagiliaji maji ni suala muhimu sana hasa katika mabadiliko ya tabia nchi na ukosefu wa mvua. Sasa je, Wizara yake ina mpango gani wa kujengwa mabwawa ili wakulima waweze kufaidika na uvunaji wa maji ya mvua hayo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, wizara yangu tuna washirika wa maendeleo wa Korea ambao tumeingia katika suala la *Irrigation* katika mabonde mengi ya Unguja na Pemba. Katika suala hili la ujengwaji wa Mabwawa pia tuna mpango wa kujenga mabwawa hasa katika eneo la Kilombero na Cheju ndio mwanzo tutakapoanzia.

**Nam. 4**
**Ahadi ya Ujenzi wa Eneo la Kusubiria Kuangalia Wagonjwa Hospitali ya Mnazi Mmoja**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Aliuliza:-
Mhe. Spika, suala hili nauliza namba 4 suala zito kwa wananchi wanyonge wa visiwa hivi, nimelihangaikia jua na mvua suala hili, na inapokuja neema haichagui na inapokuja dhoruba ya Mwenyezi Mungu haichagui aliyekuwemo na asiyekuwemo. Naiomba Serikali kwa suala hili iwe makini kuja kujibu suala hili. Niko tayari kuheshimu masharti ya Serikali, suala hili ni nyeti kwa wananchi, pale hapapikwi pilau wala biriani wanakuja kwa shida, Serikali iwe na jibu muafaka kwa suala hili.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:**Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia leo kuwepo hapa tukiwa hai na wazima.

Pili, nachukua fursa hii adhimu sana kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa imani yake juu yangu mimi binafsi kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Afya, lakini pia kwa imani yake kubwa kwa wananchi wa jimbo la Kiembe samaki ambao wao ndio wamenifikisha katika Baraza hili Tukufu.

Mhe. Spika, sasa naomba kwa mara ya kwanza kabisa kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya nijibu swali namba 4 la Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni Mhe. Jaku Hashim Ayoub, lakini kabla sijajibu swali hili naomba nimpongeze Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa ufuatiliaji wake wa karibu katika masuala mbali mbali yanayohusiana na Wizara ya Afya, pia amekuwa chachu ya ubunifu na changamoto mbali mbali ya huduma zote ambazo tunazitoa kwa wagonjwa pamoja na wauguzaji wao.
Naomba Mhe. Spika, kwa swali nililoulizwa kwa niaba ya Mhe. Waziri nijibu kama ifuatavyo;

Ni kweli kabisa kwamba mnamo tarehe 27/6/2014 katika Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi Maji na Nishati ambayo iliwasilishwa na Mhe. Ramadhan Abdalah Shaaban ilionesha ramani ya ujenzi wa eneo la wananchi kusubiri kuwaona wagonjwa wao, na pia kwa nyakati za usiku ambao wanatumia maeneo hayo kupumzika hasa wale ambao wanatoka mbali nje ya mji kutoka shamba.

Ramani hiyo nimekuja nayo ipo hapa leo, ila naomba kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba taratibu za ujenzi wa eneo hilo la kusubiria wagonjwa zipo hivi sasa katika hatua nzuri. Sisi kama wageni tulipoingia tumezikuta

hatua zimeshaanza na bahati nzuri tumezichukua zile hatua na tukaziendeleza kwa kuwasiliana na mamlaka mbali mbali ikiwemo mamlaka ya Mji Mkongwe, tayari kibali cha awali kimeshatolewa cha ujenzi wa eneo hilo ambapo pale pana bustani mbele ya hospitali kutokana na hii ramani iliyotolewa.

Lakini hivi sasa tumeshaanza pia mazungumzo na wafadhili mbali mbali pamoja na Serikali yenyewe, na pale kibali rasmi kitakapopatikana kutoka Serikali basi ujenzi huo utaanza mara moja. Naomba kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba Mwenyezi Mungu akitujaalia mpaka mwezi wa sita au wa saba wakati wa bajeti kazi hii tutakuwa tumeikamilisha. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:**Mhe. Spika, pongezi alizonipa Mhe. Naibu Waziri nimshukuru kwa dhati kuliona hilo na naomba nimuhakikishie wengi wa Baraza hili waliofikiria mimi nina ugomvi na Mhe. Naibu Waziri, lakini mimi ni mmoja wa wafuatiliaji wa Wizara ya Afya na nitaendelea, isijekuonekana kwamba nimemshikia mtu tu Naibu Waziri humu kwa kuwa labda nataka kumuuliza maswali mengi lakini mujue naijenga Wizara.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo mengine hayawezi kuyaona yote Wizarani, itabidi tumsaidie sisi. Kwa hiyo Mhe. Naibu Waziri tutashikiriana kwa hali na mali kukusaidia kwa maswali mengi kukujenga uwezo zaidi, isijekuonekana kama nina ugomvi na mtu, na Wajumbe walifahamu hilo pamoja na wananchi.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, Hospitali ile hivi sasa inakaribiwa na mvua za masika huko mbeleni na wananchi wanazidi kuendelea kuteseka pale, mvua, baridi hawana pa kwenda kama vile munavyojua pale hapatolewi sadaka wala chakula, wanakuja kwa shughuli maalum. Kwa nini sasa hivi kwa dharura hii musiyaondoshe yale ma- *files*, wananchi wale wakaenda pale walipokuweko mwanzo sijui umenifahamu Mhe. Naibu Waziri.

Wakoloni walipojenga Hospitali ile waliweka sehemu makusudi ya kusubiria wagonjwa wakija pale kujificha mvua ambapo sasa hivi Wizara imeweka *files*.

(a) Kwa nini musiondoshe mpaka mutakapokuwa tayari.

(b) Uzoefu wangu unanionesha mimi Wizara ya Afya si wafuatiliaji, nilikuwa na makamu wangu Mhe. Hija Hassan Hija kuna dawa zinaharibika kule Maabara Kuu Mnazi Mmoja hazipo.

Kwa hiyo, baada ya kushauriana na wenzangu humu ndani kama Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Panya tumekubali Serikali ipo itoe kauli..

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa muda unakwenda tunaomba swali lako ili ajibu muda umebakia dakika mbili tu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Tujenge banda la dharura pale mpaka Serikali itakapopata fedha, tuweke mabati kule kama 200 na maboriti tutaweka nje kwa dharura. Serikali itakapopata hizo hoja tutalivunja na tupo tayari Wajumbe wengi wameshanishauri watachangia laki moja moja kwa hilo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Pale Mhe. Spika, lile ni eneo la Mji Mkongwe huwezi kuweka maboriti na mabati kama tunavyojenga banda la gereji kwengineko.

Kutokana na ramani iliyotolewa ni ujenzi unatakiwa kufanyika kitaalamu ambao usiingiliwe na ile hadhi ambayo imeshakubaliwa kiulimwengu ya Mji Mkongwe. Hivi sasa wagonjwa wanasubiri eneo lile la mbele pale ukiingia tu Hospitali Kuu kuna maeneo yaani kuna benchi za saruji.

Eneo analosema Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba kuna ma-*files* yamewekwa hilo eneo tumelitembelea na hivi sasa tunafanya utaratibu wa kuhamisha yale ma-*files* ku-*computerise* kuondosha makaratasi na kugeuza *records* zote zile ziwe kwenye *computer,* ile yale ma-*files* yaweze kuondoshwa kabisa yasiweko eneo lile, na eneo lile litatanuliwa zaidi kwa wagonjwa kujihifadhi kwa kipindi hiki wakati tunafanya utaratibu wa kuwajengea eneo maalum la kukaa wauguzi wa wagonjwa.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana muda wa maswali umemaliza Mheshimiwa tunakushukuru.

## Hoja za Serikali

## Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga (Uanzishwaji wa Baraza la Usajili wa Wauguzi na Wakunga namba 9 ya mwaka 1986).

*(Kusomwa kwa mara ya Pili)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamkaribisha Mhe. Waziri wa Afya ili asome mswada uliopo mbele yetu kwa mara ya pili.

Naomba tutambue kuwepo kwa wanafunzi kutoka Chuo cha Sayansi ya Afya Mbweni wa Kada ya Uuguzi ambao jumla yao ni wanafunzi 30 wakiongozwa

na ndugu Ramadhan Soud ambaye ni Rais wa wanafunzi hao; naomba wasimame tutambue kwamba wamekuja.

Wamekuja kufuatilia kwa karibu sana Mswada huu na wao ndio wadau wa mswada huu, ili wajue hatima yao itakuwa vipi baada ya Baraza hili kuujadili kwa makini na hatimaye kuupitisha kwa ajili ya wauguzi hao. Karibuni sana ndugu wanafunzi, mswada wenu uko mezani punde tu mutamsikia Waziri wa Afya akiwasilisha na Wajumbe kuujadili mswada huo. Karibuni sana. Sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Afya.

**Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:** Mhe. Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai, uzima na *taufiq* ya kufika hapa.

Pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii kwa niaba ya Wizara ya Afya kusoma kwa mara ya pili Mswada huu wa Sheria. Naomba kwa ruhusa yako kabla sijasoma nichukue dakika moja na nusu kutoa shukurani zangu za dhati mimi pamoja na Naibu Waziri wa Afya na Waziri wa Afya kwa kazi nzuri ambayo tumeikutia na moja ya matunda yao ni kusomwa kwa mswada huu leo ambapo sisi tumekuja tumeukuta.

Kwa hivyo, tunawashukuru sana kwa kazi nzito waliyoifanya, na juhudi kubwa waliyoionesha, ni juu yetu na Wajumbe wote kuwatakia mafanikio mazuri katika kazi zao mpya walizopewa.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wauguzi Wakunga namba 9 ya mwaka 1986 unafutwa na kuanzishwa badala yake Sheria mpya ya Wauguzi na Wakunga na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, Mswaada huu unakusudia kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga namba 9 ya mwaka 1986 kwa lengo la kuanzisha chombo kitachokidhi hali halisi ilivyo na mabadiliko mbali mbali yaliyotokea katika Wizara ya Afya.

Sheria ya mwaka 1986 ilikuwa imepitwa na wakati hususan pale mwaka 1999 yalipokuja mabadiliko makubwa katika sekta ya afya. Mhe. Spika, mabadiliko ya Sera ya Afya. Mnamo mwaka 1999 Serikali ilifanya mabadiliko ya Sera ya Afya iliyotilia mkazo suala la kuwepo kwa mashirikiano ya utoaji huduma za afya baina ya taasisi binafsi pamoja na kufungua milango kwa taasisi binafsi kuweza kuingia katika soko la utoaji huduma ili kuipunguzia mzigo Serikali, wakati huu ndipo ilipoanza *Public Private Partnership*. Kutokana na utelekezaji wa sera hii wadau wengi walijitokeza na kuanzisha taasisi za kutoa

huduma za kiafya, za binafsi pamoja na za kufundisha taaluma za Uuguzi na Ukunga.

Mhe. Spika, migororo ilijitokeza juu ya suala zima la usajili wa taasisi hizo baina ya Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya kutokana na kutoelezwa bayana kwa kipengele kinachohusiana na uwezo wa kusajili mafunzo hayo katika sheria hii inayotumika. Ingawaje Baraza lina jukumu la kusimamia mafunzo ya taaluma hizi.

Kutokana na Sheria za Usajili kwa taasisi za Elimu, ni kuwa hakuna mafunzo yoyote yatayotolewa katika nchi bila ya kusajiliwa na Wizara ya Elimu isipokuwa kama kuna kipengele mahususi cha Sheria ambacho kinaondoa uwezo wa Wizara ya Elimu katika usajili huo. Hivyo kuna haja kuweka bayana mipaka ya kiutendaji juu ya usajili wa taasisi binafsi zinazotoa taaluma hizo, na ni juu ya nani mwenye dhamana ya kufanya usajili huo.

Mhe. Spika, kupatikana kwa hospitali binafsi kumeongezea haja ya kuwa na wauguzi na wakunga wa ziada kufanya kazi katika hospitali hizi jambo ambalo linalazimisha pia wawe ni sehemu wa Wauguzi kwa jumla wenye kufuata maadili na miiko ya kazi zao. Hivyo mabadiliko ya Sheria hii yatatoa fursa ya kufanya uangalizi na ufuatiliaji kwa wauguzi na wakunga wote wale wanaofanya kazi katika Sekta ya Umma na binafsi, kwa upande mwengine na wao pia watapata kushiriki katika kujenga hadhi  na maadili ya kazi zao.

Mhe. Spika, mabadiliko ya ukuaji wa kiuchumi na kuongezeka mahitaji ya kijamii yanatokana na ongezeko la watu na mabadiliko ya kimazingira ikiwa ni moja ya mahitaji ya jamii katika kukuza soko la huduma za Afya yaani *Health Marketing*, na kutoa fursa kwa watu binafsi kujitafutia ajira na kuinua hali za wananchi kiuchumi. Sheria hii itatusaidia kutupa miongozo ya kuweza kudhibiti taasisi zote ambazo zinatoa huduma ya kutimiza masharti yaliyowekwa ndani ya Sheria hii.

Mhe. Spika, kutanuka kwa taaluma ya wauguzi na wakunga katika taasisi binafsi na za Serikali kumepelekea Sheria iliyopo sasa kutokidhi mahitaji ya kuhakikisha ufanisi mzuri wa kulipa mamlaka Baraza kusimamia kikamilifu utendaji wa taasisi hizo. Hivyo kutungwa kwa Sheria hii mpya kumeangalia dhima ya kudhibiti fani hizi kwa kuingiza masuala ya ukaguzi wa hospitali, vyuo na taasisi zote zinazoajiri wauguzi na wakunga waliokuwa pengine hawana sifa, ambao wanafanya udanganyifu wa vyeti pamoja na wanafunzi ambao wameajiriwa hususan kwenye taasisi binafsi bila ya kumaliza masomo yao ambapo ni kinyume na taaluma za afya.

Mhe. Spika, mswada huu umegawika katika sehemu kuu Tisa (9).

Kwanza utangulizi ambapo jina la sheria kuanza kutumika pamoja na tafsiri ya baadhi ya maneno yatakayotumika katika sheria hiyo.

Sehemu ya pili inahusiana na uanzishwaji wa Baraza la Wauguzi na Wakunga ambapo ndani yake imeainisha Kazi za Baraza la Wauguzi na Wakunga.

Sehemu ya tatu; Uongozi na Wafanyakazi wa Baraza ambapo ndani yake yameelezwa masuala yanayohusiana na uteuzi wa Mrajis wa Baraza na kazi zake.

Sehemu ya nne; Usajili na Utoaji Leseni. Ndani ya sehemu hii imeelezwa mambo yanayohitajika katika kukamilisha taratibu za usajili na utoaji leseni.

Sehemu ya tano vifungu vinavyohusu nidhamu. Sehemu hii inaeleza utaratibu wa kusikiliza malalamiko ya Baraza na kufanya uchunguzi, utaratibu wa kukata rufaa, uwezo wa kuchukua hatua za kinidhamu na kutafuta usajili na urudishwaji wa vyeti.

Sehemu ya sita vifungu vinavyohusu fedha. Sehemu hii inaelezea vyanzo vya fedha, udhibiti wa fedha, ukaguzi wa hesabu na utaratibu wa kulipia usajili.

Sehemu ya saba inaelezea kuhusu makosa na adhabu zake. Katika sehemu hii imeelezewa adhabu kutokana na makosa mbali mbali.

Sehemu ya nane ni mengineyo. Sehemu hii inaruhusu utungaji wa sheria ndogo ndogo au kanuni pamoja na kanuni zake. Mhe. Spika, sehemu ya tisa ni ya majadweli.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, nawaomba Wajumbe wote waupitie mswada huu, wauchangie na baadae waupitishe ili Wizara iweze kuwa na chombo madhubuti chenye kusimamia maadili, maslahi ya utendaji kazi wa wauguzi na wakunga, kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa jumla.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri hoja imeungwa mkono, ikimaanisha kwamba sasa tujadili mswada huu. Nafasi ya kwanza basi nimpe Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii (Mhe. Mgeni Hassan Juma):**Mhe. Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima tukaweza kukutana tena katika Mkutano wa Kumi na Saba kwa malengo ya kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, napenda kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusiana na Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga Nam. 9 ya Mwaka 1986 na kuanzisha badala yake Sheria Mpya ya Baraza la Wauguzi na Wakunga na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, aidha napenda kumshukuru Waziri wa Afya, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupa wakati wa kupitia mswada huu. Hakika mashirikiano yao yalituwezesha kuifanya kazi hii kwa ufanisi mkubwa. Pia kupitia Afisi ya Baraza la Wawakilishi, na kwa mujibu wa Kanuni zetu ambapo kanuni ya 83 (5) na 83 (6) inaruhusu kuwepo kwa utaratibu wa kushirikisha wananchi kwa kuwapa fursa ya kutoa maoni yao juu ya miswada inayowasilishwa katika Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, kupitia utaratibu huo, Kamati yangu imeweza kushirikiana na wadau katika kuupitia na kuuchambua mswada huu muhimu ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa sheria itakayoanzishwa. Hivyo, natoa shukurani zangu za dhati kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na wadau mbali mbali wakiwemo Jumuiya ya Wauguzi Zanzibar *(ZANA)*, Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar *(ZAFELA)*, hospitali binafsi mbali mbali pamoja na Chama cha Wanasheria Zanzibar *(ZLS).*

Mhe. Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila iwapo nitashindwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano makubwa waliyonipatia katika kutekeleza jukumu hili muhimu ulilotuagiza, na naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama hivi ifuatavyo.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Hassan Hamad Omar | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ali Salum Haji | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mohammed Mbwana Hamad | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Farida Amour Mohammed | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Abdi Mosi Kombo | - | Mjumbe |

Aidha, Kamati ilishirikiana kwa karibu sana na Makatibu wetu ambao wamekuwa wakitusaidia katika kazi zetu kwa ufanisi mkubwa nao ni:-

1. Ndg. Asha Said Moh'd - Katibu
2. Ndg. Maryam Rashid Ali - Katibu.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo mfupi, sasa kwa ruhusa yako naomba niende katika mswada moja kwa moja. Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga (Uanzishwaji wa Baraza la Usajili wa Wauguzi na Wakunga) Nam. 9 ya Mwaka 1986 na kuanzisha badala yake Sheria ya Wauguzi na Wakunga na mambo yanayohusiana na hayo, umekuja kwa lengo la kufuta sheria inayotumika hivi sasa, ambayo kwa kiasi kikubwa imeonekana kupitwa na wakati na badala yake kupendekezwa kuanzishwa kwa sheria mpya ya Baraza la Wauguzi na Wakunga ambayo itaweza kusimamia vyema misingi na taaluma ya Uuguzi na Ukunga ili kuweza kuendana sambamba na mabadiliko ya nchi kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mhe. Spika, ni dhahiri kuwa nchi yetu imekuwa ikijitahidi kuchukua hatua mbali mbali katika kuboresha afya ya mama na mtoto. Katika kuhakikisha kuwa akina mama wanapata huduma bora za uzazi ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga, sheria mbali mbali zimekuwa zikitungwa ili kufikia azma hiyo. Miongoni mwa sheria hizo ni pamoja na *The Nursing Sister (Retiring Allowance Decree cap:46/1929)* na baadae *The Midwife Decree cap:71/1947* ambapo zote zilikuja kufutwa na Sheria ya Wauguzi na Wakunga *(Act No. 9/1986)* kwa lengo la kuanzisha Baraza la Wauguzi na Wakunga ambayo sheria hiyo inatumika hadi hivi sasa.

Mhe. Spika, tangu kutungwa kwa Sheria ya Wauguzi na Wakunga Nam. 6 ya mwaka 1986, nchi yetu imepitia mabadiliko makubwa ambayo imepelekea sheria hiyo kupitwa na wakati. Miongoni mwa mabadiliko hayo ni pamoja na mabadiliko ya Sera ya Afya ambayo mnamo mwaka 1999 Wizara ya Afya ilifanya mabadiliko ya sera hiyo na kufungua milango kwa sekta binafsi kutoa huduma za afya ili kuipunguzia mzigo Serikali na kuzifanya huduma za afya kuwa bora zaidi.

Mhe. Spika, mbali na mabadiliko hayo, mabadiliko ya kiuchumi na kuongezeka kwa mahitaji ya kijamii yanayotokana na ongezeko la watu na kutanuka kwa taaluma ya uuguzi na ukunga, imekuwa ni chachu ambayo imepelekea kuwepo haja ya kuifuta sheria hiyo ili iweze kuendana na mabadiliko hayo.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria unaopendekezwa kwa kiasi kikubwa utazingatia taaluma, fani na maadili ya wauguzi na wakunga ambapo kwa namna moja au nyengine utapelekea kuwepo kwa ufanisi zaidi, kwani Baraza la Wauguzi litakuwa na mamlaka ya kusimamia kikamilifu utendaji wa taasisi hizo ambapo sheria hii imetambua masuala ya ukaguzi wa hospitali, vyuo na taasisi zote zinazoajiri wauguzi na wakunga, kwa lengo la kudhibiti ongezeko la wauguzi na wakunga ambao hawana sifa na ambao hufanya kazi kinyume na maadili ya fani hii.

Mhe. Spika, Kamati yangu baada ya kuupitia na kuuchambua kwa kina mswada huu imependekeza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuuboresha zaidi mswada huu muhimu. Miongoni mwa marekebisho ni kurekebisha jina la mswada ambapo Kamati imependekeza lisomeke "Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga (Uanzishwaji wa Baraza la Usajili wa Wauguzi na Wakunga) Nam. 9 ya Mwaka 1986 na kuanzisha badala yake Sheria Mpya ya Baraza la Wauguzi na Wakunga na mambo yanayohusiana na hayo".

Aidha, katika kifungu cha 4(1) kinachohusu "Muundo wa Baraza" katika aya ya (b) imependekezwa kusomeka: "Muuguzi Mkuu kiongozi kutoka Wizara ya Afya". Hii ni kuhakikisha kuwa tafsiri ya mswada wa Kiswahili na Kiingereza zinalingana na kuleta maana inayokusudiwa ambapo mswada wa Kiingereza unasomeka:

(b) "*The Chief Nursing Officer in the Ministry;*

Vile vile aya ya (d) ya kijifungu hicho hicho imependekezwa isomeke:

"Mkuu wa Kitengo cha Uuguzi Zanzibar"

Sababu ya mapendekezo hayo ni kuweza kumshirikisha Mkuu wa Kitengo cha Uuguzi kuwa Mjumbe wa Baraza badala ya kuwa Mkuu wa Chuo cha Uuguzi kama inavyosomeka katika mswada huo.

Aidha, aya ya (g) imependekezwa isomeke:

"Muuguzi Mkuu kutoka Hospitali ya Serikali ya Rufaa"

Sababu ya mapendekezo hayo ni kwamba Mjumbe aliyekusudiwa hapa ni Muuguzi Mkuu na siyo muhudumu kama inavyosomeka katika mswada.

Mhe. Spika, Kamati pia imefanya marekebisho ya kuongeza kifungu, ambapo kifungu kilichoongezwa ni kifungu cha 2 ambacho kitasomeka kama ifuatavyo. Maelezo ya pembeni yatasomeka “matumizi”.

“ Sheria hii itatumika kwa Zanzibar tu”.

Sababu ya mapendekezo hayo ni kuiwezesha sheria hii kutumika Zanzibar tu na siyo kwengineko.

Aidha, katika kifungu cha 4(5) kimependekezwa kisomeke:

“ Mtu hatokuwa na sifa za kuwa Mjumbe ikiwa;

Ametiwa hatiani kwa makosa ya jinai ambayo adhabu yake ni kifungo kisichopungua miezi sita.

Sababu ya mapendekezo hayo ni kuweka bayana aina ya makosa ya jinai ambayo mtu akitiwa hatiani atakuwa hana sifa za kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza, na sio makosa yoyote tu ya jinai hata yakiwa ni madogo sana kama vile makosa yanayohusiana na Sheria za Barabarani.

Katika kifungu cha 5 kinachohusu “Kazi za Baraza” aya ya (b) imependekezwa isomeke;

“kumsajili muombaji kwa kufanya mtihani, kwa kumthibitisha au kwa kuweka viwango vyengine vya usajili; ”

Sababu ya mapendekezo hayo ni kuendana na tafsiri ya mswada wa Kiingereza katika kuleta maana halisi iliyokusudiwa.

Katika kifungu cha 9 kinachohusu “Uteuzi wa Msajili” Kamati imependekeza nafasi ya Msajili ambaye atakuwa ndiye Katibu Mtendaji wa Baraza, nafasi hiyo itangazwe na watu waombe badala ya kuteuliwa na Waziri, na Kamati ilipendekeza kuwa Waziri atafanya uteuzi huo miongoni mwa majina matatu yatakayopelekwa kwake kutoka kwa majina ya watu wenye sifa walioomba. Hivyo, kifungu hicho kimependekezwa kisomeke kama ifuatavyo:

9 (1) “ Waziri kwa kushauriana na Baraza atamteua Msajili wa Baraza ambaye atakuwa Katibu na Mtendaji Mkuu wa Baraza miongoni mwa majina matatu ya nafasi zilizoombwa”.

Mhe. Spika, sanjari na mapendekezo hayo Kamati pia katika kifungu hicho cha (2) ambacho kinaelezea sifa za mtu kuteuliwa kuwa Msajili, Kamati imependekeza kuwa ili mtu ateuliwe kuwa Msajili ni lazima awe na shahada ya juu badala ya stashahada kama inavyosomeka katika mswada, hivyo kijifungu hicho kisomeke kama ifuatavyo:

(b) "mwenye shahada ya juu ya uuguzi au ukunga au fani yenye kuhusiana na uuguzi au ukunga. "

Sababu ya mapendekezo hayo ni kuhakikisha kuwa Msajili ambaye atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Baraza ana sifa zitakazomuwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mhe. Spika, mbali na marekebisho hayo, Kamati yangu pia imefanya marekebisho ya lugha na uchapaji kama inavyoonekana katika marekebisho niliyowasilisha kwako na nakala kusambazwa kwa Wajumbe wako. Hivyo, natumia fursa hii kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wayapitie kwa lengo la kuchangia mswada huu.

Baada ya kuyasema hayo, naomba Wajumbe wachangie, waboreshe na hatimaye waupitishe mswada huu, kwani mswada huu ni muhimu katika kuboresha maendeleo ya afya ya mama na mtoto katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nawashukuru kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana, maoni ya Kamati yamewasilishwa, tuendelee na mjadala.

**Mhe. Salma Mohammed Ali:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuchangia Mswada wa Sheria wa kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga Nam. 9. Mhe. Spika, katika kifungu cha 3 (1) kunaanzishwa Baraza la Wauguzi na Wakunga likiwa ni Wakala wa Serikali. Na pia katika sheria inayofutwa ya mwaka 1986 Baraza hili la Wauguzi na Wakunga lilianzishwa lakini halikuwa Wakala wa Serikali. Hapa panaonekana ndipo penye mabadiliko ya kwanza na ya msingi. *(Makofi)*

Sasa namuomba Mhe. Waziri anifahamishe nini faida ya Baraza hili kuwa Wakala wa Serikali. Je, wakunga na wauguzi watapata faida gani. Na nini walikuwa wakikikosa kabla ya Baraza hili kuwa Wakala wa Serikali, na sasa watafaidika nacho baada ya Baraza lako kuwa Wakala wa Serikali. *(Makofi)*

Vile vile, Mhe. Spika, katika kifungu cha 4 (1) (a) Mwenyekiti awe na cheo cha uandamizi. Mhe. Spika, nini maana yake. Tusiige tu maneno ya watu tukaharibu Kiswahili chetu. Nashauri sana Mhe. Spika, neno uzoefu litumike badala ya uandamizi. *(Makofi)*

Lakini je, Mhe. Spika, miaka 15 sio mingi? Namuomba Mhe. Waziri aniambie wapo wangapi wenye angalau digrii ya uuguzi na ukunga na uzoefu wa miaka 15. Isije ikawa Mhe. Spika, kuna mmoja tu anatafutiwa nafasi. *(Makofi)*

Vile vile, Mhe. Spika, katika orodha ya Wajumbe wa Baraza la Wauguzi na Wakunga nashauri paongezwe Wajumbe wawili, Mkunga wa Jadi kutoka Pemba na Mkunga wa Jadi kutoka Unguja. Mhe. Spika, nashauri hivi kwa sababu hawa wakunga wa jadi wana mchango mkubwa katika shughuli hizi, hasa vijijini.

Mhe. Spika, tukiendelea katika kifungu cha 4 (5) hakifahamiki kimekusudia nini. Namuomba Mhe. Waziri anifahamishe kwani Baraza linateua muuguzi au mkunga. Naomba anifahamishe na akiwa ametiwa hatiani kwa makosa ya jinai, hawezi tena kuwa mkunga au muuguzi. Naomba kidogo Mhe. Waziri anisaidie hapa. Pia naomba nifahamishwe na Mhe. Waziri katika kifungu cha 6 (6), naomba ninukuu, "Muundo na utaratibu *terms*, na makatazo ya kamati yatawekwa na Baraza", mwisho wa kunukuu.

Mhe. Spika, nini maana ya neno hili *terms,* na je, Wizara haikupata neno la Kiswahili la kuliweka hapa. Namuomba Mhe. Waziri anifahamishe kwa sababu hichi kifungu mimi bado sijakifahamu.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 13 (1) neno "mwandamizi" limejirudia. Nashauri sana Kiswahili cha kwetu kitumike, iwe ni "Wauguzi na wakunga wenye uzoefu". Mhe. Spika, pia kifungu hichi cha masharti ya usajili ya kusajiliwa kwa wakunga na wauguzi ni kizuri, lakini je, wale wakunga wa kijadi vijijini ambao mchango wao mkubwa na hawana diploma wala digrii watatambuliwaje. Namuomba Mhe. Waziri pia anifahamishe hapo.

Mhe. Spika, lakini vile vile kifungu cha 18 kinazungumzia mkunga kuomba leseni na kulipia ada. Mhe. Spika, leseni na ada zinatolewa pale ambapo pana shughuli za biashara na faida. Sasa ukunga ni kazi ya huduma, ikiwa ni hivyo, hayo malipo ya ada mkunga atoe wapi. Mhe. Spika, mimi kifungu hiki siungi mkono mpaka nipate maelezo mazuri.

Mhe. Spika, lakini mwisho kwa kumalizia, kifungu cha 21 cha kuwatambua wakunga na wauguzi hawafanyi kazi kwa kumkashifu mtu anayemuhudumia kwa mdomo. Sijui hapa Mhe. Waziri kajiandaa vipi. Maana hawa wauguzi na wakunga, wanavyolalamikiwa na wanawake wanaokwenda kujifungua Mhe. Spika, kwa kweli matusi yao hayasemeki, usije ukaugua utapata lako. Je, Mhe. Waziri atawaadhibu wangapi.

Mhe. Spika, vile vile katika kifungu hichi namuomba Mhe. Waziri anifahamishe, hapa waliposema kwa hisia. Mhe. Spika, mimi napata hofu kidogo hapa huji kuambiwa mkunga au muuguzi hafai kazi kwa sababu ya hisia. Mhe. Spika, sijui hisia Mhe. Waziri wameitafsiri vipi, kwa sababu hisia zimo katika moyo wa mtu na hisia nyengine zinaweza zikaonekana, lakini nyengine ni hisia zipo ndani humjui mtu hisia yake ilivyo. Hofu yangu ni kuwa mtu asije kupeleka malalamiko kama hisia za yule, mimi naziona ni hivi ikaja ikawa nini. Kwa hivyo hapa namuomba Mhe. Waziri hili neno hisia hapa wamelitafsiri vipi.

Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana, naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa.

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa:** Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nikiwa mzima wa afya.

Mhe. Spika, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kuchaguliwa kuwa Mawaziri katika wizara hii. Pia niwapongeze na watendaji wao kwa kutuletea sheria hii ya wauguzi na wakunga.

Mhe. Spika, Mswada wa sheria unaopendekezwa kwa kiasi kikubwa utazingatia taaluma, fani, maadili ya wauguzi na wakaguzi ambapo kwa namna moja au nyengine utapelekea kuwepo kwa fani zaidi, kwani Baraza la Wauguzi litakuwa na mamlaka ya kusimamia kikamilifu utendaji wa taasisi hizo ambazo sheria hii imetambua masuala ya ukaguzi wa hospitali, vyuo, na taasisi zote zinazoajiri wauguzi na wakunga kwa lengo la kudhibiti ongezeko la wauguzi na wakunga ambao hawana sifa kufanya kazi.

Mhe. Spika, sheria hii ya wauguzi na wakunga ikipitishwa watafanya kazi zao vizuri. Mimi nikiwa ni Mjumbe wa kamati hii, Mswada huu tumeupitia vizuri kama Mhe. Mwenyekiti alivyowasilisha katika hotuba yetu hii. Naomba Wajumbe wachangie na pia nawaomba waipitishe sheria hii, kwa sababu sheria hii ikipita wakunga na wauguzi watapata kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Spika, mimi nikiwa Mjumbe, maoni yangu yalikuwa hayo. Mwisho kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi, naunga mkono mswada huu asilimia mia juu ya mia. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwanaidi. Tunaendelea na mjadala. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi asubuhi ya leo hii. Kwanza kabla sijaanza kuchangia Mswada huu mimi nakubaliana asilimia mia kwa mia.

Mhe. Spika, nilikuwa na kitendawili katika nafsi yangu, kwa sababu mara nyingi sana huwa karibu sana na hospitali, nilisema lini kutaweza kuletwa sheria ambayo itaweza kueleza sifa za muuguzi, mkunga na halikadhalika. Lakini leo ni siku ambayo imefika *alhamdulillah rabil-alamin*, tunaanza kuichangia ili kuweza kutoa michango yetu.

Mhe. Spika, nitajaribu kwenda kidogo kidogo kwa sababu siyo yule Mshimba wa mwaka jana, na nimeona niweze kutoa sifa hizi. Mimi nina historia nzuri na hospitali, na niseme ukweli hivi karibuni mimi mwenyewe nilikwenda operesheni na nimeona kuwa kweli tukidhamiria tunaweza tukafanya jambo lenye kuleta tija kwa wananchi, hakutokuwa na maana ya kuwa sasa kwa kuwa hospitali yetu imekuwa nzuri. Binadamu hawezi kukosa na kasoro, hata mimi ni mzuri lakini sasa hivi sauti sina. Sasa na hospitali yetu halikadhalika ni nzuri inaendana na wakati na neno la rufaa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, imenipasa mimi nichangie jinsi ambavyo nimeona huduma kati ya hawa wakunga, kati ya hawa wauguzi, nimeona jinsi gani wanavyopata tabu katika kufanya kazi zao na jinsi gani hasa wanavyokuwa wanataka kupata taaluma endelevu ili kuweza kufikia *standards* ambazo zinahitajika katika hospitali nyengine ambazo zinakwenda sambamba na hospitali za rufaa.

Mhe. Spika, nimefurahi sana tukienda katika ukurasa huu wa 31 tumeoneshwa hapa jinsi gani mkunga maana yake ni mtu ambaye aliyefaulu na kutimiza mafunzo ya ukunga katika Zanzibar au katika nchi yoyote inayotambulika na Baraza la Usajili na kupewa leseni ya kutoa huduma za ukunga.

Mhe. Spika, hilo ni la msingi, kwa sababu siku hizi tunakwenda na sayansi na teknolojia, haiwezi kuwa wewe mtu unajiita una fani fulani wakati hata shahada au hujapata mafunzo ambayo yaliyokuwa yanathaminika na kupata cheti, lakini Mswada huu umetueleza kabisa jinsi gani sasa hivi tunavyotaka

kuelekea na kuweka sheria ambazo zenye kuleta mantiki nzuri. Mhe. Spika, kuna Mabaraza na tulikuwa hatuna kitu hicho, kazi za Baraza zimeainishwa jinsi gani kazi hizo zitaweza kuoneshwa Baraza kazi yake ni nini.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana nalo, na kitu chochote huwezi ukakiita kitu tu kama Baraza au kamati au Tume, ikawa hujaeleza nini kazi zake zinawajibika kwa hao ambao waliotungiwa humu. Mhe. Spika, ukurasa huu wa 33, niingie katika kazi za Baraza, zitakuwa na kuhakikisha huduma za wauguzi na ukunga zitatolewa katika hali bora.

Mhe. Spika, mara nyingi sana tunatunga sheria, lakini sheria hizi zinakuwa zina upungufu wa kutokufanyiwa kazi kwa mujibu wa utaratibu, kitu ambacho kinasikitisha sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, wauguzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja wanajitahidi ipasavyo lakini kuna mambo ambayo kwa mujibu wa sheria hii kama ni kweli yatakuwa ni hivyo, basi nawaambia wauguzi sasa hivi munakula keki ndani ya sahani. Mhe. Spika, kwa sababu hawa watu wanafanya kabla ya yule *specialist* kufika, na sasa hivi muuguzi kuna *limit* ile kuweza kuwauguza watu, sasa yeye anakuwa *over* kupindukia mpaka. Mhe. Spika, sasa kwa kweli hili suala ni la ushujaa kabisa, kwa sababu kuna *international level* ya kuweza kuuguza watu ili ile akili iweze kutulia isipate *frustration* ya aina yoyote, lakini sisi wauguzi wetu wanakuwa *over loaded* kwa kuweza kuwauguza watu kupindukia mpaka.

Mhe. Spika, mimi niishukuru sana kuwa waangalifu ambalo sasa hivi linatoka katika sheria hii ambayo tutaiunga mkono, mimi nimesema *the first time* nimeunga mkono kutokana na hali halisi ilivyo. Lakini naomba kabla sijaendelea na kuuchangia Mswada huu, nitoe pongezi za dhati kabisa kuhusiana na suala hili la hospitali.

Mhe. Spika, nilikuwa na tatizo la *goitre* kwa muda wa miaka 15, lakini nilikuwa na woga woga wa kuingia katika hospitali kwenda kulipeleka kwenda kufanyiwa tiba, ukiniambia wewe mimi nitakupeleka haraka sana lakini mimi nilikuwa ni mwoga, na kwa sababu gani. Nilifika pahali nikajiuliza hivi kweli madaktari wetu wanaweza kuniuguza? kunifanyia tiba?

Mhe. Spika, lakini nimshukuru sana Katibu wangu Dkt. Jidawi ni shujaa, ameni-*convince* kwa asilimia kubwa na kuniomba Mheshimiwa kubali kuondoa hili tatizo. Mhe. Spika, nashukuru sana na nimefanya vipimo kwa mujibu wa sheria na nikaonekana nina-*fit* kwa kuweza kufanya dawa ile. Mhe. Spika, kulipita maneno ya hapa na pale, ooh! tumpeleke hospitali India Mshimba, tumpeleke wapi. Mhe. Spika, mimi sikutaka India, kwa sababu

nimewaamini wauguzi ambao tayari wana taaluma kwa mujibu wa sheria na niliamini kuwa vifaa Zanzibar katika Hospitali ya Rufaa, vifaa vipo kwa nini niende India. Nikasema kama kuna fungu la kunipeleka mimi India basi tafadhali wagaieni waliokuwa hawana uwezo ndugu zao wa kuwapeleka India. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimefanyiwa dawa *alhamdulillah Rabil-alamin*, na mpaka sasa hivi vipimo vya jana na juzi bado matatizo ya pale pale kwa sababu sauti yenyewe kama munavyoijua hii, haijawa katika *condition* nzuri kwa sababu miezi sita haijafika.

Mhe. Spika, ninachoomba sana, sheria tunazoziunda ziwajibike kuwafanyia wale tuliowatungia sheria. Mhe. Spika, ni aibu leo hapa Wawakilishi wako waliosoma na kubobea wanakaa wakakamua sauti zao kupitisha sheria, halafu baadae inaishia kwenye *briefcase* au kunako *table*, ni kitu ambacho hakileti ufanisi mzuri. Tunakuwa tunajiona wengine ovyo kweli, aah! nakuwa nakauka pale sauti yangu halafu leo sheria tunaipeleka haifuati mkondo wake.

Kwa hivyo, naomba sana Wizara husika na sasa hivi ina *new faces*, ina Waziri madhubuti, ina Naibu Waziri madhubuti, ina Katibu Mkuu madhubuti, ina Wakurugenzi madhubuti, naamini kutokana na sheria hii Waziri hatokuwa katika kusinzia atafanya kazi vizuri sana. Naibu Waziri wake ni mtu shupavu sana, ana *good experience*, kwa sababu kuna mambo tayari sasa hivi wameshaanza kuyafanya yawe *changing* katika Wizara ile.

Kwa hivyo, naomba sana na Waziri atafuata nyayo, Naibu Waziri atafuata nyayo za Naibu Waziri aliyeondoka kwa sababu na yeye alikuwa *24 hours* unamkuta hospitali. Yeye alikuwa hajui, yeye akipanda juu, mimi naanza kuwepo chini, alikuwa hajui yeye hivyo lakini tunapishana kwenye ngazi. Mimi mara nyengine huuliza Mheshimiwa kaleta wagonjwa, kumbe anatembea jinsi gani kuona wale wafanyakazi zile kazi zinavyofanywa kila leo na jana. Mhe. Spika, mimi nishukuru sana kuwa sheria hii itatufikisha pahala pazuri.

Mhe. Spika, naingia ukurasa wa 35. Mhe. Spika, katika kifungu cha 8, wanasema sheria hii ya Baraza kwa kushauriana na Waziri, uteuzi na uwezo wa ukaguzi. Mhe. Spika, hapa kidogo ningeomba hapa wakati wowote muafaka au kuingia katika maeneo ya mafunzo ya ukaguzi, haya mambo ya kuteuliwa mara nyingi sana tunachukua muda mrefu.

Mhe. Spika, naomba sana kipengele hichi kitafutwe neno la kushindikiza, maana yake kuonesha ile umuhimu. Kwa sababu tunakuwa tunapewa sheria ya kuteua lakini tuna-*delay* kwa sababu panatokea athari katika sehemu ile.

Mhe. Spika, sasa mimi naomba sana kwa kuwa huyu mtu ameshafika uwezo, anao uwezo wa utendaji wa kazi, ana uwezo wa kusoma basi kipengele hichi ningemuomba sana Mhe. Naibu Waziri au Mhe. Waziri tutafute njia ya kuweza kutoa shindikizo. Kwa sababu ni kweli mkaguzi aliyeteuliwa chini ya kifungu hicho kidogo na kifungu chengine ana uwezo, lakini sasa tuangalie hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, halafu haya mambo ya kupenyazana sasa hivi kwa mtu ambaye mtoto wa mjomba, mtoto wa shangazi na hii ndiyo hitilafu, kwa sababu kule wauguzi kuna matatizo yake, unatakiwa kusoma na kustahamili, wengine wanakuwa jeuri tu. Sasa nalo hili tulioneni jamani *system* ya jeuri jamani tulisimamie kwa mujibu wa sheria, na kama mtu akigundulikana sheria hiyo itafutwe aweze kuwajibika, kwa sababu wengine wanawatukana wazee katika kuuguza kwao. Lakini vile vile na wao sio kwa kuwa wanasoma na wana vyeti tu, hata mafao na wao waongezewe na *security* na nini ipatikane. Mhe. Spika, kwa mfano kuna sehemu ya mashine ya *CT-Scan*. Mhe. Spika, mashine ile kwa jicho langu mwenyewe nimeona, wale wafanyakazi wa mule ndani hawana *security*, aina ya vazi la aina yoyote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nalo hilo naomba sana kuwa wauguzi wale wanauguza lakini wapo hatarini, kwa sababu hujui *effects* zake zikoje kile kitu, na wakati wewe mgonjwa unatakiwa ufanyiwe mara moja tu mashine ile. Sasa seuze huyu *24 hours* yupo katika utibuji. Mhe. Spika, kwa hivyo, naomba sana na hawa watu *security* ziangaliwe nazo ziwemo katika sheria ili kuweza kuwalinda, wana-*risk*. Kwa hivyo, Mheshimiwa naomba sana hili suala kuwa tuliangalie katika mifumo ambayo itaendana na vyeti, iendane na uadilifu na iendane na *security* ya kuwalinda hawa watu.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nimeingia kwenye ukurasa huu wa mwisho wa 37, ambapo hapa ndipo katika majukumu ya misingi ya usimamizi. Mheshimiwa hapa katika kifungu namba 2 kitakuwa na jukumu la kila msimamizi kwa muuguzi au mkunga aliyesajiliwa na aliye chini ya wasimamizi wake kufanya yafuatayo:

Kusimamia kwa mujibu wa miongozo. Waheshimiwa sheria ndiyo kama nilivyosema, Muuguzi lazima awe *serious* katika kazi yake, katika kusimamia ndiyo kufanikisha, lakini Mheshimiwa sitaki nirudie lugha hii hii, unamchagua mtu lakini hana ile hamu ya kazi yenyewe, lakini kwa kuwa kasoma tu basi, lakini tunampeleka tu. Mheshimiwa hili suala linaumiza sana, kwa sababu kule hospitali sio mwahala mwa kuchezea, *one mistake* unaua, *mistake* ndoto tu unaua, lakini sioni sheria hii katika uuguzi aliyekuwa mzembe akasababisha maafa, katika kuangalia angalia kwangu kwa ghafla sijaona humu kuna vitu kama hivyo ambavyo sheria imewekwa. Kama

hamuna naomba sheria ichukue mkondo wake. Mwanasheria mpya tunaye, nakushukuru sana, Mwanasheria njoo tunakupokea nipo mimi *adviser* wako nipo hapa usijali.

Sasa Mhe. Spika, nimeona hii kwa ghafla hapa sijaangalia vizuri kwa kuvaa miwani, hivi navyo tuweke sheria, kwa sababu muuguzi ukiwa mzembe kusimamia au kufuatilia, ikitokea tatizo la mtu kufa, yeye atawajibika nini. Naomba sana ushauri wangu wa bure huo, kuwa hili suala liangaliwe na kuwekewa sheria ya hali halisi ilivyo, lakini muuguzi akiwa mzuri, hakuna tatizo Mheshimiwa na havitatokea vifo vya hapa na pale hata siku moja.

Kwa hivyo, nikiendelea nije katika kifungu cha 14 katika Daftari la Usajili wa Wauguzi na Wakunga. Mhe. Spika, huo ndiyo wajibu wetu, kwa sababu jambo lolote liwe na kumbukumbu, nakubaliana nalo. Leo sehemu ya kuweka kumbukumbu kule hospitali sijui kama mpaka leo kumetengenezwa vizuri.

Mhe. Spika, kumbukumbu za Serikali zinapotea hasa katika Wizara ya Afya, kwa sababu hatukuwa na *special room*, iko *room* lakini imeshajaa mafaili, yanasambazwa ovyo ovyo. Sasa mimi nina wasi wasi na daftari hili sijui litawekwa wapi, hata ikiwa mwenye udhamini wa kusajili yupo lakini sasa na yeye sijui kama atapata *special room* ya kuweza kulipeleka.

Mhe. Spika, hili suala bado hospitali naomba sana, tunapitisha sheria hii, kama nilivyoeleza hapa, daftari litakuwa na usajili kujumuisha majina, anuani, sifa na taarifa nyengine zitakazohitajika kwa muuguzi na mkunga mwenye sifa hizo, lakini utamuwekea wapi na sisi leo hatuna chumba cha kuhifadhia madubwana haya. Sasa nalo hili ni hitilafu.

Mhe. Waziri mpya na Naibu Waziri mpya liangalieni, kwa sababu kitu historia ni kitu muhimu sana, unapotaka kutafuta jambo likusaidie katika kumbukumbu ya kesi unataka kuhukumu, kama huna sehemu ambayo umewekwa historia ile, basi Mheshimiwa Spika, inakuwa ni tatizo au utahukumu vibaya, utawapelekea taaluma ile au sheria iliyopitishwa na wajuzi hapa iwe ime-*fail*. Mhe. Spika, mimi sitokubaliana nalo suala hilo.

Mhe. Spika, nilisema mara nyingi sana kuhusu suala la kuhifadhia madaftari kule, ma-*file*. hii ni mara nyengine itakuwa ni mara ya tatu. Tunatunga tena sheria itakuwa na madaftari ya usajili ya kujua wauguzi; sifa zao, majina na sehemu gani. Kwa hivyo, hichi kitu kinakuwa hakuna. Mimi Mhe. Spika, nakuwa kidogo mkaidi kutokana na hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, nikiendelea katika ukurasa huu wa 38, masharti ya usajili wa chini ya kifungu (1) na kifungu hiki ni kama ifuatavyo.

Kuwasilisha ushahidi utakaoathiri Baraza, awe amehitimu na kufaulu mafunzo. *Yes* Mheshimiwa hili suala nikubaliane nalo, kifungu hiki ni kweli. Siku hizi nataka kutoa tahadhari, kuna vyeti feki sasa hivi, lakini vile vyeti feki ni sawa na vile ambavyo ni *international*. Sasa lazima hili Baraza liwe na wataalamu wenye uzoefu wa kuvijua hivi vyeti ambavyo sio halali na vile vilivyokuwa ni halali. Lakini je, sheria, au hawa Baraza kama akipenya mtu ambaye amepata vyeti hukumu iko wapi. Mheshimiwa mimi sijaiona hukumu humu.

Kwa hivyo, mimi napendekeza sana Mheshimiwa tuwe na tabia ya kutoa agizo la utendaji, halafu baadaye na utendaji ukiwa una kasoro, tuwe na vifungu ambavyo vitaweza kufanywa sheria kwa wale watu waliozembea. Kwa hivyo, Mheshimiwa hii mimi sina tatizo nalo nakubaliana nalo bila ya tatizo lolote.

Mhe. Spika, nikiingia chini yake hapa, kuwasilisha ushahidi kama walivyoeleza hapo ni ukurasa huo huo wa 38, kifungu cha 4. Pindipo ikitokea kutokuwepo na lolote kati yaliyoelezwa katika kijifungu kidogo (a) na (b) cha kifungu cha 3 na kifungu cha Baraza kinafanyika mtihani na muombaji naye atapaswa kufaulu mitihani hiyo, ikiwa muombaji... Hapa kidogo sijui mantiki yake wamekusudia vipi. Nakirudia tena Mheshimiwa kifungu hiki. Pindipo ikitokea kutokuwepo kwa lolote, kati yaliyoelezwa katika kijifungu kidogo (a) na (b) kijifungu kidogo cha (3) na kifungu hiki Baraza litamfanyia mtihani muombaji na yeye atapaswa kufaulu mitihani hiyo.

Sasa hapa ina maana Baraza linafungua darasa jipya, wakati ameshaonesha vyeti vyake. Mimi nafikiria hapa tungesema kuwa Baraza lingeweza kumfanyia *interview*, ambapo *interview* hiyo impime katika vile vyeti alivyonavyo. Lakini tunaanzisha tena kumfanyia mtihani mwengine. Mheshimiwa namalizia. Kumfanyia mtihani mwengine ni kum- *frustrate* yule kijana ambaye ameomba kumrudisha tena katika hali aliyokuwa.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana nalo na kwa kumalizia kwamba naiunga mkono na niwape sana hongera wataalamu wetu wa Cuba, Wazanzibari pamoja na wauguzi wote. Mwenyezi Mungu awabariki awape kila la kheri, na sisi tuache kwenda kutibiwa nje Waheshimiwa tuwajali ma-*expert* wetu hapa na tutibiwe hapa. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**Mhe.Spika:** Mheshimiwa Makame Mshimba Mbarouk tunakushukuru. Naomba sasa nimkaribishe Mheshimiwa Abdalla Juma Abdalla.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutia baraka zangu kidogo katika mswada

huu muhimu sana, ambao malengo yake ni kuendeleza afya za akina mama na kuepuka vifo vya kina mama na watoto.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tusikilize mjadala unaendelea. Minong'ono imekuwa mingi sana, Mheshimiwa Makame Mshimba Mbarouk na Mheshimiwa Abdalla pale.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Nianze na Sehemu ya Pili, Kifungu cha 4. Ukisoma kifungu cha 4(1) Baraza linaundwa na Wajumbe wafuatao. Sasa (a) kwanza ni Mwenyekiti, Mwenyekiti ambaye atakuwa na cheo cha uandamizi wa masuala ya uuguzi au ukunga na uzoefu wa miaka 15.

Sasa hapa mimi tatizo langu ni moja, haidhuru Kamati ya Ustawi wa Jamii ilifanya marekebisho katika kifungu hiki, lakini pamoja na marekebisho ya Kamati na mimi naomba kurekebisha jambo jengine, kwamba huyu Mwenyekiti, haikutajwa *authority* ambayo itamteua. Kwa sababu ukisoma kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, kinasema;

"Wajumbe wote watateuliwa na Waziri isipokuwa wale ambao watakuwa Wajumbe kwa nafasi zao".

Lakini kwa kawaida Mwenyekiti, mara nyingi ukitaja kutakuwa na Mwenyekiti, basi unataja na *authority* ambayo itamteua yule Mwenyekiti. Sasa naomba hapa katika kifungu hiki kidogo cha (1) (a) itajwe kabisa hapa basi, kama ni Waziri basi tumuone hapa kwanza, au kama kuna *authority* nyengine itakayomteua Mwenyekiti, lakini ielezwe katika kifungu hiki kidogo cha (1) (a), hilo moja.

Mhe. Spika, ukisoma kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki cha 4, inasema;

"Ni marufuku kwa Baraza kumteua muuguzi au mkunga ikiwa, kuna masharti matatu pale, (a) (b) na (c). Sasa mimi nina-*doubt* na sharti hili la namba (a) kwamba ametiwa hatiani kwa makosa ya jinai.

Mhe. Spika, hii imekuwa ni *principle* sasa, kila sheria ikitungwa inamuengua mtu anayetiwa hatiani kwa kosa la jinai. Makosa ya jinai Mhe. Spika, yako mengi na yana mazingira tofauti. Sasa ukisema mtu anapoteza pengine heshima yake katika jamii kwa sababu ametiwa hatiani kwa kosa la jinai bila kuainisha ni kosa lipi na kwa mazingira gani, itakuwa hatuwatendei haki watu wengine.

Maana kuna mtu anapata *accident* tu barabarani, anashtakiwa kwa kosa la jinai pengine anatiwa hatiani, lakini *accident* ni kudra ya Mwenyezi Mungu

hakuitaka yeye mwenyewe. Sasa mimi nadhani wakati wa kusema hili tuzingatie kwamba hilo kosa la jinai aliloshtakiwa nalo au alilopatikana na hatia nalo basi amelifanya katika mazingira gani, sio pengine tunakuja kumnyima haki yake ya kibinadamu kwa sababu ya kutiwa hatiani kwa kosa ambalo yeye mwenyewe hakuwa na makusudio nalo kulifanya. Kwa hivyo, nilikuwa napendekeza kifungu hiki (a) ama kiongezewe maneno au kifutwe kabisa.

Jambo jengine Mhe. Spika, ni kazi za Baraza kifungu cha 5. Ukisoma kazi (b) ni kumsajili muuguzi aliyefaulu mitihani yake, lakini kumthibitisha. Kazi nyengine ni kuweka viwango vyengine vya usajili. Sasa mimi nilitaka Mhe. Waziri akija hapa anipe ufafanuzi kidogo, ili viwango vyengine vya usajili, hasa vinawalenga akina nani, kwa sababu hapa tayari sifa za muuguzi ambaye anapaswa kusajiliwa zimewekwa hapa. Ni sifa za kielimu, awe na cheti cha Stashahada sijui na nini, sasa ukiacha hao wenye sifa hizo, kuna viwango gani vyengine ambavyo Baraza hili linaweza kutoa usajili. Nafikiri kunahitaji maelezo zaidi. Kwa hivyo, naomba Waziri akija hapa atufafanulie kidogo.

Jambo jengine Mhe. Spika, ni kifungu cha 6 Kamati za Baraza. Ukisoma kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 6, kinasema; "bila kuathiri madhumuni ya kifungu kidogo ya kijifungu hiki".

Inaonekana hapa kuna maneno yamekosekana. Nilipokuwa naangalia waraka wa Kamati, kuna marekebisho wamefanya, lakini bahati mbaya mimi sikuridhika nayo moja kwa moja. Kwa hivyo, naomba na mimi kuongeza marekebisho hapo.

Kamati wanasema wao wanafuta maneno yale yaliopo kwenye kifungu kidogo (2) mstari wa kwanza ambayo yanasomeka; "ya kifungu hiki" wao wanayafuta, mapendekezo ya Kamati ni kwamba wanayafuta. Mimi nadhani yale maneno tusiyafute, kwa sababu tukiyafuta yale maneno yatakuwa yanaweka utata katika hii sentensi. Kwa hivyo, naomba irekebishwe hivi; "Bila ya kuathiri madhumuni ya kijifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Baraza linaweza kuanzisha Kamati zifuatazo". ninachokusudia kusema, yale maneno ambayo Kamati ya Ustawi wa Jamii walipendekeza yafutwe. Yasifutwe na badala yake yaongezwe tu, kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki. Nafikiri hiyo italeta maana nzuri zaidi.

Nikiacha hapo, kifungu hiki hiki cha 6(3), pia kuna neno limekosekana pale, kwa madhumuni ya kijifungu cha (2) cha kifungu hiki. Mimi nadhani iandikwe kwa madhumuni ya kijifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki. Yaani lile neno kidogo liwekwe pale, ndiyo itaweza kuleta maana nzuri zaidi, na hapo chini yake kifungu kidogo cha (4), naona hiki kina *repetition* nyingi.

Sasa naomba nikisome, halafu naomba kifutwe kwa sababu tayari kuna vifungu vimeshachukua hiyo dhamana. Vinasema, Baraza lina uwezo wa kuanzisha Kamati yoyote kwa ajili ya kufanya kazi za ujumla au mahususi na linaweza kukasimu kazi kwa Kamati yoyote kadiri itakavyoona inafaa. Sasa hiki kifungu kidogo cha (4) kina *repetition* ya vifungu viwili.

Cha kwanza kifungu cha 6(1), itabeba ile Baraza kuunda Kamati na kwa idadi ambayo itaona inafaa. Kwa hivyo, hapa hakuna haja ya kueleza tena hili. Halafu na kifungu cha 7, kifungu cha 7 nacho kinatoa uwezo wa Baraza kukasimu madaraka yake kwa Kamati. Kwa hivyo, mimi napendekeza kifungu hiki kidogo cha (4) kifutwe kabisa, kwa sababu madhumuni yake yameshakuwa *represented* katika vifungu hivyo nilivyovitaja.

Nikitoka hapo kwenye kifungu hicho cha 6, kifungu hicho hicho cha 6(6) kinaeleza muundo, utaratibu, halafu kuna neno la Kiingereza pale limetiwa "*terms*", na makatazo ya Kamati yatawekwa na Baraza. Sasa hapa kuna tatizo, kwanza hili neno "*terms*" naona kama halina maana hapa, na hata kama lina maana basi lingepaswa liandikwe kwa Kiswahili, lisiandikwe kwa Kiingereza, hakuna sababu ya kuliandika kwa Kiingereza.

Pia, hapa napo nilikuta marekebisho kwa Kamati. Kamati imekirekebisha hicho kifungu cha 6 kwa kusema muundo, utaratibu, makatazo na masharti mengineyo ya kamati yatawekwa na Baraza. Hili sina pingamizi nalo nakubaliana na Kamati, ila na mimi nilikuwa nimeweka *proposal* hapa, naomba nisome, Waziri akiona inafaa anaweza akaichukua. Mimi nilisema hivi muundo na utaratibu wa utendaji wa kazi za Kamati utawekwa na Baraza. Sasa akiona ya Kamati mazuri zaidi, yangu mimi anaweza akayaacha, na akiona yangu mazuri zaidi anaweza kuyaacha ya Kamati.

Nikiondoka hapo niende kwenye Kifungu cha 8(2), pale kuna mkaguzi, kinasema; mkaguzi aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, anaweza. Sasa mimi *objection* yangu hapa iko kwa huyu mkaguzi. Huyu mkaguzi hakuwekewa sifa. Niliposoma kwenye waraka wa Kamati, Kamati imeweka sifa hapa, inasema; awe muuguzi au mkunga ambaye amesajiliwa au Afisa Afya ya Jamii na awe na uzoefu usiopungua miaka 15. Wamejitahidi Kamati ya Ustawi wa Jamii.

Mimi nilidhani Mhe. Spika, unapomuweka mtu kumsimamia mwenziwe basi yule msimamizi awe na sifa bora zaidi kuliko yule anayesimamiwa. Sasa kama Muuguzi na Mkunga ana *diploma* basi anatakiwa Mkaguzi awe na zaidi ya *diploma*, pengine angalau na *degree*. Kwa hivyo, ninaomba hapa Mhe. Waziri azingatie hapa kwamba huyu mkaguzi ambaye atakagua wenziwe

elimu yake iainishwe kabisa hapa, kwa sababu anaokwenda kuwakagua imeelezwa kuwa watakuwa na kiwango cha stashahada.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, niende kwenye kifungu cha 10 cha mswada huu kifungu kidogo (f) kuhakikisha, yaani hizo ni kazi za msajili hizo (f) inasema "kuhakikisha uwekaji mzuri wa hesabu na mali, kuandaa makisio ya mwaka na ya ziada matumizi ya fedha". Kwa hivyo, hapa nina tatizo kidogo, tatizo langu ni kwamba hizi kazi ambazo amepewa msajili, hususan kazi za fedha, kwa kweli kazi hizi anatakiwa afanye *auditor*.

Kwa maana hiyo, hili Baraza la Wauguzi linatakiwa liwe na *auditor* wake na haya masuala ya kuchunga fedha, madaftari  pamoja na mambo mengine yote afanye mhasibu na wala sikusudii *auditor* nakusudia mhasibu na sio yafanywe na msajili kwa sababu msajili anazo kazi zake nyengine. Mhe. Spika, naomba kazi hizi iainishwe kwamba atafanya mhasibu badala ya msajili.

Nikiendelea na mchango wangu naomba sasa niende kwenye kifungu cha 12(2) kinasema "Maafisa na Wafanyakazi wa Baraza katika utendaji wao wa kazi watawajibika kwa Msajili". Nadhani kwa sababu Baraza hili lina Mwenyekiti, kwa nini wasiwajibike kwa Mwenyekiti wa Baraza moja kwa moja na wawajibike kwa msajili ambaye ni afisa tu katika Baraza. Kwa hiyo, naomba hawa maafisa wote na wafanyakazi wa Baraza wawajibike kwa Mwenyekiti moja kwa moja.

Halafu kifungu cha 13(2)(b). Sasa kifungu cha (2) kinasema itakuwa ni jukumu la kila msimamizi wa muuguzi au mkunga aliyesajiliwa aliyechini ya usimamizi wake kufanya yafuatayo. Huyo msimamizi ambaye anasimamia wakunga na wauguzi, basi moja katika majukumu yake ni "kufanya uchunguzi kuhusiana na shtaka na malalamiko yoyote dhidi ya muuguzi au mkunga aliyesajiliwa ikijumuisha utendaji mbaya, uzembe na tabia mbaya na kuwasilisha taarifa kwa Baraza;"

Mhe. Spika, hii nataka niipongeze sana kwa sababu sisi kama viongozi wa umma tumekuwa tukilalamikiwa sana na wananchi, kwamba akinamama wakienda hospitali basi miongoni mwa changamoto kubwa wanayokabiliana nayo pale ni tabia mbaya za wakunga wetu au sijui ni wauguzi kule hospitali sijui niwaite vipi, lakini wana tabia mbaya ya kuwasumbua kwa maneno ya kashfa au udhalilishaji kiasi ambacho wengi wao ...

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, naomba tupunguze minong'ono, ili mjadala huu wende kwa mtiririko mzuri. Mheshimiwa Abdalla Juma Abdalla endelea unazo dakika kama tano.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** *Inshaallah*. Kwa hivyo, wananchi wanakuwa wanapata usumbufu mkubwa sana kutokana na maneno ambayo kwa kweli siyo mazuri ambayo wanayapata akinamama wajawazito pale hospitali. Sasa namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa kushirikiana na wasimamizi wake basi wasimamie vyema, ili akinamama wasipate matatizo pale hospitali.

Vile vile napendekeza kwa kweli Mhe. Waziri katika hili awe mkali, maana yake tumeshasema sana Mhe. Spika maneno haya na bado ndugu zetu kule hospitalini wanatufanya sisi kama hatuna maana, yaani wanaendeleza usumbufu ule ule. Kwa hivyo, Mhe. Waziri awe mkali sana, ili tuone kwamba tatizo hili linarekebishika.

Mhe. Spika, tatizo hili ndilo lililopelekea mpaka hivi sasa kuna wakunga katika mitaa na hao wakunga watu wengi wanakwenda kujifungulia kule kwa sababu ya kukwepa ule usumbufu ambao wanaupata akinamama wajawazito pale hospitali. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri alisimamie vyema hili, ili tuone kwamba matatizo haya yanaondoka.

Jambo jengine ambalo nataka niishauri sana Serikali kuhusiana na sifa ambazo anatakiwa mkunga awe nazo ndiyo asajiliwe. Mhe. Spika, ukisoma kifungu kidogo cha 15(2)(a)(i) hii ndiyo inatoa sifa ya mtu ambaye anaweza kusajiliwa kuwa mkunga au muuguzi na inasema awe "amehitimu na kufaulu mafunzo ya uuguzi au ukunga kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu na kutunukiwa diploma, shahada au zaidi kutoka katika chuo kinachotambulika na Baraza;"

Mhe. Spika, sifa hii ukiiangalia kwa upande mmoja wa shilingi ni nzuri maana yake inapandisha *status* ya viwango vyetu vya kutoa huduma hizi za afya. Lakini ukiiangalia kwa upande wa pili italeta matatizo makubwa na italeta matatizo kwa sababu Mhe. Spika, katika jamii yetu tunao wakunga wengi sana ambao ni wazoefu sana wa siku nyingi na wanafanyakazi hizi za kuwasaidia akinamama wajawazito kwa ufanisi mkubwa.

Vile vile huku nyuma nilitangulia kusema kwamba akinamama wajawazito wengi wanapenda sasa kwenda kwa wakunga hao, kwa sababu hawapati usumbufu na wanapata huduma nzuri za kibinadamu ambazo ni za kihuruma sana. Lakini leo kifungu hicho wote kinawa-*disqualify* wale.

Nadhani Mhe. Waziri na ninaomba hapa anisikilize vizuri. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri anisikilize vizuri sana, kwamba hiki kifungu kisibakie hivi kilivyo tu, isipokuwa kuwe na marekebisho mengine ambayo yatafanya hao wakunga wa kienyeji wawewana- *survive*, yaani wanaendelea kutoa

huduma watambulike rasmi na ikiwezekana kama kuna *course* nyengine zaidi wapewe, kwa sababu Mhe. Spika, tulikuwa na daktari hapa Zanzibar na sijui kama mpaka leo anafanya hizo kazi au ni marehemu sina hakina.

Lakini huyu daktari alikuwa ni daktari wa macho na aliishi sana pale Abdalla Mzee Hospitali na elimu yake ilikuwa ni darasa la saba tu, lakini alikuwa akifanya kazi za kutibu watu macho na *operation* akiwashinda mpaka watu wenye *degree* au zaidi kwa uzoefu wake.

Sasa hawa wakunga wa kienyeji ambao wameshafanya kazi kwa muda mrefu sana japo kuwa hawana shahada wala stashahada, lakini kwa sababu wanafanya kazi kwa ufanisi ni watu ambao wanaoisaidia jamii sana na ni watu ambao wanaopunguza ule mzigo wa akinamama wajawazito kukimbilia pale Hospitali ya Mnazimmoja na Hospitali ya Mwembeladu kwenda kujifungulia.

Kutokana na hali hiyo, hawa tusiwa-*disqualify* moja kwa moja, isipokuwa tuwatafutie utaratibu tuwaongezee taaluma, tuwatambue, tuwasajili kwa kiwango chao hicho walichonacho, lakini waendelee kuisaidia jamii yetu. Lakini ukiwatoa moja kwa moja kwa kweli utaitia nchi katika matatizo makubwa.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri hili alione na ndani ya mswada huu basi kuwe na kifungu kinachowatambua hawa wakunga wa kienyeji japo huko mbele ya safari tunaweza kuwadondosha mmoja mmoja taratibu, lakini kwa ghafla namna hii tunaweza kusababisha matatizo makubwa kabisa.

Mhe. Spika, kwa kuwa ninaheshimu sana muda wako japokuwa nina mengi ya kuzungumza. Lakini naomba nimalizie hapa kwa kusisitiza kwamba Mhe. Waziri asimamie vyema baadhi ya wakunga wetu ambao wana tabia mbaya za kudhalilisha akinamama, si jambo jema hata kidogo na tumeshalisema sana na mara nyengine tutalazimika hivi sasa kwenda kuwavizia na tukiwagundua kwa kweli tutawashtaki na wasijewakatuona wakorofi baadaye, tena mimi na Mhe. Jaku Hashim Ayoub tutakuwa tukivizia pale Hospitali ya Mnazimmoja na tukipata watu wanapewa maneno ya kashfa namna hii tutakuwa hatuvumilii tena. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Ali Salum Haji na afuate baada ya hapo Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Spika, nikushukuru kwa dhati kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia mswada huu wa Baraza la Wauguzi.

Mhe. Spika, kwa bahati mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Naomba nichukue fursa hii adhimu kuipongeza wizara baada ya kuona baadhi ya mapungufu kwa Sheria Namba 9 ya mwaka 1986 na kuona kuna namna na haja ya kuweza kufanya mabadiliko na hadi kuleta mswada huu wa kuunda Baraza hili la Wauguzi.

Mhe. Spika, mswada huu ambao tunategemea baadaye kuwa sheria baada ya kuangalia kwa kina na kuupitia vifungu kwa vifungu tumeona namna ya haja ya Serikali katika kuweza kuwasaidia wauguzi pamoja na wakunga kwa namna ya kuwapa utaalamu, kuwajengea uwezo, ili kuweza kuwahudumia wananchi wetu.

Kwa kweli, mara nyingi tumekuwa tukipiga kelele, akinamama wakipiga kelele namna ambavyo wanapata huduma ambazo ni duni, yaani huduma ambazo hazistahiki, lakini Wizara ya Afya kwa kuona au kujali shida za wananchi wetu wakaona kwamba haja imefika ya kuweza kuunda chombo hiki ambacho kitaweza kuwatatulia matatizo wananchi wetu hususan akinamama na watoto.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie jambo dogo sana, ukiangalia mswada Mhe. Spika hauna tatizo na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwamba tuunge mkono kwa asilimia mia moja, ili uweze kuwa sheria na kuweza kuwatatulia wananchi wetu matatizo yanayowakabili.

Lakini katika kuunda vyombo kama hivi vya sheria kuna mambo mawili. Haja ya kwanza kuunda kile chombo chenyewe cha kisheria na kikaweza kusimamia yale matatizo au matakwa ya wananchi.

Pia kuna jambo jengine la msingi ambalo ni la upande wa pili, basi baada ya kuunda hiyo sheria ni kupata vyombo au zana za kisasa ambazo zitaweza kutoa huduma kwa hao wananchi wenyewe, kwa sababu tunaweza tukawa na sheria nzuri pamoja na wakunga wazuri, lakini kama hatukuwa na vyombo vya kisasa ambavyo vinakidhi mahitaji ya wananchi wetu basi bado itakuwa sheria ile au wanataaluma wale hawataweza kufanya kazi vizuri sana.

Sasa Mhe. Spika, niseme na niiombe Wizara ya Afya kupitia kwako, kwamba pamoja na kuipitishia mswada huu kuwa sheria basi niwaombe pia waandae mikakati ya kutosha kuona kwamba na hiyo kada yenyewe basi inatengenezewa zana ambazo zinaweza zikasaidia kutoa huo ufanisi wa watu wetu.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka kulizungumzia kwa bahati mswada huu una malengo ya Baraza hilo la Wakunga na Wauguzi. Moja ya malengo yao

ni kuwajengea ufanisi na utaalamu na kuwajenga kimaadili. Kwa hivyo, niseme moja ya jambo ambalo ni zuri wamelileta ni hili, kweli maadili ya wauguzi na wakunga sio kama yalikuwa ni mabaya lakini baadhi ya wauguzi na wakunga walikuwa hawatumii fursa zao vizuri katika utendaji wao wa kazi.

Sasa kuupitisha mswada huu na malengo haya yakakamilika na zile sifa au utaalamu ukajengwa vizuri, basi imani yetu kwamba mama zetu wataondokana na yale mashaka ambayo kwa muda mrefu walikuwa wakiyapigia kelele katika suala zima la kupata huduma za wauguzi.

Jengine ambalo nataka nilipongeze namna ya kuweza kudhibiti ongezeko la wauguzi na wakunga, ambao kipindi cha nyuma walikuwa hawana sifa ambao hufanya kazi zao kinyume na maadili ya fani hii. Kweli jambo hili linaweza kusaidia wananchi wetu, kwani wananchi wengi walikuwa wakipiga kelele na vifo vingi vilikuwa vikitokezea kutokana na wauguzi na wakunga ambao fani zao za kitaalamu zilikuwa duni, ambazo zilikuwa zinapelekea mara kwa mara watoto wachanga kufariki wakati wa kujifungua akinamama.

Kwa hivyo, nishukuru kwa hilo na niseme kwamba lengo na dhamira Mhe. Spika, ya kuchangia mswada huu ilikuwa ni kutia chachu tu ya kuwataka Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kuona haja na umuhimu wa mswada huu katika kuwasaidia ndugu zetu pamoja na wananchi wetu, ili kuweza kupata tiba iliyokuwa stahiki, nzuri ambayo ilikuwa ni kero na inaweza kuwaondoshea matatizo yao.

Baada ya hayo Mhe. Spika, niseme naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Salum Haji. sasa nimkaribishe Mhe. Wanu Hafidh Ameir ambaye atafuata baada ya hapo Mheshimiwa Hija Hassan Hija.

**Mhe. Wanu Hafidh Ameir:** Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukutana tena mara nyengine tukiwa katika hali ya uzima, kwa ajili ya kuendelea na kazi zetu za kawaida za Baraza.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa nafasi hii ambayo umenipatia ili na mimi niseme machache katika Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga na Uanzishwaji wa Baraza la Usajili wa Wauguzi na Wakunga.

Mhe. Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa jitihada nzuri ambayo inaichukua kuona kwamba hatua tofauti zinachukuliwa, ili vifo vya mama na mtoto kwa namna moja au nyengine vinapunguzwa.

Mhe. Spika, serikali imeanza na kuondoa malipo ama gharama ambazo zile mwanamke anapokwenda kujifungua anatakiwa kulipia gharama hizo na hiyo ilikuwa ni hatua ya kwanza. Lakini hivi sasa tumekwenda mbali zaidi na kuleta huu mswada ambao utaunda Baraza la Wauguzi na Wakunga, ili kwa lengo lile lile kuwa vifo vya akinamama na watoto vinapungua, kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya wanawake kujifungua.

Mhe. Spika, hii ni hatua nzuri na niseme kwamba kuundwa kwa Baraza hili ni kuwawezesha hawa wauguzi na *midwifery* kuona kwamba kazi zao zinafanywa sasa ki-*profession* na hii inathibitishwa Mhe. Spika katika kifungu cha 5(b) ambacho kinazungumzia kazi za Baraza, ambacho kinasema "kumsajili muuguzi aliyefaulu mitihani yake, kumthibitisha au kuweka viwango vyengine vya usajili".

Kwa kweli hii inaonesha kwamba sasa wauguzi na wakunga wote ambao watahusika na kazi zao ni kwamba watakuwa wanafanya kazi zao kitaamu, kwa sababu watakuwa wameshasajiliwa pamoja na kuthibitishwa kwamba ile kazi wanayofanya wana ujuzi nayo.

Mhe. Spika, sambamba na hayo yote ni vyema pia pamoja na serikali imejaribu kuondoa gharama zile za akinamama kujifungua, pia hivi sasa wameleta mswada ambao utaunda Baraza la Wauguzi na Wakunga kwa pamoja, basi ni vyema kama Mhe. Ali Salum Haji alivyochangia kwamba tukaboresha vitendeakazi pamoja na huduma zote ambazo zinaambatana na kazi hizi.

Mhe. Spika, nasema hiyo kwa sababu hawa wauguzi na wakunga pamoja na kuwaundia mambo haya wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, na yale mazingira magumu ambayo wanayafanyia kazi ile *frustration* yote ya kazi inaishia kwa wagonjwa ambao ni akina mama ambao wanakwenda pale kujifungua. Kwa hivyo ni vyema tukawawekea mazingira mazuri ya kufanyia kazi ili kuona kwamba ile huduma ambayo wanatakiwa watoe kwa kina mama inatolewa ipasavyo.

Mhe. Spika, hakuna muda ambao mwanamke anahitaji *comfort* na ile *nursing care* kama pale anapotaka kujifungua, lakini ukienda katika hizi hospitali zetu na mimi siwalaumu kwa sababu ya mazingira ambayo wanayafanyia kazi na mambo yote yanayoambatana na hayo, zile *frustration* zao za kazi zinaishia kwa wale wanawake ambao wanakwenda pale kujifungua.

Mhe. Spika, majibu ambayo wanawake wanapata pale sio mazuri kabisa, kwamba mtu anakwenda na ugonjwa lakini *nurse* anachangia na yeye kumuongezea yule mgonjwa maradhi kutokana na yale majibu ambayo anayapata. Kwa hivyo tunajua kwamba wanafanya kazi katika mazingira magumu lakini na wao pia waangalie yale maadili yao ya kazi na *ethics* zile zinazowaongoza ili kuona kwamba wanatoa hizi huduma kwa kina mama kama inavyotakiwa.

Mhe. Spika, *some time* tukienda pale Mnazi Mmoja *wallahi* utatamani ardhi ipasuke uingie kutokana na majibu ambayo tunayapata kutoka kwa wauguzi wetu na wakunga. Hivyo ni vyema Serikali ika- *improve* mazingira yale ya kufanyia kazi pale pamoja na kuwawekea vitendea kazi vizuri ili kuona kwamba hizi kazi zinafanywa kwa ufanisi na kwa taaluma kama inavyotakiwa.

Mhe. Spika, Baraza hili pia tunashukuru kwamba sasa hivi kutakuwa na chombo cha pamoja ambacho kitawaunganisha wauguzi na wakunga, jambo ambalo watu hawa wawili wakifanya kazi kwa pamoja hamna shaka kwamba ufanisi katika kazi zao utaongezeka. Kwa hivyo ni jambo jema sana ambalo Serikali imelifikiria.

Jengine Mhe. Spika, ni kwamba naunga mkono hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ambayo imesema kwamba mtendaji mkuu wa Baraza aombe nafasi hiyo, athibitishwe halafu ndio apewe hiyo nafasi na hili sio jambo jipya. Kenya wenzetu wanafanya, Tanzania Bara wanafanya, kwa hivyo na sisi ni vyema kwamba mtendaji mkuu wa Baraza hili ni vyema akachaguliwa.

Lakini jengine Mheshimiwa Spika, tunashukuru kama nilivyosema kwamba Baraza hili litakuwa pia lina - *power* ya kusimamia yale maadili ya wakunga na wauguzi. Kwa hivyo, tunashukuru kwa hili kwa sababu tunajua kwamba sasa kutakuwa na chombo maalum cha kusimamia maadili ya kazi ya watendaji hawa, kama nilivyosema mwanzo kwamba kuna malalamiko makubwa kwamba wauguzi na wakunga hawana huduma nzuri kwa wateja wao ambao ni wagonjwa, na mara nyingi wanakuwa kinamama ambao wanakwenda kujifungua.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono mswada huu mia kwa mia na naomba Wajumbe wenzangu nao waunge mkono. Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**Mhe. Hija Hassan Hijja:** Mhe. Spika, nichukue nafasi hii na mimi kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia mswada huu muhimu sana, mswada ambao nilipokuwa kwenye Kamati ya Ustawi wa Jamii miaka mitatu

nyuma, nilikuwa nikitamani ungetokezea kwenye kamati ile kwa sababu sisi kama Kamati miaka ile mitatu ya nyuma, kwa kweli wakunga na wauguzi mbali mbali walituletea sana kilio chao na leo ndio matokeo ya mswada huu. Kwa hivyo nichukue fursa hii kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani kuipongeza Wizara hii chini ya Waziri mpya Mheshimiwa Rashid Seif Suleiman, na Naibu Waziri wake kaka yangu Mheshimiwa Mahamoud Thabit Kombo kwa jinsi ambavyo wamefikia. Kwanza kuanza tu na *speed* yao ya kuleta mswada huu kwa ajili ya kusimamia maslahi ya W akunga na Wauguzi wetu lakini kwa kusimamia maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, niseme kwamba madhumuni ya mswada huu yemeelezwa vizuri sana na kubwa ni kuwepo maslahi ya wakunga na wauguzi wetu, jambo ambalo pengine litaondosha ile migogoro na migomo mbali mbali ambayo wakunga wetu walikuwa wakifanya siku hadi siku, ni uungwana tu wa wafanyakazi wetu hawa walikuwa wakivumilia lakini kwa kweli walikuwa na hali ngumu, walikuwa hawathaminiki kiasi hicho na walikuwa wakifikia hatua sasa ya kuamua kugoma jambo ambalo kwa kweli liliashiria maisha magumu kwa Wazanzibari wetu. Sasa pengine mswada huo chini ya usimamizi wa Wizara hii utaleta majibu ya wafanyakazi wetu hawa, wasomi wetu hawa na pia utaleta majibu kwa wananchi wetu wa Zanzibar ambao wanahitaji kupata huduma nzuri ambazo hazina malalamiko, hazina maudhi pale wanapokuwa na matatizo ya kuumwa.

Mhe. Spika, kwa hivyo mswada huu unakusudia kuleta majibu muafaka kwa wafanyakazi wetu hawa na sio tu kwa wao lakini kwa Wazanzibari wote kwa ujumla. Mhe. Spika, nianze kwanza kwenye kifungu cha tatu wenzangu wamezungumza lakini nilidhani kwamba kifungu cha tatu kuanzishwa kwa wakala wa Serikali ambao watajulikana kwenye Baraza la Wauguzi pamoja na wakunga. Ningeshauri kwamba wakala wa Serikali aipate tafsiri kwenye hatua ya tafsiri hili liwekwe wazi wakala Serikali inao, kwa sababu hili neno Serikali lilichomoza kwenye kifungu cha tatu lakini kwenye tafsiri hatukuliona. Kwa hivyo napendekeza kwamba neno wakala wa Serikali pia liwepo.

Mhe. Spika, kifungu cha (4)1(a) kiko wazi kwamba Mwenyekiti ambaye atakuwa na cheo cha uandamizi wa masuala ya wauguzi na wakunga na uzoefu wa miaka kumi na tano, Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti huyo wa Baraza ukiangalia kazi zake kazi moja ya baraza sehemu (g) inasema, "kuthibitisha mafunzo na mitaala ya wauguzi na wakunga". Sasa Mwenyekiti ambaye ni muandamizi ana uzoefu miaka kumi na tano lakini haikutajwa elimu yake Mheshimiwa Spika, huu si wakati tena wa kuficha mambo tuweke wazi kwamba Mwenyekiti huyu atakuwa na elimu isiyopungua stashahada ya

uuguzi na ukunga, tuweke sifa mwanzo hatuwezi kwamba Mwenyekiti huyu wa Baraza ndio hatimae atasimamia mitaala ya wasomi hawa lakini eti na Afisa muandamizi tu ana uzoefu lakini elimu yake hatuijui.

Kesho kutwa anachukuliwa Hija hapa alikuwa mwalimu wa nasari anakuwa ni Mwenyekiti wa Baraza la Wauguzi haiwezekani, lazima tuwe na sifa ambazo zitazungumzwa wazi wazi awe na elimu ambayo haipungui stashahada kwa fani hii ya uuguzi na ukunga, pamoja na sifa ile ya uzoefu ambao ni miaka kumi na tano ya kazi.

Mhe. Spika, suala jengine niende ukurasa wa thalathini na nne, kifungu cha tano (g)(q) na (r) vyote vina madhumuni mamoja, kifungu (g) naomba nisome, "Kuthibitisha mafunzo na mitaala ya wauguzi na wakunga". Kifungu (q) kinasema; "Kuanzisha, kusimamia muhtasari mitaala ya masomo na mafunzo ya wauguzi na wakunga" na kifungu (r) "Kutoa na kusimamia miongozo ya kufundisha mafunzo ya wauguzi na wakunga"; vyote hivi vifungu vitatu vina maana moja. Kwa hivyo Mhe. Spika, napendekeza kwamba vifungu hivi vitatu sasa vifungwe kiwa kimoja kisomeke kama ifuatavyo, kwamba kutunga kuidhinisha, kusimamia mitaala ya fani ya uuguzi na ukunga.

Mhe. Spika, kifungu (6) (2) naomba nisome. Bila ya kuathiri madhumuni ya kifungu kidogo cha kifungu hiki Baraza linaweza kuanzisha kamati zifuatazo:-

Kamati ya mwanzo ambayo imetajwa hapa ni kamati ya fedha hii naunga mkono iwepo, Kamati ya pili ni Kamati ya elimu na taaluma nasema iwepo, kamati ya tatu ni Kamati ya miiko na nidhamu, naomba iwepo kamati ya nne ni mipango sera na utafiti. Lakini Wizara imesahau kazi muhimu sana ya Baraza lazima kuwa na kamati ya maslahi ya wauguzi na wakunga tusiweke mambo ambayo yatainufaisha Wizara tu, tuweke mambo ambayo yatanufaisha wasomi wetu kuwe na kamati maalum ambayo italinda maslahi ya wauguzi na wakunga, ili kuondosha migogoro, kuondosha madhila na kuondosha matatizo ya wauguzi wetu na wakunga.

Mhe. Spika, tarehe kumi na nne hadi kumi na saba mwezi huu nilikuwa Dubai, nilitembelea pale ofisi ya Ubalozi mdogo wa Tanzania tulishuhudia Mzanzibari mwenzetu naomba nisimtaje aliondoka hapa kwa ajili ya kufanya kazi nje ya nchi kazi ya uuguzi, aliondoka hapa kwa kufuatilia maslahi baada ya kufika kule akapewa kazi ya mama wa nyumbani. Maana yake aliondoka hapa kwa shida ya kwenda kufanya kazi ya uuguzi kwamba maslahi madogo Zanzibar lakini kufika Dubai kazi aliyopata kule ni kazi ya mama nyumbani, sasa ubalozi unamsaidia huduma ili aweze kurudi Zanzibar. Kwa hivyo

lazima kuwe na kamati maalum ambayo italinda maslahi ya watu wetu hawa ili wasiondoke ovyo ovyo na wanapokuwa na shida basi wapate maslahi yao ndani ya nchi na nje ya nchi.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba kamati ya maslahi ya wauguzi na wakunga lazima iwepo kwenye kamati za kudumu za Baraza hili kwa ajili ya maslahi yao, lakini vile vile kanuni sasa iweke wazi uwezo wa Baraza kuunda kamati hizi kamati tano ni muhimu sana lakini baadae wasije wakapata mwanya wakaunda kamati zaidi ya arubaini. Hii maana yake nini, maana yake zitaathiri mapato ya Baraza, zitaathiri mapato ya Serikali na kwa hivyo kuwe na ukomo wa kuundwa kamati. Kwa hivyo kanuni ya sheria hii Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba iweke wazi idadi ya kamati hizi ili kulinda maslahi ya watu wetu bila ya wasi wasi.

Mhe. Spika, kifungu cha (6) (1) na (4) kwa mtazamo wangu kinafanana, kwa hivyo kiwekwe sawa na kiwe kifungu kimoja na hivyo hivyo kifungu cha (6) (6), muundo utaratibu *times* naomba tupatiwe ufafanuzi wa hili neno "*times"* maana yake sijalielewa ili likae sawa kwa ajili ya kulinda maslahi ya watu wetu.

Mhe. Spika, kifungu cha tisa kuna sifa za Mrajis, hapa zimeandikwa kwamba mwenye Stashahada ya uuguzi au ukunga au fani yenye kuhusiana na wauguzi au ukunga, Mheshimiwa Spika, kifungu hiki mimi sikikubali nashauri na napendekeza sifa ya Mrajis lazima awe na shahada ya kwanza na kwa nini? Chini huku kifungu cha kumi na moja wasaidizi wake wana shahada lakini yeye mkubwa ana stashahada ni dhahiri kwamba haiwezekani mkubwa ana Diploma, lakini mdogo ana *Degree*. Nashauri kwamba mkubwa ndio awe na *Degree* na mdogo angalau awe na stashahada ya fani ya uuguzi na ukunga na sifa jamani ziwepo kwa sababu ndugu zetu wamesoma hawa, musiandae mazingira ya kutafuta watu waliostaafu ambao kuwa wana uzoefu wa miaka sitini lakini hawana elimu tukaacha ndugu zetu ambao wamesoma. Kwa hivyo, lazima sifa ya *Degree* na Diploma ziwekwe wazi ili watu wetu waweze kufanya kazi na wafaidike na wa-*enjoy* na ile taaluma ambayo wameipata.

Mhe. Spika, hakuna fani ngumu kusoma kuliko fani ya udaktari. Kwa hivyo kama hatuwaenzi hawa watu waliosoma na tukatafuta watu kwa ujanja tu wa kupenyeza watu wenye sifa za uzoefu fulani mzoefu alikuwa anakosha vidonda muda mrefu haiwezekani, lakini na sifa za taaluma ziwekwe ili watu wetu waweze kupata manufaa ambayo yanastahiki.

Mhe. Spika, mwisho kabisa ningeshauri mswada huu kwa kweli unatambua wakunga na wauguzi wenye taaluma ya Diploma na kuendelea juu, lakini

Wazanzibari wasisahau kwamba wazee wetu vijijini huko wala skuli hawakusoma, lakini wamekuwa wakitoa mchango mkubwa kuzalisha watu wetu majumbani. Ni nani asiyetambua hapa kwamba miaka zaidi ya arubaini, wakunga hawa wa kienyeji ndio ambao wametuzalisha sisi na hatimae leo Wazanzibari wamekuwa na afya nzuri.

Kwa hivyo nashauri Mheshimiwa Spika, mswada huu kuwe na kipengele maalum Baraza liwatambue watu hawa kwa masharti maalum na kuwapa vibali maalum, kwamba wafanye kazi hata kama hawana shahada au stashahada kwa ajili ya kuokoa maisha ya watu wetu. Mheshimiwa Spika, kwa mshahara huu wa laki moja na arubaini mtu aliyesoma na shahada yake hatobakia kwenye Wizara akafanya kazi kwa ufanisi, kwa hivyo wazee wetu vijijini wawezeshwe wadhibitiwe chini ya Baraza wafanye kazi kwa mashirikiano na Baraza chini ya uangalizi wa Baraza ili watoe huduma kwa wananchi wetu bila ya matatizo, vyenginevyo Mhe. Spika, Wazanzibari watapata tabu na madhara yaliyokusudiwa vifo vya watoto vitaongezeka na si lengo kwa Serikali.

Nashauri kwamba mswada huu kuwe na kipengele maalum kiwatambue wafanyakazi hawa ili wawe na nafasi maalum. Mheshimiwa Spika, likikubalika hilo la kuwa na kipengele maalum kwa ajili ya kuwatambua wakunga wetu wa jadi, mswada huu nitaunga mkono halikukubalika mimi sitokuwa sehemu ya kuunga mkono mswada huu.

**Mhe. Abdalla Moh'd Ali:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kunipa fursa ya kusema machache katika mswada huu uliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, najua kwamba sasa tunataka kuvaa vaa soksi kwa ajili ya kuimarisha au kutenda kazi zetu vizuri wazungu wanasema, wangine Wakuu wa Walimu nawaambia kula kula soksi, na mswada huu umekuja nahisi kwa lengo hilo la kuona wafanyakazi wetu wanawajibika. Lakini kwa kila mwenye kwenda mbio sana huwa anatoka jasho sana, mara nyingi mwisho wa mbio huwa anatakiwa anywe maji mengi. Sasa mswada huu umekuja utakuwa una walinzi wa kuwaangalia hawa ambao watakuwa wanafanya kazi, usiangalie kuwapangia kazi nyingi tu tuangalie pia na maslahi yao yatakuwa namna gani.

Mhe. Spika, mimi kidogo nijikite katika muundo katika muundo hapa wa Baraza tumependekeza Mkuu wa Chuo cha Uuguzi Zanzibar, ni mawazo yangu kwamba katika sheria hii itaruhusu vyuo binafsi vya uuguzi. Sasa moja kati ya wajibu wa Baraza ni kutunga mitaala kwa ajili ya wanafunzi watakaokuwepo vyuoni pale, sasa ikiwa tutamchukua muuguzi mmoja tu ambaye atatoka chuo hiki cha serikali nafikiri itakuwa ni kinyume nyume.

Sheria hii ingeangalia kwamba wakati wowote tutakuwa na vyuo vya uuguzi katika nchi yetu, wakati wa kutunga mitaala wasije wakagongana wengine wakaona sisi tumeingizwa sisi tumeshirikishwa wengine hawakushirikishwa. Kwa hivyo mimi nahisi tukaiweka kwamba ni wakuu wa vyuo vya uuguzi Zanzibar ili kupewa fursa na wao wakaweka mawazo yao katika hiyo mitaala itakayokuwepo.

Lakini jengine Mheshimiwa Spika, sheria hii nahisi kama itatoa fursa kwa watumishi wa umma, aidha kuamua kuendelea na utumishi wao au kuachana na utumishi wao kwa sababu kila mtumishi hapa ama awe muuguzi au awe ni mkunga ni mtumishi wa umma, lakini inawezekana pengine mtumishi huyu akaonelea mimi leo kwa hapa nilipofika sitaki tena nisajiliwe na kuendelea na kazi hii. Sasa sijui sheria hii inamlazimisha huyu ambaye ni mtumishi wa umma hivi sasa lazima asajiliwe au atakuwa na hiyari ya kusajiliwa na kutosajiliwa, na kama atakuwa na hiyari yake akiamua yeye kutokuendelea kwamba mimi sitaki tena kuendelea na utumishi wa umma kuwa muuguzi au kuwa mkunga je, haki zake atahesabika vipi kama kastaafu yeye katika kada hii na atapewa haki zake au akikataa kuendelea na kazi hii atahesabika vyenginevyo na kukosa haki zake?

Ningemuomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa hili ukalifafanua lisije likawahangaisha watumishi wetu. Kwa sababu nahisi pia itatoa fursa kwa wengine labda kuondoka na kwenda sehemu nyengine. Sasa je, sijui Wizara imejipanga imeona hivyo kwamba fursa hii itatoa fursa pia kwa wale ambao hawataki kuendelea kufanya kazi katika nchi hii, kuondoka baada ya kutokuwa tayari kusajiliwa katika hilo Baraza la Uuguzi.

Mhe. Spika, lakini nije kidogo katika kifungu cha 15. Kifungu hiki kimetoa fursa kwa wageni yaani mgeni anaweza akaja hapa akaomba yeye kusajiliwa na akaonesha vielelezo vyake. Sheria hii inasema kwa mtu ambaye anatoka nje ya nchi atalazimika kuonesha vitu hivyo, lakini pindipo akiwa hana vitu hivyo afanyiwe mtihani.

Mhe. Spika, mimi nafikiri Mhe. Waziri lazima afikiri tena, kwa sababu viwango vya elimu ulimwenguni vinatofautiana. Kuna wengine wanaipenda nchi hii na huwa watakalofanyiwa lolote au mishahara yoyote pengine watakayopewa wataridhika wakiangalia hali katika nchi zao. Sasa kumruhusu mtu tu kuja hapa akaonesha cheti, mimi nafikiri sio utaratibu mzuri. Kama mtu amekuja hapa hata kama atakuwa ana vyeti vyake basi ni lazima tuanzishe utaratibu wa kumfanyia mitihani. Sio aje aoneshe vyeti na kukubalika moja kwa moja.

Mhe. Spika, kama kaja hapa na akawa hana hata cheti basi huyo asifanyiwe mtihani moja kwa moja, huyo awekwe yeye katika fungu jengine asihesabiwe hasa. Itakuwaje mtu atoke huko awe hana ushahidi wowote afike hapa aombe kufanyiwa mtihani wa udaktari na aingie katika kusajiliwa. Hii Mhe. Waziri mimi nafikiri haikubaliki. Kwa hiyo mtu kama kaja hapa hana lolote aje aombe tu huyu asiruhusike moja kwa moja. Kwa hiyo na huyu ambaye atakuja hana vyeti basi Mhe. Spika, lazima afanyiwe mtihani sio aje na vyeti vyake atuoneshe tu.

Mhe. Spika, tunajua utaratibu wa ulimwengu ulivyo watu wanatumia *computer* kwa njia wanazozijua wenyewe na utaalamu huo unaongezeka, kupata cheti ni rahisi sana hivi sasa ulimwengu wetu huu wa leo. Kwa hivyo tusiamini hayo ni lazima mtu akija hapa kama anatoka nje ya nchi afanyiwe utaratibu huo na hii pia itaondosha ile ya watu kuingia katika nchi hii wakapatiwa ajira. Kwa sababu inawezekana mahospitali binafsi wakatumia fursa hii. Wazalendo ambao hivi sasa tunao karibu *batch* mbili zimetoka lakini mpaka hivi leo hawana ajira. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri kipengele hiki kiondoshwe moja kwa moja, uweke tu kwamba mtu atakapokuja hapa basi afanyiwe mitihani.

Mhe. Spika, hivi sasa tunaboresha uuguzi na ukunga. Jambo la kusikitisha ni kwamba hadi hivi sasa hatujafikia lengo hasa katika kitengo cha Ukunga. Nahisi tunasomesha zaidi wanaume kuliko wanawake, *ethics* zetu hazitaki kuwa mkunga awe ni mwanamme. Lakini wataalamu wa hali ya juu hivi sasa katika vitengo vya ukunga unakutia ni wanaume. Kwa hivyo nahisi kuna haja hivi sasa Mheshimiwa Spika, ya kuona kwamba wanawake wanapewa fursa zaidi ya kusomeshwa ili wawe wakunga kulikoni wanaume, hasa katika sekta hii ili kwenda zaidi na yale maadili yetu.

Mhe. Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja.

**Mhe. Asha Bakari Makame:** Mhe. Spika, kabla ya yoyote na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kukutana tena katika mustakbali wa kujenga mambo yetu kwa taifa letu. Pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia Mswada huu ambao ni roho ya binaadamu.

Mhe. Spika, niwaunge mkono wale wenzangu wote ambao wamechangia kwa yale yote ambayo wameyataja katika Mswada huu. Mimi nitachangia hapa na pale. Kwanza niseme tu Mhe. Spika, sisi tatizo letu kubwa huanzisha jambo lakini bado hatujafanya utafiti na huanzisha jambo ambalo hatujalifanyia kazi. Naomba sana Wizara husika kwamba tumeanzisha Mswada huu ambao ni roho ya binaadamu. Kwa sababu Mkunga na Muuguzi anaangalia roho ya

binaadamu itatoka tokaje, pamoja na kwamba mwenyewe Mwenyezi Mungu ndio muwezeshaji.

Mhe. Spika, sasa ningeliomba sana Wizara hii husika Mhe. Spika, iwe makini katika suala hili lililoanzishwa. Niwaombe Wauguzi pamoja na Wakunga wawe makini katika kutenda kazi zao na shughuli zao hizi ambazo zitawajibisha mambo yote ambayo yameainishwa katika Mswada huu.

Mhe. Spika, jengine niwaunge mkono wenzangu kwamba kwa kweli unapokwenda hospitali sisemi wauguzi wote au wakunga wote, kuna baadhi ya wauguzi na wakunga maneno yao sio mazuri. Mtu anakwenda anaumwa na uchungu na uchungu tunasema kwamba mambo yote mwenyewe Subhanahuu Wataala yupo, lakini hili anakuwepo hasa hivi, hatumuoni tu, ingawa sehemu zote yupo, lakini hili anakuwepo.

Unapomtolea maneno mtu katika wakati ule mgumu kwa kweli humtendei haki, sisemi wote nasema narudia tena ni kwamba baadhi ya Wauguzi na Wakunga. Kwa hivyo jambo lile usimtolee maneno, "ulivyokutana na mumeo usiku mimi nilikuwepo, ulitaka nini, ulitaka nini?" Mhe. Spika, yote hayo yanatokea. Kwa hivyo ni vyema mgonjwa ambae anakwenda kuzaa basi umpe maneno mazuri, kwa sababu pale roho toka nitoke. Niwaombe Wakunga pamoja na Wauguzi wote.

Mhe. Spika, jengine tujidhatiti vizuri katika sheria hii, tuwe na vitendea kazi vyenye uhakika, kuwa na ukaguzi maalum katika hivyo vituo ambavyo vitaweza kufanya kazi. Tatizo letu ni kwamba hatupitii mara kwa mara katika shughuli zetu. Sasa niiombe Wizara husika Mhe. Spika, jambo hili ni muhimu.

Mhe. Spika, jengine wazee wetu wa zamani ambao ndio walikuwa wakunga, wakunga wa zamani na mimi niunge mkono kwamba hiyo miaka ya nyuma hospitali haikuwa kila kijiji na hasa vijijini niseme kulikuwa hakuna hospitali kila kijiji wala kulikuwa hakuna wauguzi wanaokwenda kupelekwa kwa magari. Takriban wengi wetu miongoni mwetu tumezalishwa na wakunga wa jadi wa zamani watu wazima ambao ndio waliokuwa wanafanya kazi hiyo. Tena walikuwa majasiri na walikuwa madhubuti na walikuwa na tahadhari kubwa sana, ulikuwa husikii kabisa watoto kufa ovyo ovyo.

Mhe. Spika, kwa hivyo na mimi naunga mkono suala hili, wapatikane hawa na kuwe na Kamati hii vile vile iwaone kwamba wakunga wa zamani wazee wetu wale wakunga wa jadi wasitupwe, waangaliwe vizuri ili na wao waweze kunusuru hasa kwa upande wa vijijini, wengine wanazalia magarini, wengine

wanazalia njiani na wanazalishwa na hawa hawa wakunga wetu wa jadi wa zamani hawa.

Mhe. Spika, kwa hivyo hili naliomba sana na naiomba sana Wizara husika walitilie mkazo na kwa kweli liwemo katika mambo ya maorodhesho ambayo yameorodheshwa humu. Kwa hivyo niseme hilo nilitilie mkazo.

Mhe. Spika, nije kwenye maslahi, sio maslahi ya fedha tu ni maslahi ya wauguzi na wakunga wote ambayo yawezakuwa *by laws* ndogo ndogo au kuwe na kitu ambacho kitawalinda wao lakini pia kitalinda kwa upande wa serikali. Maana yake na sisi tuna matatizo, tunasomeshwa na serikali hii lakini baadaye tunaona serikali hii siwezi kuitumikia. Kuwe na sheria maana yake kuwa na *by law* ambayo itambana mtu kwa kweli watu wengi sana, madaktari wengi sana tumewasomesha na kusomea udaktari ni jambo kubwa sana sio miaka miwili wala mitatu ni miaka mingi. Serikali inachukua juhudi kutoa fedha nyingi kuwasomesha lakini baadaye wanakimbia. Sasa sikijui kitu gani ambacho, lakini wasomeshwe mambo ya uzalendo, uzalendo ni muhimu Mheshimiwa Spika.

Mhe. Spika, naiyomba Wizara husika watu sasa hivi watilishe mkataba hasa, kuwe na mkataba maalum ambao utawezesha vijana wetu kutokukimbia upuuzi, kutokuhama hama upuuzi na kutokufanya mambo ambayo hayalete maslahi ya nchi ambayo imechukua jitihada ya kukusomesha wewe mpaka ukafika hapo, kulikuwa na wengi lakini imeona ikusomesha wewe ili uweze kusaidia nchi yako.

Mhe. Spika, na mimi nitilie mkazo tuwe *serious* kwenye mambo haya tusiwe na shahada tu hivi hivi za ovyo ovyo. Tuwe na shahada ambazo zitahakikisha kwamba wewe kweli ni muuguzi, amesema hapa Mheshimiwa Hija hapa. Hili si jambo la kulifanyia mchezo, hili ni jambo la ambalo kwa kweli la kulitia maanani. Leo usije ukampa mtu cheo kwa kusema kwamba ana uzoefu. Uzoefu una *matter* lakini kwenye mambo haya ya uzalishaji na mambo ya udaktari na mambo ya upasuaji si mambo ya kusema awe na uzoefu tu. Lazima asomee kitu ambacho kwa kweli kitaleta maslahi ya yule ambaye anamfanyia.

Mhe. Spika, baada na mimi ya kusema hayo niunge mkono Mswada huu mia kwa mia ili tuuboreshe zaidi kwa kuweza kuufanyia kazi ipasavyo. Asante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Mhe. Asha Bakari tunakushukuru, Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Asante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu juu ya Mswada wetu huu ambao upo mbele yetu.

Mhe. Spika, mimi vile vile nichukue fursa hii kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uteuzi wake ambao ameufanya juu ya mabadiliko ya Mawaziri. Lakini pia Mwanasheria Mkuu, lakini hasa hawa kwa Naibu Waziri somo yangu hapa ambaye ni Naibu katika Wizara hii ambaye kwa leo tunaichangia hapa.

Mhe. Spika, mimi nianze kwanza katika jina la huu Mswada wetu. Mswada wetu unasema ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga, Uanzishwaji wa Baraza la Usajili wa Wauguzi na Wakunga.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kusaidiwa zaidi kwa nini tuwe na Baraza tusiwe na Bodi au Kamisheni. Mimi nahisi ni jambo la msingi sana kama tungelikuwa tuna Bodi badala ya kuwa na Baraza kama ambavyo hapa ilikuwa imeainishwa.

Mhe. Spika, vile vile, eneo jengine ambalo nilitaka kuchangia ni pale katika ukurasa wa 32 Ibara ndogo ya (4) kwenye orodha ya Wajumbe ambao watakuwa wanaunda Bodi au Baraza hilo. Hapa kuna idadi ya wajumbe kutoka (a) mpaka (k) ukiangalia hawa ni Wajumbe zaidi ya kumi. Mimi nahisi ni wengi kuunda Bodi hii.

Mhe. Spika, tusisahau kwamba tuna baadhi ya Bodi ambazo wakati mwengine zinashindwa kuendelea na shughuli zake kutokana na kwamba mafao yale ya kulipana inakuwa hatuna. Sasa tunapokuwa na bodi kama hii kubwa kama hivi nahisi kwamba itakuwa vile vile yale matatizo ambayo tunayo yanaendelea na hapa yatazidi kuongezeka. Sasa mimi ningependekeza Wajumbe hawa badala ya kuwa zaidi ya kumi tuwapunguze wawe wajumbe saba au tisa. Wapo wengine nahisi kwamba wapunguzwe.

Jengine Mhe. Spika, ukiangalia kazi ya Baraza maisha yote inakuwa ni katika masuala mazima ya kutunga kama sheria na mambo mengine mengine. Lakini hapa kuna ufatiliaji na utendaji. Sasa kila nikiangalia nakuta kwamba iko haja hata hili jina la huu Mswada wenyewe badala ya kuwa ni Baraza sasa tufanye kwamba iwe ni Bodi.

Mhe. Spika, lakini ukirudi katika ile orodha ya Wajumbe ambao wanakuwa wanaunda ile Bodi yenyewe. Ukiangalia hao wauguzi wote wamo humo pamoja na Mkuu wa Chuo, Mwakilishi kutoka Jumuia ya Wauguzi,

Wawakilishi kutoka Jumuia ya Wakunga, wahudumu, yaani watu wote wamo humu. Sasa sijui nani anakuwa *regulator* hapo.

Mhe. Spika, ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie zaidi. Nahisi kwamba tungetengeneza utaratibu pamoja na Wajumbe ambao tutakuwa tunahisi kwamba wawemo katika Bodi hii, awepo na *regulator* ambaye atakuwa anashughulikia katika masuala haya na kuwa yeye anaweza kutoa maelekezo ambayo yanaweza kusaidia taasisi hii ikaweza kwenda vizuri na kuweza kuendesha shughuli zake kwa mujibu wa uhalisia ambao tulikuwa tunaukusudia.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Spika, tunapokuja katika kifungu cha 37 hichi kifungu naomba nikinukuu Mhe. Spika. Kifungu cha 37 kinasema:

37. "Mtu yeyote au Taasisi itakayoainisha mafunzo ya uuguzi au ukunga au anatoa taaluma yoyote katika kada ya uuguzi au ukunga bila ya kuthibitishwa na Baraza, ametenda kosa na akitiwa hatiani atalazimika kulipa faini isiyopunguwa milioni tatu au isiyozidi milioni tano fedha za kitanzania au kifungo kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja faini na kifungo."

Mhe. Spika, ukiangalia hapa katika kipengele hichi hii Bodi itakayokuwa inafanya kazi hii ipo kwetu na hizi sekta nyengine ambazo zitakuwa zinatoa matibabu yaani kama tunasema ni kliniki au hospitali nyengine ndogo ndogo zitakuwa zinategemea hapa. Hapa tayari patakuwa panaushindani Mhe. Spika, hatuhisi kwamba hii itakuwa ni njia moja wapo ya kuvidhibiti na kuzifanya hizi hospitali ndogo ndogo zisiweze kufanya kazi kwa uhuru na haki.

Mhe. Spika, naomba haya mambo ambayo tumeyazungumzia Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie maelekezo ya kina ili tuzidi kukubaliana na tuzidi kuboresha Mswada huu ambao umekuja kwetu kwa lengo la kupitisha na baadaye ili iweze kuwa sheria na iweze kutumika katika nchi yetu. Kwa haya machache Mhe. Spika, naunga mkono hoja na zaidi nikishakupata majibu ya haya ambayo nilikuwa naomba maelekezo yake. Mhe. Spika, ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe kuna muda wa dakika kama 20 ambao unawezesha kumtosha Mheshimiwa Mjumbe mmoja akachangia kama ataweza kumaliza, karibuni. Inaonekana tumeridhika.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu ambao umeletwa mbele yetu leo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, sina mengi lakini kuna mambo machache ambayo ningeomba tuyazingatie. Katika Mswada huu hili Baraza lina haki ya kushtaki na kushtakiwa. Mhe. Spika, wauguzi kwa kiingereza ni *nurses* hawa hospitali nzima wameenea kuanzia kufunga kidonda mpaka kwenye *operations* huko. Wakunga wao wana *specialization* yao maalum wanahusika na mambo ya uzazi zaidi, sasa unaposema wanaweza kushtakiwa wakunga na *nurses* wetu ni hawa hawa tulionao sidhani kwamba wanakuja wengine. Na hapa wajumbe wengi waheshimiwa wamesema kwamba kuna vitendo vimekuwa vikifanyika mahospitalini na vyengine bila kufanya utafiti unajua kabisa hii ni dharau. Sasa unapofika mahali hapo kwamba hii ni dharau bila ya utafiti na mtu akapoteza maisha sijui kesi hii kwa Baraza hili na hili Baraza tusisahau ni *affiliation* ya Serikali haliko *independent* yaani ni kama Shirika la Umeme au Shirika la Bandari na hili Baraza ndivyo lilivyo.

Sasa hii kushtaki na kushtakiwa mimi ninajua moja katika vitu ambavyo vitatokea hapa ni hili Baraza au Serikali kujidhatiti zaidi. Kwa sababu kesi ya mahkamani ikaamuliwa kwamba kweli huyu alikufa kwa uzembe sidhani kwamba kuna malipo ya maisha ya mtu, hili sheria hii imezingatia vizuri watu watakuja na kesi na watu wana uwezo mkubwa wa kuendesha kesi hizi mpaka mahkama ya rufaa na mwisho akashinda nani analipa gharama hii. Baraza ndio fedha zake tumeziona zinavyopatikana pale. Je, inapotokea hukumu hiyo kwamba huu ni uzembe wa mkunga ni uzembe wa muuguzi, muuguzi mwenyewe hata ukimfukuza kazi bado haijakuwa malipo ya roho ya mtu inakuwaje hapo. Sasa ni vizuri atakapokuja hapa atueleze litakapotokea kwa sababu tunapofanya jambo tusiangalie hapa tu tuangalie na mbele zaidi, litakapotokea jambo kama hilo na sisemi kwamba halitotokea kwa sababu limekuwa likitokea.

Kuna kesi moja wakati wa kujifungua mkunga inasemekama katika kumpokea huyo mtoto alim-*twist* sasa mtoto anapozaliwa anakuwa ni tepe tepe ikasemekana ile kum-*twist* ile *brain* nayo ika-*twist* na ikawa ndio sababu ya mtoto ama kuwa zezeta au vitu kama hivyo. Sasa nasema hii mtu anaweza kuichukua kama ni kesi, mwanangu amekuwa *handled* vibaya badala ya kuzaliwa katika hali ya kawaida amezaliwa ni zezeta, sasa mnanilipa nini? Sasa nauliza mimi je, inapotokea kitu kama hicho au mtu amefariki kwa uzembe wa *nurse* au mkunga nani atalipa gharama hii ni Serikali au ni nani. Ninafikiri Waziri atakapokuja hapa atuelezee vizuri ili sheria hii tutakapoipitisha isije ikaonekana kwamba haya hatukuyazingatia.

Jengine bahati nzuri katika kifungu cha 5(h) cha mswada huu hizi ni kazi za Baraza zitakuwa (h) inasema:

Kwamba kushirikiana na mamlaka nyenginezo katika masuala yanayohusiana na mafunzo na elimu ya uuguzi.

Sasa mimi hapa nilitaka tuongeze neno kwa sababu mafunzo na elimu ni kitu kimoja lakini washirikiane kwa vitu hivi viwili tu isiwe na shughuli zenyewe, hizi shughuli zenyewe hizi kwa sababu elimu au mafunzo ni moja katika shughuli zao hawa. Lakini hizi shughuli nyengine zenyewe za ukunga na uuguzi kwa nini wasiweze kushirikiana na mamlaka nyenginezo. Kwa hivyo nilikuwa nashauri kwamba kama tukiongeza neno jengine pale shughuli hizi tunazozungumza hapa isiwe tu ni mafunzo na elimu. Jengine naona limerekebishwa hapa katika (i) kutoa halafu *renew* maana yake kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza lakini naona kamati wameliona hilo. Mimi nilikuwa nasema kwamba kama ilikuwa tafsiri ya neno ku-*renew* ni kulifanya upya kama neno la Kiswahili halikupatikana kwa hili neno ku-*renew*.

Katika kifungu cha 4 Mhe. Spika, muundo wa Baraza. Muundo wa Baraza wametajwa hapa lakini kwenye (e) kuna Mwakilishi kutoka Jumuiya ya Wauguzi na Wakunga Zanzibar maana yake hii ni Jumuiya moja. Ile Jumuiya ni ya wauguzi na wakunga. Lakini (f) mwakilishi kutoka Jumuiya ya Wakunga, sasa suala langu nauliza hakuna Jumuiya ya Wauguzi. Jumuiya ya Wakunga hapa imekuwa *identified* lakini Jumuiya ya Wauguzi na Wakunga vile vile imekuwa *identified*. Hakuna Jumuiya pekee ya Wauguzi. Sasa kama imewekwa Jumuiya ya Wakunga basi na Jumuiya ya Wauguzi iwepo.

Lakini katika Wajumbe hao waliotajwa kuna mmoja humu sijui amewekwa wapi au sijui ndio hii iliyokusudiwa wajumbe wawili kutoka jamii ambayo kwa uzoefu wao wanaweza kusaidiana na Baraza. Lakini mimi nilikuwa nasema hapa tuwe *clear*. Waheshimiwa wenzangu hapa wamesema kwamba wengi wetu hapa na walioko nje ya hapa tumezaliwa katika hali ya kienyeji, hii habari ya hospitali ni mambo ya siku hizi. Lakini *since time being immemorial* jadi na jadi watu wanazaliwa huko hakuna habari ya hospitali wengine wanapona wengine wanakufa, lakini lazima tukubali kwamba wako wakunga wa kienyeji ambao uzoefu wao unashinda hao wakunga ambao wamesomeshwa.

Wengine ni wataalam kiasi ambacho hao wakunga waliofundishwa basi *intensive* yao ile kujifunza kwao wanapelekwa kwa hao wakunga wa kienyeji, ili na hao wakunga wa kienyeji nao tuwatambue waone kama kumbe na Serikali wanatujua. Mimi ningeshauri kwamba miongoni mwa wajumbe wa Baraza hili awe Mwakilishi miongoni mwa wakunga wa kienyeji. Na Wizara ya Afya wanawajua maana yake si kitu cha kutafuta hicho wanajua kabisa kwamba kijiji hiki kuna bibi huyu kuna hivi kuna hivi, kuna hivi watafute mmoja miongoni mwao hata kama hao hawana Jumuiya lakini nina hakika

huyo mmoja au pengine wanayo nina hakika huyo mmoja atawakilisha sana uzoefu wake katika miundo hiyo.

Mhe. Spika kama nilivyokwambia mimi sikuwa na mengi lakini naomba mchango kwa leo uishie hapa. Ninakushukuru sana.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe inaonekana kama tumefikia pahala tumesharidhika kumbe Mhe. Fatma Mbarouk Said anataka atumie dakika kumi kutoa mchango wake, karibu.

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia machache kwenye Mswada wa Sheria na kwa kuanzia kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia Mswada huu wa Sheria ya kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga na uanzishwaji wa Baraza la Usajili wa Wauguzi na Wakunga Namba 9 ya mwaka 1986. Vile vile niishukuru kamati ambayo imewasilisha hapa kwetu sisi kwa ufasaha mapendekezo ambayo wameyaona na marekebisho mbali mbali.

Kwa kweli Mhe. Spika, mswada huu umekuja kwa wakati muafaka na kwa sababu Mhe. Spika, hii kazi yetu kuipitia miswada hii na kuirekebisha na kuiboresha hii ni moja ya kazi ya Baraza la Wawakilishi ambao sisi wajumbe wake tumeingia humu kwa niaba ya wananchi na sisi tuseme kwamba ndio wananchi wenyewe ambao sisi tuna majukumu hayo ya kupitisha miswada hii ili mambo yetu yaende kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, nikianza na sehemu ya kwanza ambayo ni ya utangulizi mimi kwa upande wa utangulizi sina matatizo yoyote nimesoma kwa ufasaha na nimeona kwamba hii ni lazima na jambo lolote linapoanza lazima liwe na kianzio na tunaona ni namna gani mswada huu umeanza kwa jina na ufafanuzi kwenye sehemu yake ya kwanza.

Mhe. Spika, nipongeze kwa Wizara kuona kwamba sehemu ya pili imeenda kwenye kuanzishwa kwa Baraza. Hii niseme kwamba itakuwa ni *pillar* ya sheria hii kwamba kuweko na chombo hiki ambacho kitaanzishwa kisheria kwenye Mswada huu wa Sheria ya Uuguzi.

Mhe. Spika, nimeona namna gani hapa muundo wa Baraza ambalo limeundwa kwa wajumbe wake hao lakini vile vile Mhe. Spika, niende kwenye sehemu yake ya tatu ya sheria hii ambayo kuna uongozi wa wafanyakazi wa Baraza.

Mhe. Spika, pahala popote ili pawe na ufanisi basi kunahitajika kuwe na uongozi. Hapa Mhe. Spika, kuna kifungu cha 11 ambacho kinasema; Naibu

Msajili. Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, kutakuwa na Naibu Wasajili wawili wa Baraza mmoja kutoka Pemba na mmoja kutoka Unguja. Kwa kweli haya ni mambo ya ufanisi zaidi na niipongeze Wizara kwa kuona kwamba kila mahala panapata haki yake. Kwa sababu kuwasajili hawa wawili Pemba kukawa na Manaibu, mmoja ambaye atakuwepo Unguja na mwengine atakuwepo Pemba, hili ni jambo zuri kabisa kwa sababu kunakuwa na uwiano na kunakuwa hakuna matatizo ya hapa na pale. Kwa hivyo mimi niseme kwamba nimeunga mkono kwenye sehemu hii ya uongozi wa wafanyakazi wa Baraza.

Mhe. Spika, nikienda sehemu ya nne usajili na leseni ni jambo la kupongezwa kwamba mahala popote ni lazima kuwe na kitu au *identification* yoyote ile ambayo inakufanya wewe kwamba umeingia pale kihalali. Kwa kuwepo kwa sehemu hii ya usajili pamoja na leseni mimi ninaiunga mkono kwa niaba ya wananchi wangu ambao wamenichagua wa Jimbo la Amani na ni kazi yangu ambayo nasema kwa niaba yao na mimi nasema kifungu hiki nimekubali.

Vile vile, kifungu cha 15 kwa mujibu wa masharti kwenye sehemu hiyo hiyo ya nne ambayo ina usajili, inasema kwamba; kwa mujibu wa masharti ya sheria hii mtu yeyote ataweza kusajiliwa kuwa muuguzi na mkunga baada ya kutimiza masharti yaliyopo kwenye kifungu hiki. Hizi ni moja ya sifa ya kusajiliwa kwa mtu ambaye anataka kuifanya kazi hii ya uuguzi au ukunga.

Mhe. Spika, sehemu ya tano ina masharti na nidhamu. Mhe. Spika, kwa kweli kila pahala panatakiwa pawe na nidhamu na hata yale maadili ya ile kazi yenyewe. Kila kazi ina maadili yake niseme hata wale wezi basi wanakuwa na maadili yao kwamba ukikamatwa huko umeshaiba na wenzio basi kuna maadili pengine wao watakuwa wameweka kwamba hata kama umekamatwa basi usimtaje mwenzio. Kwa hivyo mimi ninaamini kwamba hii sheria imezingatia mambo yote ambapo itakuwa umeenda kinyume na maadili ya kazi basi itakuwa kwa kweli umefanya kosa na mtu akifanya kosa Mhe. Spika, ni lazima aadhibiwe kutokana na lile ambalo amelikosa. Na hii kazi ni nzito, wauguzi wana kazi nzito na hasa wale wakunga.

Kwa hivyo Mhe. Spika, naunga mkono sheria hii, namna ilivyojipanga kwa vifungu mbali mbali na yote haya ni kutaka kuboresha zaidi. Kwa sababu sheria imeonekana kwamba imefanywa mabadiliko mara nyingi. Kwa hivyo ili jambo liende vizuri ni vizuri kuona kwamba baada ya viraka viraka na sasa ikaja sheria nzuri ambayo sasa hivi tutakapoipitisha na niwaombe sana waheshimiwa wenzangu kwenye Baraza hili waipitishe, tuipitishe kwa sote.

Vile vile nimeona Mhe. Spika, sehemu ya sita, masharti ya fedha. Hiki ni kifungu muhimu sana kwa sababu fedha siku zote usipoitunza vizuri kwa

kweli italeta matatizo. Lakini nishukuru sana kwamba hapa kuna fedha hizi za Baraza ambazo zitakuwa ni raslimali zitajumuisha fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi ambao ni sisi. Kwa hivyo pesa hizi ni lazima zitumike vizuri na vile vile itumike ile sheria ya manunuzi ya mwaka 2005 ambayo inasisitiza kwamba unapotaka kununua kitu chochote ambacho kitazidi labda milioni kumi basi iwe lazima utangaze tenda. Vile vile kwa fedha ndogo ndogo basi uwe na *supporting document* ambayo itakuwa ina *quotation* ambayo zitakufanya wewe utumie fedha zile kihalali. Mhe. Spika, kifungu hicho hicho cha fedha kinasema kwamba fedha zikaguliwe ni muhimu vile vile fedha hizo kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nilikuwa na mengi lakini kutokana na wakati naona umeshaenda, kwa hivyo kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani naunga mkono mswada huu mia kwa mia. *(Makofi).*

**Mhe. Spika:** Mhe. Fatma ninakushukuru kwa mchango wako huo na kuunga mkono hoja. Nilifikiri kwamba wajumbe walikuwa karibu tumemaliza lakini nilipokuwa natoa kauli ya kwamba imeonekana tumeridhika wamejitokeza wajumbe wengine kama wanne. Kwa hivyo wakati wa jioni Mungu akitujaalia tutaanza kumsikiliza Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Amina Idd Mabrouk na atafata Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya, muda ukiwepo tutamsikiliza Mhe. Naibu Waziri wa Afya. Lakini kabla ya Naibu Waziri wa Afya atafata Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na yeye atataka kuweka mambo sawa na hatimaye kama muda utakuwepo baada ya mtiririko huo tutamwita Mhe.Waziri.

Baada ya machache hayo basi Waheshimiwa Wajumbe sasa ninaahirisha kikao hiki hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii kuweza kutoa mchango wangu kuhusiana na huu mswada ulioko mbele yetu.

Mhe. Spika, mswada ulioko mbele yetu ni muhimu sana sio tu kwa mimi Mwakilishi wa Jimbo la Wawi, lakini mswada huu wote humu ndani ni wadau. Kwa sababu nadhani katika hili hakuna ambaye hajawahi kuuguzwa

na muuguzi, sidhani kwamba kwa upande wa kina mama hakuna ambaye hajawahi kukutana na mkunga ni wachache sana. Sasa mswada huu ni muhimu sana sio tu kwa wauguzi na wakunga pamoja na Serikali, lakini hata sisi wananchi kwa ujumla kwa sababu mswada huu unagusa kila mtu.

Mhe. Spika, mimi nimelazimika kutia nyalio katika mtihani kwa kuchangia kidogo kuhusu mswada huu kutokana na kuona baadhi ya mambo hayakunikalia vyema. Kwa mfano nilipoangalia hapa katika madhumuni na sababu ya kuletwa huu mswada katika ukurasa wa 51, naomba kidogo hii fasili ya mwanzo niinukuu;

> "Madhumuni na sababu ya kutungwa kwa sheria hii mpya ni kuleta pendekezo la kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga, Sheria Nam. 9 ya Mwaka 1986 ambayo imeonekana kwamba imepitiwa na wakati na kupendekezwa na kuanzishwa kwa Sheria mpya ya Wauguzi na Wakunga ambayo itaweza kusimamia vyema misingi ya taaluma na maadili ya fani hii ikiendana na mabadiliko ya nchi, kisiasa, kijamii na kiuchumi".

Mhe. Spika, nimelazimika ninukuu hii kwa sababu nadhani kwa kiasi fulani ina mapungufu, hii ibara hii kwamba neno "maslahi" hapa halikutumika, neno "maslahi" halikuingizwa tunaangalia taaluma na maadili tu ya fani hii kutokana na mabadiliko ya nchi kiuchumi, kijamii pamoja na kimaisha. Lakini maslahi ya wauguzi na wakunga mswada huu inaonekana haikuangalia vyema.

Mhe. Spika, kama kuna watu ambao Serikali iliyo makini inataka iwaangalie na kuwatupia jicho la huruma ni wauguzi na wakunga, kwa sababu katika kipindi tulichonacho hawa watumishi wa umma wanafanya kazi katika mazingira ya kubahatisha sana, katika mazingira yaku-*risk* maisha yao, wakati sasa hivi magonjwa yameongezeka, wakati hospitali zetu na vituo vyetu vya afya vikiwa na vifaa visivyotosheleza sana kama ni *passive measures* za hawa wakunga na wauguzi kuendelea kutoangalia maslahi yao, basi nadhani ni kitu cha kuwadhalilisha sana.

Mhe. Spika, sasa hivi unawakuta hawa ma-*nurses* wametofautiana; kuna hawa ma-*nurses* wanaoguza wagonjwa wa kawaida katika wodi hizi za kawaida na kuna hawa *sacoptic nurseries* ambao hawa *sacoptic nurses* kazi yao ni kuuguza, sisemi kwamba ni kutibu, lakini ni kuuguza hawa wagonjwa wa vichaa.

Mhe. Spika, sasa wewe muuguzi wa kichaa kum-*handle* kichaa ukampa tiba aliyopewa na daktari ukatoka salama ushukuru. Sasa mimi nadhani katika hili

neno maslahi lingeingizwa naomba isomeke tu kwamba hapa yangeongezwa maneno kama ifuatavyo:

"Sheria mpya ya wauguzi na wakunga ambayo itaweza kusimamia vyema maslahi, taaluma na maadili ya fani hii yanayoendana na mabadiliko ya nchi, kisiasa, kijamii na kiuchumi".

Lakini neno "maslahi" litangulie, naomba sana Serikali ione kwamba hivi sasa unaweza ukaenda wewe, unae *nurse* anamtibu mgonjwa wa maradhi fulani na yeye maradhi yale yale yakamrukia. Sasa utakutia tatizo linaloikumba Serikali yetu inaangalia katika kada ya afya sana, tunaangalia maslahi ya madaktari tu, lakini hawa ma-*nurses* ni tatizo kidogo. Kwa hivyo, naomba mswada huu vile vile nao ujali sana maslahi ya *nurses* pamoja na hasa wale wanaofanya katika mazingira hatarishi, kwa mfano hawa *sacoptic nurses.*

Mhe. Spika, nikiingia ndani sasa katika huu mswada, nakuja katika muundo wa Baraza. Tukiangalia katika muundo wa Baraza hili umeacha watu muhimu sana,yaani muundo huu umeacha watu muhimu sana. Ilikuwa hapa waingie kama wenzangu walivyopendekeza katika muundo huu, waingie wakunga wa kienyeji wale wa jadi. Vile vile, napendekeza viingie katika vipengele vyingine vitatu kwamba waingizwe hawa wakunga wa jadi wawepo ma-*specialists* wawili, angalau mmoja akiwa muuguzi na mwingine akiwa mkunga. Vile vile, kuwepo na mtaalamu katika mambo ya wanawake katika Baraza hili, awepo *gainer psychologist* mmoja aingie tena aliyebobea hapa.

Halikadhalika, kuhusu Mwenyekiti, napendekeza kwamba suala la Mwenyekiti kumuachia tu kwamba awe mtu mwenye cheo cha uandamizi katika masuala ya uuguzi na ukunga ni kutaka kumbambikiza mtu madaraka. Lakini nahisi Mwenyekiti angekuwa na sifa za kitaaluma na sio hii, pengine ingetajwa hasa kwamba Mwenyekiti wa Baraza hili awe angalau mtu mwenye *degree* ya pili katika mambo ya *nursing and midwife*. Hii ingesaidia sana kuliko kuacha tu katika mambo yakawa hivyo.

Mhe. Spika, nimelazimika kutetea sana hawa wakunga wa kienyeji kwa sababu hawa hawana taaluma na nilipokuja kuziangalia sifa za kusajiliwa huku nimeona kwamba wakunga wa kienyeji katika kifungu cha 15 hapa sifa za kuweza kusajiliwa wote hawa mswada huu ume-*regard* zaidi *academic performance* ya mtu, ndiyo aweze kusajiliwa. Hili ni tatizo.

Mhe. Spika, kwa sababu amesema hapa asubuhi bi Asha kwamba hawa wameanza kazi zamani ya kuwazalisha mama zetu hawa, yaani wameanza kazi zamani tena hawa wanafanya kazi katika kipindi kirefu sana katika nchi hii. Mimi nakumbuka katika miaka ya 1970 mwanzoni Chake Chake pale

tulikuwa na Hospitali ya Chake Chake na mji mzima tulikuwa na vituo viwili tu vya afya. Kwa hivyo, ilikuwa si rahisi mzazi kumtoa Kuungeni, Mgelema,Vitongoji na Umangani ukampeleka Chake Chake Hospitali kwa ajili ya kwenda kupata huduma.

Mhe. Spika, walikuwa wakizalishwa na wakunga hawa wa kienyeji, tena walikuwa wanawazalisha vizuri sana, walikuwa wanawazalisha vizuri huku wakiwa hawana taaluma. Wamefanya kazi miaka mingi ya kusaidia umma na wenzetu Wazungu wanasema kwamba usiache kumpongeza kwa yule anayefanya vizuri, yaani anayefanya kazi nzuri lazima apongezwe. Kumpongeza kwa anayefanya kazi nzuri hapa ni kuwajali hawa wakunga wa kienyeji.

Mhe. Spika, hawa wamekuwa wakifanya kazi siku nyingi tena walikuwa si kama hawa wakunga waliosomea, aah! Hawa walikuwa wakifanya kazi za kuzalisha, wewe ukiwa hu-*push* huna *cytosine*, sio kama anakufanyia *intervenes injection* au *cytosine,* lah! Wewe watakufanyia mbinu, bidii na maarifa yao bila ya kutumia pesa wala kukupiga sindano ya *cytosine*, walikuwa wakikutia ukindu tu, mimi nakumbuka kuna mama mmoja siku moja alikuwa ha-*push* akatiwa ukindu katika mdomo, ule ukindu akaingizwa kwenye mdomo hivi akafanya kukohoa kidogo, hatimae taratibu mtoto akatoka bila ya *cytosine*. Sasa hawa wanawania *seizure*,yaani hawa wa sasa wanaowafanyia *seizure,* wana ukindu tu, mwanangu unatia kwenye mdomo na anakutilia, halafu una-*push* na mtoto anatoka, hakuna *cytosine* wala *seizure*. Leo tunawadharau kiasi hiki! Namna gani?

Mimi nadhani katika hili ni vyema wakunga wa kienyeji hawa wakawemo hasa katika huu mswada na wakajaaliwa na wakaingizwa katika Baraza. Kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu nawaomba kwamba wote sisi ni wadau wa wauguzi na wakunga japo wanaume, sisi katika wakunga si wadau wao, lakini wake zetu ni wadau wao kwa vile tusifanye shida katika kuupitisha huu mswada. Mswada huu ni mzuri na ni mswada mzuri sana na wakati umesibu.

Mhe. Spika, mimi nimehudhuria katika hadhara kadhaa za ndani na nje ya nchi, hizi zinazojadili malengo ya *millennium* katika *reduction* ya *mother child mortality rate,* nimehudhuria hadhira kadhaa hapa ndani na nje ya nchi. Nimeangalia yaani wakina mama wanaojifungua katika vituo vya afya katika Tanzania, ukilinganisha na wakina mama wanaojifungulia katika vituo vya afya pale Kenya, Rwanda na Burudi, sisi tuko nyuma. Hii si kwamba tuko nyuma kwa sababu tu ya nini, lakini ilikuwa hakuna chombo kinacho-*govern* haya mambo ya *reduction of mother child mortality rate.* Sasa mimi naamini kwa sababu kuna sheria hii, naamini kwa kiasi kikubwa na sisi tuta-*mixed*

*demand* ile ya *millennium goals* za kuweza kufanya *reduction* ya *mother child mortality rate*.

Kwa hivyo, naomba musiwe wagumu katika kuupitisha huu hasa wakina mama, yaani musiwe wagumu katika kuupitisha huu kuunga mkono kwa ajili yenu na kina baba na nyinyi huu ni kwa ajili yenu. Waheshimiwa nawaombeni sana tuupitishe kwa sababu Tanzania iko nyuma sana, hatuna watu wa kutoa taaluma za kuweza kuwashawishi mama wa kutosha kuripoti katika vituo vya afya vya kuzalia kwenda kupima ujauzito kwa wakati, matokeo yake watoto wengi wanafariki na wa mama wanakuwa na matatizo mengi wakiwa katika uzazi na tunakuwa nyuma katika kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Naamini utakapopita huu mswada, basi haya mambo na sisi tutakuwa mbele, mimi nilikuwepo kwenye *EYALA* mwaka jana, nikaona haya kwamba Zanzibar sisi tuko nyuma kidogo, lakini naamini tukikubali hapa katika haya mambo, basi na sisi tutakuwa mbele na tutakuwa na *say* katika Jumuiya za Kimataifa kuona kwamba na sisi nchi yetu ina-*regard* afya za mama na watoto wetu. Tusishindwe na nchi kama hizi za huku, sisi bwana tumeendelea zaidi ukilinganisha na nchi nyingine. Kwa hivyo, tuupitisheni huu mswada kusudi tuone kwamba na sisi wa mama wanapata afya na watoto wanakuwa juu. Naunga mkono hoja juu ya mswada huu mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:** Mhe.Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia jioni hii ya leo tukiwa wazima na kuweza kutekeleza majukumu yetu kama ilivyokusidiwa. Lakini pia, nichukue fursa hii ya dhati kabisa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo ili na mimi niwe mchangiaji katika mswada huu muhimu sana kwa maslahi ya Taifa letu.

Mhe. Spika, nitakuwa sijaitendea haki kwamba ikiwa sijampongeza Mhe. Waziri, kwa namna alivyotuletea mswada huu kwa wakati muafaka, lakini pia, mswada huu ni muhimu sana kwa Taifa letu na ustawi wa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa kweli *professional* hii ya *nurse* au muuguzi ni muhimu sana kwa huduma yetu hii ya afya. Lakini pia, ukiangalia *professional* hii *nurse* na mkunga ni muhimu sana kuliko daktari. Nasema hivi kwa sababu wote ni mashahidi kwamba *nurse* au muuguzi yeye muda wote huwa anakuwa na mgonjwa kuliko daktari.

Lakini si hilo tu, daktari ukiangalia kwamba yeye kwa siku anaweza akapiga *round* mbili au tatu. Lakini *nurse* yeye ndio mara zote huwa anakaa na

mgonjwa wakati wowote, lakini pia, anajua shida za mgojwa yule. Inapotokea tu dharura yeye *nurse* ndiye anayechukua jukumu la kumpigia simu daktari au kumtafuta kumwambia kwamba kuna *emergence* wodini, kwa hiyo, daktari unahitajika.

Mhe. Spika, lakini si hilo tu ukija katika fani ya mkunga wote ni mashahidi, kina mama tunafahamu, lakini na kina baba pia tunafahamu kwamba ni dhahiri kina baba pamoja kuwa yeye sio anayezaa, lakini yeye anachukua jukumu la kumpeleka mama hospitalini. Kwa hiyo, anaona kwamba mkunga ni mtu muhimu sana sana kwa mzazi na kama hujapata huduma ya kutosha kwa mkunga, basi hata ile huduma uzazi inawezekana ikawa haiko sawa. Kwa hiyo, mimi niseme kwamba maisha yetu yote ya wagonjwa wetu wanategemea watu wawili hawa, kwa hivyo, niseme kwamba mswada huu kwa kweli ni muhimu sana na umekuja wakati unaostahiki.

Mhe. Spika, mimi niseme kwamba kina mama kwa kweli mswada huu unatugusa kwa asilimia mia moja. Lakini si hilo tu, kwa kweli sisi akina mama tuliokuwemo humu ndani, lakini hata wanaotusikiliza basi ni dhahiri kwamba kina mama tumefarajika kuletwa mswada huu. Kwa hiyo, niombe au niseme kwamba mimi binafsi na kina mama wenzangu tunaunga mkono asilimia mia moja kwa mswada huu.

Lakini si hilo tu niombe taasisi basi ambazo zinashughulika zinazohusiana na mambo haya au na vitengo hivi, basi kuhakikisha kwamba wanasaidia kwa nguvu zote kutekelezwa kwa mswada huu, kwa sababu uzoefu unaonesha kwamba miswada mingi tunaipitisha hapa miswada mizuri inatusaidia wananchi miswada kupitishwa au kutekelezwa miswada hiyo tunayoipitisha, lakini hatimae miswada mingi inakuwepo katika ma-*draw*. Kwa hiyo, niombe Mhe. Waziri, mswada huu tutakapoupitisha, basi tuufanyie kazi mara moja na uweze kutekelezeka.

Mhe. Spika, nikiingia ndani ya mswada huu nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri, nikiingia katika ukurasa wa 39 kuna kipengele cha 19 hiki kinasema kwamba ni marufuku kwa mtu au taasisi kuendesha mafunzo ya uuguzi au ukunga isipokuwa kwa idhini ya Baraza.

Mhe. Spika, tunafahamu kwamba kipindi cha nyuma kulikuwa na vyuo vingi tu ambavyo vilikuwa vinatoa mafunzo hayo ya uuguzi. Lakini si hilo tu Mhe. Spika, kuna baadhi ya vyuo vilikuwa havina viwango vya kuitwa vyuo na nasema hivyo kwa sababu ili chuo kiwe na kiwango lazima iwe na maabara, lakini pia, kuwe na vifaa ambavyo vinastahiki kusomeshea katika chuo kile. Hivi karibuni tunasikia kwamba kulikuwa na chuo kilikuwa kinasomesha

mambo haya yanayohusiana na uuguzi, lakini kwa bahati kilipofatiliwa chuo kile kilikuwa hakina sifa ya kuitwa chuo.

Lakini mimi niipongeze Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa dhati kabisa kwa kukuchukuliwa hatua chuo kile kwa kukifungia. Lakini hivi karibuni nasikia chuo kile kimefunguliwa kwa maana kwamba kimetekeleza yale masharti ambayo yanastahiki kuitwa chuo. Kwa hiyo, mimi nimuombe Mhe. Waziri, kwamba bado Baraza letu hili lina kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba inavipitia vyuo vyetu vyote hapa nchini kuona kwamba vinastahiki kuitwa vyuo, lakini pia, vinatoa yale mafunzo ambayo yanastahiki.

Mhe. Spika, mswada kwa kweli huu ni mzuri na mambo mengi yamejitosheleza, kwa hiyo, sipendi kuchukuwa muda mrefu.

Lakini niingie katika ukurasa wa 38. Tumeambia kwamba hapa ukurasa wa 38 kuna kipengele hichi cha tatu kinasema kwamba pindipo ikitokea kutokuwepo kwa lolote kati yaliyoelezwa katika kijifungu kidogo cha (a) na (b) na kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki Baraza litamfanyia mtihani muombaji na yeye atapaswa kufaulu.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi hapa nimepata mashaka kusema kwamba leseni mtu anaweza akapewa kama yuko nje ya nchi ametoka nje ya nchi. Pengine ana Shahada wanasema kwa mtu ambaye anatoka nje ya nchi atalazimika kuwasilisha ushahidi utakaoliridhisha Baraza kuwa amesajiliwa au amestahiki au anastahikia kusajiliwa kwa kuwa muunguzi au mkunga kati ya nchi yake. Kuwasilisha ushahidi kuwa amehitimu na amefaulu mafuzo ya uuguzi au ukunga. Lakini ukiangalia katika kipengele cha pili, wametuonesha kwamba mtu anatakiwa ahitimu kufaulu mafunzo ya uuguzi au ukunga.

Mhe. Spika, sasa mimi mashaka yangu yako hapa, kwamba mtu pengine ametoka nje ya nchi sasa kipengele hiki kinaweza kumfanya kwamba mtu pengine katoka nje ya nchi pengine hana cheti au hana Shahada yoyote ambayo inamuonesha kwamba yeye ana sifa za kumfanya awe mkunga au muuguzi. Lakini kwa kuwa kwetu Zanzibar kuna kipengele hiki ikawa kimbilio la watu ambao wanatoka nje na inawezekana mtu huyu anaweza kwenda akafanyishwa mitihani, lakini mitihani hiyo anaweza akafaulu sawa, lakini sasa mtu huyu hana cheti.

Kwa hiyo, mimi naona hii kidogo itawavunja moyo wale watu ambao wanasoma na wote tunafahamu mtu anajipinda kwa kutegemea jambo, lakini hatimae anaweza akaja mtu tu kuwa hana cheti, lakini mtu yule yule akawa anaweza akapewa huo usajili. Sasa mimi niombe labda Mhe. Waziri, kipengele hiki kidogo kama itawezekana basi kiondoshwe.

Mhe. Spika, lakini jengine Mhe. Waziri, ametwambia kwamba mtu akiwa ameshamaliza masomo yake basi anaweza kupewa usajili. Sasa hatuoni kwamba pamoja na kuwa mtu amemaliza masomo yake, lakini kuna mambo na vigezo vingi ambavyo mtu vinaweza vikamfanya awe Mkunga au Muuguzi, kwa mfano nidhamu ni kitu muhimu sana hasa katika sekta hii ya afya.

Lakini pia, kuna mambo mengine ni muhimu sana, sasa mimi niombe kama itawezekana basi hii usajili iwe japo mtu amepata cheti, lakini uwe kwa muda isiwe apewe tu usajili wa moja kwa moja. Sasa tutaangalia kwamba labda apewe usajili wa mwaka au miaka miwili au mitatu ili aangaliwe mtu yule. Kwa sababu kama tutakuwa tunampa tu huo usajili anaweza mtu akafanya anavyotaka.

Mhe. Spika, baada ya hayo kama nilivyotangulia kusema kwamba mswada huu ni mzuri na umeletwa wakati muafaka mimi nimuombe sana Mhe. Waziri, lakini niwaombe Wajumbe wenzangu tuupitishe mswada huu ili uweze kufanya kazi mara moja pamoja na marekebisho yake ili tuweze kuwasaidia Wazanzibari ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Spika, baada ya hapo niseme kwamba naunga mkono mia juu ya mia mswada huu nakushukuru.

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa na mimi nafasi ya kuweza kuchangia Mswada wa Sheria ya Wauguzi na Wakunga na uanzishwaji wa Baraza la usajili wa Wakunga.

Nianze kwa kuunga mkono hoja na baadae niwapongeze viongozi wapya wa Wizara ya Afya ambao wamekabidhiwa majukumu kwa sasa kazi zipo, naomba wajipange vizuri. Wizara ya Afya si nyepesi sana, lakini Mwenyezi Mungu atawasaidia na sisi tuko tutawasaidia. Lakini tujipongeze na sisi tuliondoka kwa sababu naamini kwamba tulifanya kazi vizuri.

Kwa hiyo, tumewatengenezea njia ambayo kwao ilikuwa...ili kuweza kupita.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie kuhusu Mswada huu. Kwanza ningependa kuzungumzia suala la kada za Afya. Suala la kada za Afya ziko nyingi fani tofauti, lakini nako kuna mngawanyo wa kazi...Kwa hiyo, ndiyo mgawanyo wa kazi ulivyo sio kwamba...ikiwa ni mtu wa maabara anapima ndio kazi yake ikiwa mtu wa madawa anasoma buku anatoa dawa kazi yake ndiyo hiyo.

Lakini Mkunga na Muuguzi wao wana nafasi...ni ukweli usiopingika kwamba katika kada hizo mbili hizo nasema kama ndiyo jembe la Wizara ya Afya hao

waliobakia kila mmoja kwa nafasi yake, lakini kiini cha wizara hii katika utibabu tunategemea wakunga na wauguzi. Kwa hivi sasa wakunga na wauguzi waliopo kidogo, wagonjwa na wazazi wengi, watu...kiasi ambacho wanafanyakazi kupindukia idadi ya wagonjwa ambao wanatakiwa wawatibu, lakini wanafanya kwa sababu hakuna mtu, wanatakiwa wafanyakazi. Kwa hiyo, wanafanyakazi kwa kadiri ya uwezo wao. Unapofanya kazi kama hiyo lawana hazitokosa kwamba labda...malalamiko ya hapa na pale yapo.

Lakini kama saa nyengine wanafanyishwa...isipokuwa mzigo unapokuwa mkubwa unafanya unapojaaliwa kufanya na hayo masuala ya...

Sasa mkunga anafanya kazi yake kwenye *clinic* za kina mama huko ndiko majukumu yake yaliko. Lakini mkunga muunguzi hufanyakazi popote katika *clinic* yoyote hufanyakazi ya kuzalisha, anafanyakazi ya mama na mtoto anafanya kazi ya kuwafundisha wangonjwa wenye matatizo tofauti ya upasuaji na mengine.

Kwa hiyo, mkunga muunguzi yeye yuko...Lakini Mkunga peke yake...Kwa hiyo, ningependa nimwambie yule aliyesema kwamba kwa nini hakuna mkunga peke yake kwa sababu hakuna muunguzi peke yake kuna mkunga na muuguzi...Sasa kwa utaratibu siku zote tukiwa na mgonjwa kwenye familia inafika wakati watu wanagombana,yaani ugomvi unakuwa mkubwa na katika familia mko watu wengi tu. Lakini ulalamishi hawishi wengine hununa tunakuwa hatuna hatusaidiani hata kwa wazee wetu waliotuzaa, unadiriki kumchukuwa ukenda kumpeleka hospitali na hali unajua kwamba hakuna kitakachoweza kusaidia kwa mgonjwa yule, bora abaki nyumbani, lakini anapokelewa.

Wanapokelewa na wanahudumiwa katika hali hiyo ambayo wanayo. Sasa seuze Mnazi Mmoja hospitali kwenye wodi isiyopungua watu arubaini au zaidi kuna muuguzi mkunga mmoja na *ordeal* mmoja unategemea aifanyeje kazi ile. Lakini wanafanya kwa sababu ndio hali halisi.

Kwa hiyo, tunapowasema wakunga, wauguzi katika...kama hatuwatendei haki, sisemi kwamba mabaya hawafanyi, hapana, hayo yana nafasi yake tafauti. Lakini kwa kweli iko hivyo kwamba wakunga, wauguzi...lakini yanakosekana yale mazuri.Wakati huo huo atoe dawa na usiku huo apige sindano za masaa...

Lakini ukitizama na upande wa pili wamechagua wenyewe kazi hiyo hakuna anaelazimishwa wanaomba kwenye vyuo wanasoma...

Hawana sababu ya kutukana wagonjwa na kutoa maneno yasiyokuwa na maana kwa kisinginzio chochote, yule anaefanya hivyo...sisemi hawapo, wapo wafanyakazi wa hospitali, wafanyakazi wodini na wapo nimefanya kazi kama Naibu Waziri wa Afya kama wanaweza kunambia mimi wanayoyataka, itakuwa mgonjwa na anaepita wapo.

Kwa hiyo, niseme hivi kwamba malalamiko mengine ni ya kweli bali isipokuwa tu tujirekebishe ili hii sifa mbaya iondoke tuwe na sifa inayolingana nasi. Kwa hiyo, nichukuwe nafasi hii kuwaambia wakunga na wauguzi kwamba jamani tufike pahali sasa iwe basi inatosha kusikia kila siku tunalaumiwa sisi kwa sisi na mpaka sasa Mhe...hapana isifike hali hiyo tujirekebisheni tuwe wakunga na wauguzi wazuri na Baraza lisimamie wakunga na wauguzi wake wazuri wanavyostahiki.

Lakini si hilo tu mimi nimegundua wakunga na wauguzi wana tabia nyengine mbaya ya kumsema mtu mnavyotaka, mtu yule kwenye wodi ile kuna mtu anamjua halafu salamu zinafika kwa wenyewe, sio vizuri...Sasa mimi nafikiria kwamba katika sehemu za kazi za wakunga na wauguzi wako katika makundi mawili

(*Hapa Mheshimiwa hakutumia kipaza sauti*)

**Mhe. Spika:** Tunakushukuru Mhe. Dkt. Sira, kwa mchango huo na kuunga mkono hoja. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baada ya hapo nimkaribishe Mhe. Naibu Waziri wa Afya. *(Makofi)*

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii jioni ya leo angalau na mimi nitoe mchango wangu mdogo katika mswada huu wa Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba na mimi pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia neema na afya, na leo tumekutana hapa tukiwa tayari tunatekeleza majukumu ambayo yametuleta ndani ya chombo hiki.

Pili Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa imani yake kwangu ya kuniteua kuwa Mwanasheria Mkuu wa tatu kwa kipindi chake hiki cha miaka minne. Naomba Mhe. Spika, kwa kupitia Baraza hili kumuahidi Mhe. Rais kwamba nitafanya kazi zangu kwa umakini, hekma, uadilifu, na kwa kadri ya uwezo wangu nitafanya kazi hizi bila ya woga wala upendeleo. *(Makofi)*

Tatu Mhe. Spika, naomba nikushukuru wewe na Wajumbe wako wa Baraza hili, tokea asubuhi nilipoingia humu mumenipokea vizuri na mumenikaribisha vizuri. Naomba huu uwe ni mwanzo mzuri wa kufanya shughuli zetu pamoja. Mimi si mgeni kwao, tumefanya kazi miaka mingi, na muda mwingi nilipokuwa Naibu Mwanasheria Mkuu tumefanya kazi mimi na wao vizuri. Kwa hiyo, naomba ule uhusiano wetu ambao tumeujenga uendelee katika wadhifa wangu huu mpya wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nadhani tukishafanya hivyo tutaona sasa kumbe sote lengo letu ni moja. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe kwamba tushirikiane katika kutimiza majukumu haya ambayo tumekabidhiwa. *(Makofi)*

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba sasa na mimi nitoe mchango wangu mdogo katika baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameya-*raise* tokea asubuhi ya leo.

Kwanza, nianze na mapendekezo ambayo Kamati imekuja nayo asubuhi. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Kimsingi mengi ya yale waliyopendekeza mimi nakubaliana nayo moja kwa moja. Wamefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

La pili Mhe. Spika, katika yale ambayo wamependekeza kwenye sehemu ya kwanza ya waraka wao kifungu cha 2 wanapendekeza kwamba tuongeze kifungu kipya cha 2 ambacho *marginal note* yake itasomeka "matumizi" na kifungu hicho kisomeke "Sheria hii itatumika kwa Zanzibar tu".

Natambua na ni ushauri mzuri, lakini ningependa kuwaambia Kamati kwamba ukisoma Sheria Nam. 7 ya mwaka 1984, Sheria ya Tafsiri, *Interpretation and General Provisions Act* kifungu cha 22 (1) kimeelezea kwamba sheria zote zinazotungwa na Baraza la Wawakilishi zitatumika kwa Zanzibar nzima. *(Makofi)*

Sasa kwa msingi huo nadhani hakuna haja ya kuongeza kifungu kidogo cha 2 kwa sababu tayari kuna sheria nzima ambayo inafafanua utekelezaji wa sheria ambazo zinatungwa na chombo hiki. Kwa hiyo, kwenye hili ningewaomba wanakamati kwamba tukubaliane kama hivi ilivyo ibakie hivi hivi na tuiache Sheria Nam. 7 ichukue masharti yake yatekeleze.

Lakini la pili Mhe. Spika, kwenye sehemu ya pili kifungu cha 4 (1) cha mswada wamependekeza kwenye aya ya (h) kwamba katika ile *list* ya Wajumbe, Wajumbe wawili kutoka taasisi binafsi iingizwe badala ya Wawakilishi wawili kutoka hospitali binafsi.

Mimi ningeshauri kwa sababu hospitali binafsi ina sheria yake, ina Sheria Nam. 4 ya mwaka 1994 nadhani imetoa masharti mazuri ya ku-*regulate* kazi na taratibu zinazofanywa na hizi hospitali binafsi. Na ndiyo maana katika Wajumbe ambao wamependekezwa kuingia kwenye Baraza hili wakawa ni Wajumbe kutoka katika hospitali binafsi, kwa sababu ni rahisi kuuona ule utaratibu wao kisheria ulivyoeleza. Tofauti na hii ambayo Waheshimiwa wameshauri kama tuitoe hii na tuweke badala yake Wawakilishi wawili kutoka taasisi binafsi za afya.

Sasa mimi ningewaomba kwa sababu kuna sheria ambayo ina-*govern* utaratibu mzima wa *private hospitals,* ni vyema tungeacha hii ambayo Wizara imeshauri, kuwa hawa watu wawili watoke kule.
\
Jengine Mhe. Spika, ni kwenye kifungu cha 4 (5)(a). Kamati inapendekeza kwamba mtu hatokuwa na sifa za kuwa Mjumbe ikiwa..." Mimi nakubaliana nayo na yale mapendekezo ambayo wameyatoa, lakini ningeshauri ile (a) na (b) ibaki, lakini ukiisoma ile (c) Mhe. Spika, kwamba hakubaliki na masharti ya sheria hii kutoa huduma za uuguzi au ukunga. Ukitizama ile *list* ambayo imewekwa ya Wajumbe, kuna baadhi ya Wajumbe hawatokuwa na sifa za kutoa huduma za ukunga na uuguzi. Kwa hivyo, mimi ningependekeza kama kifungu hichi cha 4 (5), kifungu cha (a) na (b) kibaki lakini hichi kitu kifutwe kwa sababu ya masharti yake yatakuwa ni magumu kutekelezeka, kwa sababu ya baadhi ya Wajumbe ambao wametajwa humu hawatokuwa na sifa hizi ambazo zimetajwa na sheria za kuwa na sifa za kuwa wauguzi na wakunga.

Mhe. Spika, ambalo Wajumbe wengi wamelizungumzia tokea asubuhi ni kwenye kifungu cha 6. Kamati za Baraza kifungu cha 6 (1) na (2) mpaka kifungu cha 6 (7). Ni kweli ukisoma hivi Mhe. Spika, utaona kwamba kifungu cha 6 (1) na kifungu cha 6 (4) na kifungu cha 7 (1) vyote vinazungumzia jambo moja, lakini ukisoma vizuri kama kifungu cha 6 (1) kinaelezea kuwa na idadi ya kamati. Ukisoma kifungu cha 6(4) kinaelezea kuanzishwa kwa kamati, na ukisoma kifungu cha 7 (1) kinazungumzia kukasimu madaraka. Sasa inabidi usome hivi vizuri ndio uweze kutambua madhumuni ambayo yamekusudiwa. Mimi ningeshauri kwa sababu Wajumbe wengi wame-*raise concern* ya vifungu hivi basi tukivifanyia marekebisho kifungu cha 6 (1) ili tuweze kukifuta kifungu cha 6 (4).

Sasa kifungu cha 6 (1) kisomeke, "Baraza linaweza kuanzisha kamati nyengine kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake kadri itakapoona inafaa", ili sasa kifungu cha (4) tuweze kukifuta. Mhe. Spika, lakini hapo hapo ukisoma kifungu cha 6 (2) ningeshauri pia ukisoma hichi kifungu kinaelezea kuwepo kwa hizi kamati ambazo zimetajwa na sheria, nazo ni kamati nne; Kamati ya Fedha, Kamati ya Elimu na Taaluma, Kamati ya Miiko na

Nidhamu, na Kamati ya Sera, Mipango na Utafiti. Lakini ukikisoma kifungu chenyewe hakielezei kama hizi kamati ambazo tayari zimeundwa na sheria hii. Kifungu kinasema, "Bila ya kuathiri madhumuni ya kifungu kidogo cha kifungu hiki Baraza linaweza kuanzisha kamati zifuatazo.

Nadhani tu kwa uandishi mzuri ni bora tungesema, "Baraza litakuwa na kamati zifuatazo", ambazo ni hizi tayari zimetajwa na sheria lakini wakati huo huo kifungu cha 6 (1) kimetoa fursa kwa kamati kwa Baraza kuanzisha kamati nyengine mbali ya hizi nne ambazo tayari zimeshatajwa. Sasa huu ni uwezo ambao Baraza limepewa la kuanzisha kamati nyengine, mbali ya nne hizi ambazo zimetajwa kutokana na mazingira ya kazi ambazo watakuwa wanazifanya.

Mhe. Spika, jengine ambalo kamati walipendekeza ni kwenye kifungu cha 7 (3) (b), wanapendekeza kama kifungu hichi kuongezwa maneno, "Uwezo wa kuthibitisha bajeti ya nyongeza", *(supplementary budget)*. Sasa ukikisoma hivi hivi utaona kama kwamba ule uwezo wa kuthibitisha bajeti umeondoshwa. Sasa mimi ningeshauri kama tuongeze kwenye kifungu hichi uwezo wa kuthibitisha bajeti na bajeti ya nyongeza ili hii kamati sasa iweze kufanya kazi zote mbili. Kwanza isikasimu madaraka yake ya kuthibitisha bajeti yenyewe, lakini pia isikasimu madaraka yake ya kuthibitisha *supplementary budget* ambayo inaweza kuja wakati wa utekelezaji wa bajeti hiyo ambayo imekubaliwa. Kwa hivyo kwenye haya ambayo mengine Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wameshauri, nakubaliana nayo Mhe. Spika, moja kwa moja.

Mhe. Spika, jengine ni kwenye hoja ambazo Waheshimiwa Wajumbe nao pia wame-*raise*. Moja ya *concern* kubwa ambayo imezungumzwa leo tokea asubuhi ni hii ya uwakala wa Serikali na kwa nini tunakuwa na uwakala, kwa nini Baraza lisiwe *Board of Directors*. Wajumbe wengi wameonesha hisia zao kwenye kifungu hichi.

Mhe. Spika, wakala wa Serikali umeelezwa kwenye kifungu cha 55 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma. Ukisoma Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya 2011, kifungu cha 55 (1) utaona imeelezewa uanzishwaji wa uwakala wa Serikali. Natambua kwa muda mrefu Mhe. Spika, ilikuwa hakuna utaratibu wa uanzishwaji wa uwakala wa Serikali, tofauti na unapoanzisha mashirika ya Serikali.

Ukisoma Sheria Nam. 4 ya 2002 imeweka utaratibu mzima wa kuanzisha mashirika ya umma ya Serikali. Kwa hivyo unakuwa hupati tabu unapoanzisha shirika lolote la Serikali, kwa sababu masharti ambayo yamewekwa kwenye Sheria Nam. 4 ya 2002 inabidi uyafuate kama yalivyo.

Sasa kwenye uwakala kumekuwa na matatizo kidogo na ndiyo maana baadhi ya Wajumbe wameshauri kwa nini isiitwe *Board of Directors.* Wengine wanasema Wajumbe hawa ni wengi, ni kwa sababu hiyo, hakuna muongozo ambao umewekwa kisheria kama ambavyo umewekwa kwenye Sheria Nam. 4 ya 2002. Ile imeeleza wazi Wajumbe watakuwa wangapi, kazi za bodi ni nini, *PO* kazi yake ni nini.

Mhe. Spika, sasa kwenye uwakala tumekuwa tunapata tabu kwa sababu ya hiyo, lakini kwa sababu Sheria ya Utumishi wa Umma imeshaeleza hivyo, nadhani imetoa mwanya mzuri. Na sifa za wakala ni kwamba hazifanyi biashara, hiyo ni sifa yake; inatoa huduma, na ndiyo maana inapata ruzuku kutoka serikalini.

Mhe. Spika, Mhe. Salma Mohamed aliuliza nini faida ya kuwa na wakala. Moja ya faida yake ni hiyo Mhe. Spika, kama unapokuwa wakala na kama Mswada huu ambavyo unapendekeza ni kwamba wewe unapatiwa ruzuku kutoka Serikalini, huna haja ya kufanya biashara ili uweze kujiendesha kama ambavyo yanatakiwa yafanye mashirika mengine ya Serikali. Lakini pia kwa sababu wakala ana haki ya kushitaki na kushitakiwa, inapofika hali hiyo inabidi zile taratibu zilizowekwa na sheria ya mashitaka ya Serikali *(Government Proceedings Act)* inabidi pia yafuatwe, kama kutoa *notice* ya siku 60. Lakini kubwa zaidi mawakala hawa wanapata kusimamiwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, *free of charge*. Tofauti na mashirika haya ya Serikali ambayo mara nyingi imekuwa tunawatoza ada ndogo ya kuwasaidia kufanya kazi zao. Sasa kimsingi hiyo ndio faida ya kuwa na uwakala wa Serikali.

Jengine ambalo Mhe. Abdalla aliniuliza ni *appointing authority* ya Mwenyekiti. Nadhani hii ni *error* ambayo tumeiona na *of course* sheria nyingi tunazotunga Mwenyekiti mara nyingi huteuliwa na Mhe. Rais. Kwa hivyo, nadhani hili tutalifanyia marekebisho.

Mhe. Spika, jengine ni Mhe. Hija Hassan Hija aliuliza tuongeze Kamati ya Maslahi ya Wauguzi kwenye zile kamati nne ambazo zimetajwa na sheria. Mimi ningeshauri kwa sababu kamati hizi zimewekewa kazi zake kwenye jadweli nambari tatu, ningeshauri kama kwenye Kamati ya Fedha tuongeze kazi moja ya kusimamia maslahi ya wauguzi na wakunga ili tufute ile ya kusimamia utekelezaji wa sera, kwa sababu kuna kamati nzima inayoelezea ya usimamizi wa sera. Sasa ningeshauri Mhe. Hija ameshauri jambo la msingi, lakini badala ya kuanzisha kamati mpya nyengine ni vyema kazi hii ikapewa Kamati ya Fedha na kazi moja ambayo itatakiwa ifanye ni hii kuzingatia maslahi ya wauguzi na wakunga.

Mhe. Spika, jengine ambalo wengi wa Wajumbe wameliuliza, nadhani la Mhe. Mahmoud nimelijibu la kwa nini tusiite hii *Board of Directors* ni kwa sababu hiyo, ni kwa sababu kuna sheria nzima ya kuanzisha Mashirika ya Serikali na ambayo ndani yake imeweka sasa zile Bodi zinazoanzishwa ziitwe *Board of Directors.* Kwa hivyo, hii kwenye uwakala kama nilivyosema hapo awali hatuna sheria ambayo inaongozwa, ndiyo maana tumekuwa mara nyingi tunaziita Mabaraza na mambo mengine. Lakini hii ni *tradition* kwa Wizara ya Afya. Ukitizama sheria nyingi za Wizara ya Afya; Sheria ya Madaktari, kuna Bodi, kuna Baraza, Sheria ya Chuo cha Afya, kuna Baraza labda wenyewe Wizara ya Afya wana sababu zao za msingi, lakini ni *tradition* katika sheria nyingi tunazotunga za Wizara ya Afya kuwa na Mabaraza haya.

Mhe. Spika, nadhani mengi yale ambayo yameulizwa nimeyatolea ufafanuzi. Naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Mwanasheria Mkuu tunakushukuru. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Naibu Waziri wa Afya na baada ya hapo tumwite Mhe. Waziri kukamilisha kazi. Mhe. Naibu Waziri wa Afya karibu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mchango wangu mimi utakuwa mdogo sana, kwa sababu namshukuru sana na naendelea kumpongeza Mwanasheria Mkuu na naendelea kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uteuzi kama huu uliofanyika, maana amemaliza takriban kila kitu, kiufundi kabisa amepitia kila kipengele ambacho kinahusu sheria ya Mswada huu. Kwa hivyo mimi mchango wangu utakuwa *general* zaidi kwenye mswada huu.

Mhe. Spika, juzi nilibahatika kutembelea Chuo cha Afya pale Mbweni, ilikuwa siku ya Jumapili, ndicho kinachotoa taaluma hii ya uuguzi na ukunga kwa hapa Zanzibar, ni Mbweni peke yao kwa *level* hiyo iliyokuwepo. Sasa wakati natembelea juzi walikuwa na maonesho yao mazuri. Kila kada au kila masomo yanayotolewa pale basi walikuwa wamefanya maonesho yao, na katika yale maonesho wakawa wanafanya ushindani, nani zaidi kuliko mwenzake. Kwa hivyo toka wanafamasia, kukawa na uuguzi, kukawa na wakunga na kukawa na fani zile nyengine za madawa haya asilia pia yalikuwepo pale.

Sehemu moja ambayo ilinivutia sana ni ile sehemu ya *emergency autronomy*, mgonjwa anapofika hospitali na anavyopokelewa na akabebwa watu wakaenda mbio, wakamuwekea zile za kuvutia pumzi pamoja na kupiga moyo na kadhalika. Sasa mimi nikawauliza mbona hapa nahisi munafanya vizuri kuliko kule hospitali, kwa sababu mimi sioni kule hospitali watu kuja

mabio kuja kumpokea mgonjwa kwenye *emergency*. Wakaniambia kwamba kinachokosekana katika mafunzo tunapata yote lakini kinachokosekana wakati mwengine ni zile sheria za udhibiti, na hii inafanyika zaidi kwa hizi *Council*, yaani Mabaraza ya Udhibiti, ndiyo maana kuna masuala ya maadili na taaluma.

Sasa wakati tunapitia sheria hii, mimi nikajaribu kuangalia pia sheria ya Uingereza, inaitwa *British Nursing Council* na wao hivyo hivyo wamejikita zaidi katika taaluma na maadili. Ila *British Nursing Association,* yaani jumuiya za wafanyakazi wao ndiyo wanaangalia maslahi. Mhe. Nassor alilitaja suala la maslahi zaidi. Sasa lile linaangaliwa zaidi na zile *associations* yaani jumuiya zao au vyama vyao vya wafanyakazi, na ndiyo maana katika sheria hii Mhe. Spika, utakuta katika kifungu cha 4 (1) (e) ukurasa wa 33, kuna mwakilishi mmoja kutoka Jumuiya ya Wauguzi Zanzibar kwa sababu jumuiya hiyo inawakilishwa na mtu wake humu ndani, na kuna mwakilishi mmoja kutoka Jumuiya ya Wakunga. Hili la mwanzo lilirekebishwa na Kamati ya Ustawi wa Jamii. Sasa hili limerekebishwa, kwa hivyo mwakilishi mmoja anatoka kwenye Jumuiya ya Wauguzi na mwakilishi mmoja anatoka Jumuiya ya Wakunga.

Mhe. Spika, wao katika jumuiya zile Mhe. Nassor, wao ndio wanashughulikia zaidi masuala ya maslahi ya wafanyakazi, lakini *otherwise* mambo ya maadili na taaluma yanaendelea kushughulikiwa na Baraza. Nashukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu ameelezea hawa wakunga wa kienyeji na uzoefu na wao kuwa katika sheria nyengine na hili Baraza zaidi linaangalia taaluma. Kwa sababu wale wanakwenda zaidi kwa uzoefu na kazi, wengine wamerithi, hata wale akina Saleh Madawa Mwenyezi Mungu awarehemu wengine, wao ni kazi ya kurithi anaambiwa inafanywa hivi, hawajapata bado *scientific approval*. Kwa hivyo wao wanaingia kwenye ile sheria Nam. 8 ya 2008.

Mhe. Spika, Baraza hili ni la taaluma zaidi na ni Baraza ambalo linatoa leseni. Sasa wakati tena tunapitia sheria hii, tukaangalia wenzetu Tanzania Bara wanafanyaje, wao pia wana *Tanzania Nursing and Midwifery Council* na wao wanatoa leseni kama hii ambayo ni kama *driving license*. Kwa hivyo *nurse* yeyote anayefanya kazi ndani ya Tanzania Bara anatakiwa kuwa na kitambulisho kama hichi. Kama hana kitambulisho kama hichi haruhusiwi kugusa mgonjwa, na ni miongoni mwa fani chache ambazo mtu huapishwa. Ninavyofahamu mimi daktari anaapishwa kwa sababu anagusa maisha ya mtu moja kwa moja, muuguzi ama *nurse* au *midwife* anaapishwa na wa tatu ni wakili anaapishwa. Kwa sababu hawa wanagusa maisha ya mtu moja kwa moja na wanaweza kuleta taathira katika maisha ya mtu.

Mhe. Spika, kwa wenzetu Bara tayari wameshatunga sheria hii ipo na hii imeandikwa ni leseni ya *nurse* kufanya kazi na mfano wake upo hapa. Mhe. Spika, lakini nikiendelea kuna mchango ambao umetolewa juu ya...***nursing***. Sasa katika sheria za wenzetu hawa ma-*nurses* ama wauguzi wanakuwa na kila *class,* na katika kila *class* kunakuwa na maslahi yao. Nitasoma hichi cha Tanzania Bara *Nursing and Midwifery Council* ya Bara inasema hivi, kuna *part one nurse* imeandikwa humu kwenye leseni nyuma, kuna *part two midwife*, kuna *part three public health nurse*, yule anayeshughulika na jamii, *part four ophthalmic nurse*, *nurse* wa macho, mambo ya macho tu, *part five pediatric nurse*, *nurse* wa watoto, *part six psyachiatric nusre* ndio anayeshughulika na wagonjwa wenye vichwa, na ni kweli ni kazi kidogo ya hatari.

Lakini hapo hapo inaendelea upande wa pili inasema kuna *part seven nurse tutors*, hawa ni walimu wa wauguzi, *midwife tutors,* walimu wa ukunga, *operating theatre nurse* naye ana *class* yake maalum kwamba yeye anafanya kazi kwenye *theatre* tu au chumba cha *operation*. *Part ten all advance nursing practitioners,* hawa ni wale waliobobea wenye taaluma na miaka ya uzoefu, *part eleven for other nurses and midwives not covered by the othrodox pass*. Kwa hivyo, haya yameandikwa.

Mhe. Spika, lakini katika sheria hii utagundua kwamba kuna maneno mengine ya Kiingereza yalichapishwa kwa bahati mbaya hayakuondoshwa. Naomba maneno yale yote yaondoshwe kwa sababu tayari zile sheria ama sheria imelishatafsiri maneno yale ambayo yalikuwa yameandikwa.

Mhe. Spika, kuna fani nyingi ambazo zinamlazimisha mtu apate kibali ama leseni ya kufanyia kazi. Fani ya ndege lazima upate kibali, fani ya kuendesha gari lazima upate kibali, mtu yeyote anayeendesha gari ni lazima awe na leseni. Sasa na fani hii ya hawa wakunga na *nurse*, pamoja na madaktari wana bodi yao ambayo inatoa leseni kwa madaktari ama Baraza lao ambalo linatoa leseni kwa madaktari na hapa pia nayo yanatakiwa haya yafanyike.

Pia, Mhe. Spika, kuna suala la mitihani lilikuja umuhimu wa hawa watu kufanyiwa mitihani. Sasa sheria imeweka wazi katika kifungu cha 36, sehemu ya makosa na adhabu, kufanya kazi kinyume cha sheria, taarifa au waraka wa uongo, uanzishwaji wa utoaji mafunzo ya uuguzi na ukunga pamoja na kujinasibisha na kutenda kinyume na uhalisia. Kwa hivyo, haya yote katika vifungu hivi, naamini Waheshimiwa Wawakilishi wengine watakuwa labda vifungu hivi vya huku sehemu za mbele hawajafikia. Lakini haya yote yaliyokuwa yamezungumziwa upande wa vibali na taaluma ya kufanyia kazi, basi nayo yameingizwa humu pamoja na adhabu ama hukumu ambazo zitakazotolewa kwa mapungufu hayo yaliyotokea.

Halafu Mhe. Spika, ilizungumzwa kidogo kwamba hii miaka 15 kwa huyu Mwenyekiti, uzoefu labda inawezekana kuna mtu katayarishiwa hii nafasi. Naomba niseme kwamba kinachoangaliwa zaidi ni *qualification*, lakini *qualification* ama vyeti vyake vinaendana na miaka yake ambayo amefanyakazi. Sasa katika *nurse profession* miaka 15 sio mingi, ila kama Baraza litafikiria vyenginevyo, lakini kwa kweli tumekaa sana tumejadiliana na wataalamu mabingwa ambao wako kwenye *nurse profession* na sisi tumeona kwamba miaka 15 sio mingi hata kidogo.

Mhe. Spika, tumeangalia sheria za *International Council of Nurses* ambayo Makao Makuu yake yako Geneva nchini Swissland, nao pia wanatumia uzoefu kama huo wa miaka hiyo. Kwa hivyo, hapo hakuna tatizo. Ila kama ilivyokuwa kadi kama hizi leseni na vitu vyengine vyote vina gharama zake, kwa hivyo itabidi lazima *nurse* ama mkunga lazim alipie, kwa sababu njia moja ya kipato ya Baraza hili ni kulipia kwa leseni hii. Kwa hivyo, hilo haliwezi kuepukika na kiasi gani kitalipwa hicho kitapangwa na Kanuni wakati Baraza hili litapitisha na Baraza lako tukufu Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi. Basi wao katika kujipangia zile Kanuni ndio watajipangia kwamba wata-*charge* kiasi gani.

Hospitali ya *private* ama ya *public sector*, ikiwa ya binafsi au ikiwa ya serikali inaweza kuamua kuwalipia ma-*nurse* wake wote watakaowaajiri, inaweza kuamua hivyo. Lakini la si hivyo kama *nurse* mwenyewe atataka ku-*practise* kimaadili na kitaaluma basi itabidi ajilipie yeye mwenyewe.

Mhe. Spika, naona mimi nimalizie hapa, mengine yote yameshaelezwa, mengi yamezungumzwa. Kuna machache ya mwisho ambayo wauguzi huwa wanapata kutokana na Baraza hili. Kwanza faida kubwa moja ni kudumisha ile nidhamu kama nilivyotoa mfano awali, kwamba kwenye masomo faida ile inaonekana zaidi, lakini wanapofika hospitali linakuwa halifanyiki lile kwa sababu hakuna chombo chenye kudhibiti ama mamlaka yenye kudhibiti umuhimu au uhalisia ule wa haraka na vitu vya namna hiyo.

Kwa hivyo, sheria hii ikishatungwa ikishapitishwa na Baraza lako tukufu la Wawakilishi Mhe. Spika, basi nidhamu itaongezeka miongoni mwa ma-*nurse*, taaluma zao zitatumika kwa ubora uliokuwa wa hali ya juu zaidi. Pia, mwananchi ataweza kulindwa kwa sababu atakuwa na sehemu ya kwenda kulalamika, lakini wakati huo huo kutakuwa na *council* ambayo itaangalia malalamiko pamoja na kumtazama yule muhusika ambaye ni yule aliyepewa leseni muuguzi ama mkunga.

Pia, kutakuwa na aina fulani ya kumdhibiti muuguzi, mkunga pamoja na ile *industry* nzima ya afya. Mwisho kabisa taaluma hii Mhe. Spika, itaweza kulindwa, itakuwa haiwezi kuchezewa kwa sababu ni taaluma kubwa, ni taaluma kama zile ambazo nyinyi mnazo za kisheria kama mnavyoapa vile, basi na wenye taaluma hizi wanaapa, kwa hivyo na taaluma hii pia itaweza kulindwa.

Mhe. Spika, kwa hayo, machache, mimi naomba tena kuunga mkono sheria hii au mswada huu wa sheria kwa asilimia moja na naomba sana Wajumbe wote waiunge mkono, kwa sababu Baraza la Wauguzi na Wakunga halitowasaidia wauguzi na wakunga tu, lakini litawasaidia majimbo ya Waheshimiwa Wajumbe wote waliokuwepo hapa. Kila pahala patakapokuwa na kasoro au malalamiko, upande wa uuguzi, kwa sababu muuguzi ndiye anayekaa na mgonjwa kwa muda mrefu zaidi kuliko daktari. Daktari anapiga *round* mbili, moja asubuhi moja jioni, dakika tano asubuhi dakika tano jioni dakika kumi. Lakini muda mrefu mgonjwa anakaa na *nurse* ama muuguzi, muda mrefu mzazi anakaa na mkunga ambaye ndiye anayemuhudumia pale mpaka anapotoka baada ya kipindi chake cha uzazi, ikiwa siku mbili, tatu, nne au tano inategemea na vile alivyojaaliwa na Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe waiunge mkono na mimi naiunga mkono asilimia mia kwa mia na nina amini meza yako imeshapokea marekebisho ambayo yamewasilishwa na Kamati, pamoja na marekebisho yote madogo madogo mengine, pamoja na hilo alilosema Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba kile kipengele cha pili kilichoongezwa cha Zanzibar kile kimeingia kwenye sheria mama, kwa hivyo hakina haja ya kuwemo katika sheria hii. Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Sasa ni wakati muafaka wa kumkaribisha Mhe. Waziri wa Afya.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, kwa mara nyengine leo napenda nichukuwe fursa hii kumshukuru Alla, kwa kutupa uhai, uzima na tawfiq ya kuwepo hapa pia kwa kupata nafasi hii ya kufanya majumuisho ya mswada wetu huu wa kurekebisha sheria ya Baraza la Wauguzi na Wakunga ya mwaka 1986, na kuanzisha Sheria mpya ya Wauguzi na Wakunga ya mwaka huu wa 2014.

Mhe. Spika, kwanza naomba nichukuwe fursa hii kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Mgeni Hassan Juma, kwa kuwasilisha hotuba yake na kwa niaba ya Kamati yake. Nawashukuru vile vile Wajumbe wote

ambao wamo kwenye Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Kwanza, kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupa wakati wa kujadili mswada huu katika ngazi ya Kamati. Lakini pili, namna ambavyo aliwasilisha marekebisho mbali mbali ambayo walipendekeza.

Vile vile, napenda nichukuwe fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote ambao walichangia kama ifuatavyo:

Mhe. Salma Mohammed Ali
Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Abdalla Juma Abdalla
Mhe. Ali Salum Haji
Mhe. Wanu Hafidh Ameir
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Abdalla Mohammed Ali
Mhe. Asha Bakari Makame
Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
Mhe. Hamad Masoud Hamad
Mhe. Fatma Mbarouk Said
Mhe. Saleh Nassor Juma
Mhe. Amina Iddi Mabrouk
Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili
Mhe. Mwanasheria Mkuu
Mhe. Naibu Waziri wa Afya

Mhe. Spika, kama sio hawa kwa kuchangia kwao mswada wetu ungekuwa hauko. Kwa hivyo, natoa shukrani zangu za dhati kwa kuweza kutupa yote ambayo waliotuchangia.

La tatu Mhe. Spika, napenda nitowe shukrani nyengine zaidi kwa Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya kwa kutupa uzoefu wake, wakati yeye ndiye Naibu Waziri aliyeondoka na kutilia mkazo mswada huu ili wajumbe waupitishe.

Lakini pongezi zaidi kubwa zinakwenda kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu Mhe. Said Hassan Said. Kwa kweli Mhe. Mwanasheria Mkuu kazi yetu sisi ameimaliza, kwa sababu kazi kubwa ambayo ilikuwa katika mswada huu, ni baadhi ya vifungu ambavyo vilitajwa na wajumbe mbali mbali na ninamshukuru sana, karibu vifungu vyote ambavyo vilitajwa amevipitia, ametoa ufafanuzi na ametoa fatwa. Kwa niaba ya Wizara ya Afya tunaunga mkono mawazo yake, mapendekezo yake na maamuzi yake. Kwa hivyo,

tunaomba kwamba baada ya hapa bila shaka inakwenda kwenye ofisi yake ili iweze kumaliziwa.

Mwisho kabla sijaendelea na baadhi ya mambo, naomba nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa mchango wake ambao alioutoa, na kwa kutumia uzoefu wa kimazingira na nje kuweza kutoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba Mwanasheria Mkuu ametumalizia, mimi nina mchango mdogo tu wa kutoa ufafanuzi. Kwanza ningependa niwataarifu Waheshimiwa Wajumbe kwamba Baraza hili lina mfumo wa chombo au taasisi ya kuweka viwango, yaani *Regulatory Board*.

Kwa hivyo, ndiyo maana ukaona kwamba zaidi maslahi ya wafanyakazi wale waliotajwa hayakuzungumzwa, sio kwamba hayapo, lakini ndiyo utaratibu wa chombo na kwa bahati nzuri mitandao inawasaidia, Naibu Waziri amekuja kutueleza uzoefu wa bodi ya Uingereza hapa na mimi nilikuwa tayari nimeshataja kisentensi tu bila ya kuwa na lile jambo la kushika moja kwa moja. Ni kwa sababu gani hiyo.

Kwa hivyo, wale waliozungumza kuhusu maslahi ya wafanyakazi sio kwamba vyombo hivi havishughulikii, lakini tulisema katika madhumuni ya waraka huu, mwanzo tulipouleta mswada huu kwamba chombo hiki au Baraza hili litawakusanya wale wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Sasa maana yake ni kwamba madhumuni yake ni kusawazisha mfumo wa utendaji kazi katika Sekta ya Umma na katika Sekta Binafsi. Sasa kwa maslahi Sekta ya Umma inashughulikiwa na mfumo wa mishahara na marupurupu na mafao inaitwa *scheme of service* katika taratibu za utumishi serikalini na huku watu binafsi wana taratibu zao vile vile za utumishi wao. Kwa hivyo, hiki chombo zaidi kimejikita katika kutoa na kusimamia viwango vya utendaji kazi, kama maadili na miiko ya utendaji kazi wa hawa ambao wanashughulikiwa.

Waheshimiwa Wajumbe, wengi walizungumzia kuhusu muundo, tunawashukuru sana kwa michango yao ya kurekebisha muundo na mchango ambao ametoa Mhe. Mwanasheria Mkuu, kuhusiana na muudo ambao ulipendekezwa vile vile uteuzi wa Mwenyekiti ufanywe na Mheshimiwa Rais na sisi wizara tunakubaliana nalo moja kwa moja. Kwa hivyo, tunakubaliana na mawazo yanayotolewa.

Lakini muundo vile vile unatoa nafasi ya wakaguzi. Waheshimiwa Wajumbe wale waliochangia kwamba wakaguzi wawe na elimu kubwa na wawapite wale ambao wanaowakagua. Kuna aina nyingi za ukaguzi katika kazi kama hizi za uzoefu. Kuna wale watakaokwenda kukagua taaluma aliyonayo, lakini kuna wale watakaokwenda kukagua ule utendaji wake wa kazi tu bila ya

kujali taaluma aliyonayo, kwa sababu muuguzi anatakiwa afanye mambo kadhaa wa kadhaa wakati wa kazi yake, bila ya kujali cheti alichonacho, bila ya kujali ukubwa wa elimu aliyonayo, je, ule utaratibu wa kazi aliotarajiwa kufanya anafanya. Hii inawezekana zaidi kufanywa na watu ambao wamebobea katika ile kazi, yaani wana uzoefu mkubwa.

Kwa hivyo, inawezekana kukawa na kaguzi zaidi ya aina moja, wale ambao wanakagua taaluma na wale ambao wanakagua ule ufanyaji kazi wa wale ma-*nurse*. Ndiyo maana wakaguzi wakaachiwa wawe huru na iwe *free* katika kutaja mambo yao, kwa sababu Baraza linaweza likajua kwamba fulani na fulani tunaweza tukamtumilia kwa ajili ya ukaguzi wa namna ma- *nurse* wanavyofanyakazi yao au wakunga wanavyofanyakazi zao na kuna wengine wanawakagua kutokana na taaluma yao waliyonayo je, wanaitumia au hawaitumii. Kwa hivyo, yote mawili yanawezekana.

Mhe. Spika, tunakubaliana na Waheshimiwa Wawakilishi karibu wote au wote waliozungumza, kwamba kilicho muhimu kwa ma-*nurse* na wakunga ni utumizi wa lugha nzuri na utaratibu mzuri wa kufanyakazi. Ndiyo maana ikawa hiki chombo kikaitwa chombo cha utaratibu wa kuweka viwango, yaani *Regulatory Board*. Kwa sababu imewekwa na adhabu, kumewekwa na utararibu wa kuwazuilia au kutokuwapa usajili au kutokuwapa leseni zao, yote haya yanalinda ile hadhi ya kazi ambayo wanaifanya.

Lakini jambo kubwa zaidi Mhe. Spika, ni kwamba baada ya mwaka 1999 kama ambavyo tulieleza, kulipatikana hospitali za binafsi. Sasa inawezekana mfanyakazi akawa amejisajili Zanzibar, lakini kwa sababu amejisajili katika hospitali ya serikali, akawa anaweza kufanyakazi kwa mujibu anavyotaka yeye tu, maneno anavyoona yeye tu kwa madhumuni kwamba labda anaweza akapata kazi katika hospitali za binafsi. Lakini katika utaratibu huu, akishazuiliwa leseni yake kutokana na utaratibu mbovu wa kazi yake au lugha ambazo anatumia sio nzuri, itakuwa ni vigumu kwake kupata kazi ndani ya Zanzibar hata katika hospitali za binafsi.

Kwa hivyo, yote hayo ni katika kuona kwamba wafanyakazi wanaofanyakazi katika hospitali za umma au hospitali binafsi wanakuwa na utaratibu wa kufanyakazi katika njia ambazo zinakubalika.

Mhe. Spika, kuna ambao walichangia kwamba labda hiki chombo hakina watu wa *profession* nyengine kama madaktari au wengineo. Lakini sasa hiki chombo ni maalum cha ma- *nurse* na wauguzi. Kwa hivyo, wanaotakiwa wakiendeshe ni wao, kwa sababu kuna vyombo vyengine vinakusanya vile vile madaktari ndani ya hii hii Wizara ya Afya. Kwa hivyo, kwa sababu

madaktari wana chombo chao, sio vizuri kuwachanganya tena na wengine katika *profession* hiyo, kila mmoja na fani yake.

Suala la wakunga wa jadi limeshazungumzwa kwamba liko katika Sheria ya Tiba Asili hata Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya tunamshukuru sana alitusaidia kwamba wao wanathaminiwa sana, yaani juhudi yao pamoja na kazi yao inathaminiwa, lakini kila mtu na pahala pake. Kwa hivyo, wao Wakunga wa Jadi wamewekwa *special* katika Sheria ya Tiba Asili, kwa hiyo sio kama wamedharauliwa au wameondolewa, lakini huku kwa sababu kunatizamwa ile taaluma basi sio rahisi kuwaingiza moja kwa moja katika mfumo wa Baraza hili la Wauguzi na Wakunga.

Vile vile, tunapokea pongezi zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali, ni imani yetu kwamba na Mhe. Spika nilitangulia kusema kwamba sisi tumekwenda pale kazi kubwa sana imeshafanywa. Kwa hivyo, ni matumaini yetu kwamba Waheshimiwa Wawakilishi nao watatupa ushirikiano wao, ili tuweze kuliendeleza hili jahazi ambalo tumelikuta tayari limeshajaa upepo linasafiri.

Tukichukua mchango mmoja ambayo ni *special* wa Mhe. Hija Hassan Hija, tunamuomba hapa akubali kwamba vifungu vile (g), (q) na (r) vibaki vile vile kwa sababu vinazungumza mambo tofauti ambayo yametajwa haidhuru yana uhusiano, lakini kwa kuwa ni mambo tofauti basi vibakie, ili kile kimoja kinapobaki kinakuwa na uzito wa aina yake katika shughuli ile.

Mhe. Spika, kwa haya machache kwa sababu kama nilivyosema siwezi kurudia maneno ambayo tayari nimekwishayasema, vipengele au vifungu vingi karibu vyote vilivyotajwa vimezungumzwa na Mhe. Mwanasheria Mkuu, ambapo sisi tunaunga mkono mapendekezo pamoja na majumuisho aliyotoa na pia tunakubalaina na hoja yake, kwamba marekebisho yaliyobakia ya kamati ameyakubali na sisi kama wizara tunakubaliana nayo.

Hivyo, tunawaomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waipitishe sheria hii kifungu kwa kifungu wakati utakapofika, ili baada ya hapo Mheshimiwa Rais atakapoweka saini yake Baraza hili liweze kuanza na ufanisi upate kupatikana.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri ninakushukuru nawaona Waheshimiwa Wajumbe wanaharakia, ili waje kufanya maamuzi wanaingia kwa pamoja kwa ajili ya kufanya maamuzi.

Pia, nichukue nafasi kukushukuru sana Mhe. Waziri pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine wote ambao mumechangia mswada huu, lakini hasa zaidi wale ambao wamesaidia kutoa ufafanuzi wa hapa na pale, ili tuweze kufanya maamuzi yaliyo sahihi juu ya mswada huu ambao wengi wa Waheshimiwa Wajumbe wamesema kwamba mswada huu unatuhusu karibu sote tuliopo hapa na wengine ambao hawapo hapa.

Hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe walioko nje waharakie, ili tuweze kufanya maamuzi kwa sababu hoja tayari imetolewa na Mhe. Waziri, ili kuweza kuwahoji Waheshimiwa Wajumbe tuone kama wanakubaliana na mswada huu au vyenginevyo.

Naomba Waheshimiwa Wajumbe walioko nje waharakie sana warudi humu ndani bado wapo nje na musiniambie hawapo kwa sababu wapo na waambieni waje.

Pamoja na kwamba wengine wako nje wanakuja wanaharakia, lakini nimethibitishiwa kwamba idadi ya Waheshimiwa Wajumbe waliopo ndani tunaweza kufanya maamuzi. *(Makofi)*

Baada ya hoja ya Mhe. Waziri wa Afya. Sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja.

## KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

### Mswada wa Sheria ya Wauguzi na Wakunga, 2014
### Sehemu ya Kwanza
### Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.

**Sehemu ya Pili**
**Kuanzishwa kwa Baraza**

Kifungu 3

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kifungu hiki nilizungumzia Baraza kuwa na haki ya kushtaki na kushtakiwa na nikatoa maelezo mengi kwamba hili Baraza ni la serikali na kwa sababu linahusu wakunga na wauguzi. Hivyo, inawezekana kabisa mzee au baba akapeleka mkewe kujifungua na ikatokea pengine kwa sababu *negligence* ya muuguzi au mkunga ikatokea kwamba bila ya kufanya utafiti ni kwamba ile *handling* ya mtoto pengine imesababisha mtoto kuwa zezeta au hata kufariki.

Je, inaposhtakiwa anashtakiwa *nurse* na malipo ni yake? Mahakamani pengine ikatokea kwamba kosa limetokea na kweli *nurse* au mkunga amefanya kosa na ikatolewa hukumu ya kulipa nani atalipa malipo haya iwe kama ni fedha au mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, sikupata maelezo au sikuyasikia vizuri kama imeelezwa popote pale katika hili. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi kwamba nani atawajibika kulipa gharama kama ilitokea kuna kifo na imetokea kwamba kwa ushahidi aliyesababisha kifo ni muuguzi au mkunga.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, katika masuala kama haya kuna mambo matatu kwanza yule mkunga au *nurse* anaweza akafanya kosa yeye mwenyewe kosa la *negligence* kutokana na yeye mwenyewe au kosa lile linaweza kuwa la *criminal* (jinai) au kosa lile mara nyengine au mara moja moja linaweza likawa ni la *civil*, lakini hasa haya mawili.

Sasa kama kosa alilolifanya linatokana na *negligence* yake mwenyewe au kosa alilolifanya linatokana na ile jinai yake yeye mwenyewe. Kwa hivyo, kosa lile atashtakiwa yeye kwa sababu yeye ndiye aliyehusika. Lakini wakati mwingine makosa kama haya yanaweza yakawa ni ya Baraza kutokana na mambo mbali mbali, sasa pale linashtakiwa Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pale *nurse* au mkunga huyu amefanya kosa lile wakati akiwa ndani ya kazi zake, yaani kwenye utaratibu wa shughuli zake na likatokea kosa lile ingawa atashtakiwa yeye, lakini mara nyingi hushtakiwa yeye pamoja na lile Baraza lenyewe na ikibidi kulipa kwa mfano, kwa sababu Baraza ndilo lililokuwa limemuajiri, basi Baraza wakati huo ndio litahitajika

lilipe, kwa sababu Baraza lilikuwa linamuajiri yeye kufanya ile shughuli na ile shughuli aliifanya vibaya.

Kwa hiyo, kama ameifanya yeye mwenyewe katika nyanja zake yeye mwenyewe wakati wa kulipa kutokana na *negligence* yake au *criminality* yenyewe yake yeye, hivyo yeye mwenyewe ndiye atakayelipa.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba mambo kama haya yanategemea mazingira ya kesi yalivyotokea. Kwa hiyo, yale mazingira ya kesi yalivyotokea ndio tunaweza tuka-*determine* kama Baraza lilipe au yeye mwenyewe kutokana na uzembe wake au ile *criminality* yake aliyofanya. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

**Mhe. Hamad Masoud Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Kifungu 3 Kuanzishwa kwa Baraza.
Kifungu 4

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Kwanza niseme kwamba majibu ambayo yametolewa na Mhe. Mwanasheria Mkuu nimeyasikia na nimeyazingatia na nimeyakubali. Lakini katika maelezo yake alisema kwamba kwa hapa tunaamua kubakisha neno Baraza badala ya Bodi na katika maelezo ambayo alikuwa ametoa alisema kwamba huku katika Bodi kulikuwa na utaratibu maalum, lakini katika Baraza hili tunakuja kwa utaratibu kama huu ambao tunao kwa sasa.

Je, hatuoni kwa kwa wingi wa Wajumbe hawa na uhalisi wa kipato chetu na ukiangalia kuna wajumbe ambao wanajirudia kama vile *section* (i) na (k), yaani ni hao kwa hao, kwa sababu (i) mwakilishi kutoka nje ya kada ya afya, lakini na (k) kuna wajumbe wawili kutoka kwa jamii. Kwa kweli, naona ndio lile kwa lile na wala hatuoni kwamba kwa kutumia kipengele hicho tukapunguza baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe hawa na wakawa katika idadi kama ile ambayo tunapendekeza kwamba wawe saba au sita na badala ya kuwa 11 kama walivyo sasa?

**Mhe. Mwenyekiti:** Ehee! Mhe. Waziri wa Afya.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu (i) katika marekebisho ya kamati kama watapitia wamerekebisha kilikosewa kidogo na sio nje ya kada, isipokuwa ilikuwa kada nyengine ya afya ndio tatizo liliopo. Kwa hiyo, labda marekebisho ya kamati hajayapitia vizuri, hivyo naomba

sana apitie marekebisho yaliyofanywa na kamati kwenye ukurasa wa pili wa karatasi iliyotolewa na kamati.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa.

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, tatizo langu sio neno lililotumika, isipokuwa tatizo langu ni wingi wa hawa wajumbe. Hivyo je, hatuoni kwamba tunayo sababu ya kupunguza wajumbe na wakawa saba au tisa kama ilivyokatika maeneo mengine?

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mwanasheria Mkuu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, namfahamu Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa. lakini kufuta au kuacha inategemea na sababu na ukitizama muundo wa Baraza lenyewe Wajumbe wale wote ambao wamewekwa kila mtu anaingia kwa nafasi yake maalum. Sasa Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa yeye sijui anaona katika wajumbe hao ambao wamependekezwa ni yupi hana umuhimu kuwemo katika Baraza hili. Lakini ukitizama ukiacha Mwenyekiti, kuanzia (b) mpaka (k) kila mtu anaingia kwa nafasi yake maalum.

Kutokana na hali hiyo, ushauri wangu ni kwamba usifute au kuacha kwa sababu tu ya wingi wa idadi au uchache wa idadi ambao ya waunda bodi. Lakini tufanye hivyo kwa kuwa na sababu za msingi ambazo sasa zitatupelekea kukubaliana na mapendekezo ambayo yanaletwa. Sasa hivi ilivyo Mhe. Mwenyekiti ni kweli watu wengi, lakini kwa *nature* ya chombo chenyewe nadhani hawa ambao wizara imewapendekeza wanatosha. *(Makofi)*

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Mwanasheria Mkuu leo ndio siku yake ya mwanzo na ndio anaanza mambo humu ndani naona bora tuendelee. *(Kicheko/Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

| | |
|---|---|
| Kifungu 4 | Muundo wa Baraza pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 5 | Kazi za Baraza pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 6 | Kamati za Baraza pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 7 | Kukasimu nguvu na kazi za Baraza pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 8 | Uteuzi na uwezo wa wakaguzi pamoja na marekebisho yake. |

**Sehemu ya Tatu**
**Uongozi na Wafanyakazi wa Baraza**

| | |
|---|---|
| Kifungu 9 | Uteuzi wa Msajili pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 10 | Kazi za Msajili. |
| Kifungu 11 | Naibu Msajili pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 12 | Maafisa na wafanyakazi wa Baraza. |
| Kifungu 13 | Uteuzi na majukumu ya Msimamizi pamoja na marekebisho yake. |

**Sehemu ya Nne**
**Usajili na Leseni**

| | |
|---|---|
| Kifungu 14 | Daftari la Usajili Wauguzi na Wakunga. |
| Kifungu 15 | Sifa za kuweza kusajiliwa pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 16 | Usajili wa muda. |
| Kifungu 17 | Usajili wa Mpito |
| Kifungu 18 | Leseni ya kufanya kazi ya Uuguzi na Ukunga |
| Kifungu 19 | Maombi ya ufundishaji wa Uuguzi na Ukunga |
| Kifungu 20 | Ukaguzi wa Mpango mafunzo ya Uuguzi au Ukunga. |

**Sehemu ya Tano**
**Masharti ya Nidhamu**

| | |
|---|---|
| Kifungu 21 | Msajili kupokea malalamiko |
| Kifungu 22 | Uchunguzi wa Baraza |
| Kifungu 23 | Uwezo wa Baraza kuhusiana na nidhamu |
| Kifungu 24 | Uwezo wa kukusanya ushahidi |
| Kifungu 25 | Kutokutii wito na kukataa kutoa ushahidi |
| Kifungu 26 | Kufutwa kwenye daftari la usajili |
| Kifungu 27 | Kurejesha cheti utakapoondosha usajili pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 28 | Rufaa dhidi ya kuthibitishwa kufanya kazi au kukutwa katika daftari la usajili pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 29 | Kulirejesha jina ambalo liliondoshwa. |
| Kifungu 30 | Vigezo vya kulirejesha jina kwenye daftari la usajili pamoja na marekebisho yake. |

**Sehemu ya Sita**
**Masharti ya Fedha**

| | |
|---|---|
| Kifungu 31 | Fedha za Baraza pamoja na mrekebisho yake |
| Kifungu 32 | Makadirio |

| | |
|---|---|
| Kifungu 33 | Hesabu na Ukaguzi pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 34 | Malipo ya Ada pamoja na marekebisho yake. |

**Sehemu ya Saba**
**Makosa na Adhabu**

| | |
|---|---|
| Kifungu 35 | Kufanya kazi kinyume na sheria pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 36 | Taarifa au waraka wa uongo pamoja na marekebisho yake. |
| Kifungu 37 | Uanzishwaji au utoaji wa mafunzo ya uuguzi au ukunga |
| Kifungu 38 | Kujinasibisha na kutenda kinyume na uhalisia |
| Kifungu 39 | Masharti yanayohusiana na uendeshaji kesi wa Baraza |
| Kifungu 40 | Kuajiri mtu asiyesajiliwa au kupewa leseni |
| Kifungu 41 | Kusaidia kutendeka kwa kosa pamoja na marekebisho yake |
| Kifungu 42 | Kumzuia au kumuwekea vikwazo mkaguzi |
| Kifungu 43 | Kujitangaza |
| Kifungu 44 | Adhabu ya jumla |

**Sehemu ya Nne**
**Masharti ya Jumla**

| | |
|---|---|
| Kifungu 45 | Kupeyana taarifa |
| Kifungu 46 | Kinga |
| Kifungu 47 | Uwezo wa kuweka miongozo |
| Kifungu 48 | Uwezo wa kutunga kanuni |
| Kifungu 49 | Yanayofutwa |

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mheshimiwa Spika, ilivyokuwa kamati ya kutunga sheria imeipitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuyakubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi:** Naafiki.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na Mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Wauguzi na Wakunga wa Mwaka 2014**

*(Kusomwa mara ya tatu)*

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Wakunga na Wauguzi ya mwaka 2014 usomwe kwa mara ya tatu.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na Mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Mswada wa Sheria wa Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe naangalia orodha ya shughuli za leo inaonekana mmezimaliza nawapongeza sana *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa kazi zilizokuwepo katika orodha ya shughuli za leo zimemalizika kwa ufanisi mkubwa, naomba nichukue nafsi hii kwanza kuwashukuru kwa kazi nzuri na mashirikiano makubwa tuliyopeyana kiasi cha kupitisha mswada huu hivi punde bila ya vikwazo vyovyote. Nachukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na Mawaziri kwa ufafanuzi mzuri uliotolewa katika Mswada huu, kwa maana hiyo basi sasa tusitishe shughuli zetu ili tukutane tena, kesho tarehe 23/10/2014 saa 3.00 asubuhi.

Kwa hivyo Kikao hichi nakiahirisha hadi kesho tarehe 23/10/2014 mwaka huu saa. 3.00 za asubuhi.

*(Saa 1.07 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 23/10/2014 saa. 3.00 asubuhi)*